

**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA SITA**

**Kikao cha Nane - Tarehe 18 Juni, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Bodi Ya Tumbaku kwa Mwaka unaoishia Tarehe 31 Machi, 2003 *(The Annual Report and Accounts of the Tanzania Tobacco Board for the Year ended 31<sup>st</sup> March, 2003).*

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Bodi ya Pamba na Mbegu kwa Mwaka Ulioishia tarehe 30 Juni, 2003 *(The Annual Report and Audited Accounts of the Tanzania Cotton Lint and Seed Board for the Year ended 30<sup>th</sup> June, 2003).*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 69

**Mabaraza ya Ardhi Vijijini**

**MHE. LEKULE M. LAIZER** aliuliza:-

Kwa kuwa katika utaratibu wa ardhi ya Vijiji, kila Kijiji kinatakiwa kuunda Mabaraza ya Ardhi kwa ajili ya kusuluhisha migogoro ya ardhi Vijijini na kwa kuwa migogoro ya ardhi ilikuwepo kila mara hata kabla ya kutungwa kwa Sheria ya Ardhi Vijijini:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba imechelewa kuanzisha Mabaraza hayo?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kuwaelimisha wananchi juu ya jambo hilo ili utekelezaji wake uanze kuliko kuyaacha mambo hayo kwenye maandishi tu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lekule Michael Laizer, Mbunge wa Longido, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, uamuzi wa kuanzisha Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji ulitokana na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999. Sheria hii inazielekeza Serikali za Vijiji kuunda Mabaraza ya Vijiji kwa madhumuni ya kutatua migogoro ya ardhi katika ngazi hiyo badala ya Mahakama za Mwanzo. Aidha, Sheria Na. 2 ya Mwaka 2002 ya Mahakama za Ardhi (*The Land Disputes Court Act, 2002*) inatoa ufafanuzi wa kina juu ya utaratibu, Mamlaka ya uundaji wa Mabaraza hayo na majukumu ya vyombo vinavyohusika na utatuzi wa migogoro ya ardhi ikiwa ni pamoja na Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji. Kufuatia Tangazo la Serikali Na. 223 la tarehe 8 Agosti, 2003 lililotolewa na Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Sheria Na. 2 ya 2002 imeanza kutekelezwa rasmi tarehe 1 Oktoba, 2003. Pamoja na maandalizi hayo, Wizara yangu pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, pamoja na Waziri wa Ardhi, tumeshirikiana kufanya tafsiri ya Sheria pamoja na kanuni zote zinazohusiana na masuala haya ya ardhi na sasa Halmashauri zimeshaanza kutekeleza sheria hiyo na tukitoa mifano hasa ya Rungwe, Bariadi na Monduli. Katika Halmashauri ya Monduli, Vijiji 36 kati ya 72 vimekwishaunda Mabaraza hayo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na taratibu nilizoielezea, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, Serikali imechelewa kuanzisha Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji tangu Sheria Na. 5 ya mwaka 1999 ilipopitishwa. Hata hivyo, ilikuwa ni muhimu kwa Serikali kuelekeza juhudi kwanza katika kufafanua na kutafsiri sheria ili iwe rahisi kueleweka kwa jamii wakati Mabaraza hayo yanapoundwa na Mabaraza yenyewe kuelewa vema majukumu yake, hivyo kufanya kazi kwa ufanisi na tija. Aidha, Serikali ilikwishaanzisha utaratibu wa Mabaraza ya Kata, ambayo pamoja na mambo mengine, yanayo majukumu vile vile ya kusikiliza rufaa za migogoro ya ardhi ngazi ya Vijiji.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inalo jukumu la kwanza la kuwaelimisha wananchi juu ya uundaji na uendeshaji wa Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji kwa ufanisi. Ofisi yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, pamoja na Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, inaandaa mwongozo wa kuwaelimisha wananchi kuhusu Sheria ya Mahakama za Ardhi. Aidha, waraka unaandaliwa na Ofisi yangu kuzielekeza zaidi Halmashauri juu ya Mabaraza haya. Kutokana na sheria hii inatarajiwa kwamba, mazingira katika Vijiji yataboreka zaidi kama wananchi wataelewa vyema sheria hiyo.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa tangu sheria hii ipitishwe mpaka sasa bado hayo Mabaraza hayajapata semina jinsi ya kuongoza, ni lini basi Serikali itachukua muda huo kwenda kuelimisha hayo Mabaraza ili watekeleze wajibu wao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, maandalizi yanakamilishwa kwa maana ya kuandaa miongozo mbalimbali, lakini la msingi zaidi lilikuwa ni kuweka kwanza sheria zenyewe katika lugha ya Kiswahili ambayo inaeleweka vizuri zaidi. Nina hakika baada ya muda si mrefu, juhudi hizo za kuanza kutoa elimu zitaanza.

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, Waziri atalieleza Bunge hili nani anawajibika kugharamia uendeshaji wa Mabaraza haya? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, Sheria zote ambazo zilipitishwa na Bunge hili zimeweka utaratibu mahsusi kabisa wa namna ya kusimamia Mabaraza haya katika ngazi za Vijiji na hizo ndio zitakazotumika.

**SPIKA:** Maswali mafupi mafupi kama haya ndiyo yanayotakiwa na kanuni zetu. Kwa hiyo, kuna nafasi nyingine. Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa nilikuona, maswali mafupi mafupi. (*Makofi*)

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, swali langu lilihusiana na hilo lakini sehemu ya pili yake bado halijajibiwa, kwa hiyo naomba niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mabaraza haya hayajaanza kazi na Baraza la Ardhi la Wilaya lililokuwepo bado linaendelea. Je, Waziri sasa ataeleza nini kwamba mwisho wa Mabaraza yale ya zamani utakuwa lini na haya mapya yanategemewa kuanza lini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taratibu zilivyo, Mabaraza haya yalipewa *transition period* ya miaka miwili ili kuweza ku-*handover* majukumu haya mengine kwenye Mabaraza ya Vijiji kwa ubora zaidi.

Na. 70

### **Utekelezaji Sahihi wa Mpango na Maagizo ya Kitaifa**

**MHE. MBARUK K. MWANDORO** aliuliza:-

Kwa kuwa mara nyingi panakuwepo na pengo baina ya malengo, mipango na mikakati ya Kitaifa ya maendeleo na hali halisi ya kimipango na kiutekelezaji katika ngazi za Wilaya na Vijiji na mfano hai ni matarajio ya kuwepo kwa mazao maalum ya kiuchumi na ya chakula kwa kila Wilaya, hali halisi ya ukosefu wa mipango hiyo na hatua thabiti za utekelezaji wa mipango inayotarajiwa:-

(a) Je, Serikali inatambua kwamba mara nyingine viongozi katika Halmashauri za Wilaya na Serikali za Vijiji hawazingatii ipasavyo au wanapuza tu maagizo muhimu kutoka ngazi za juu?

(b) Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuhakikisha kuwa mtiririko na utekelezaji sahihi na ulio thabiti wa mipango na maagizo ya Kitaifa ya kuendeleza sekta mbalimbali za kiuchumi na huduma za jamii hadi kufikia ngazi za Wilaya au Vijiji unasimamiwa ipasavyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbaruku Kassim Mwandoro, Mbunge wa Mkinga, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria za Serikali za Mitaa Namba 7 inayohusiana na Mamlaka za Wilaya na Namba 8 ya Mamlaka za Miji za mwaka 1982, Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na mengineyo zinao wajibu wa kusimamia na kutekeleza sera, mikakati, sheria, taratibu na miongozo mbalimbali ya kisekta.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia majukumu ya kisheria ya Serikali za Mitaa, Serikali inatambua kuwepo kwa baadhi ya viongozi ikiwa ni pamoja na watendaji wake, kutozingatia kikamilifu maagizo na maelekezo yanayotolewa na Serikali Kuu na hata maamuzi halali ya Mabaraza ya Madiwani ya Halmashauri na Mikutano Mikuu ya Vijiji. Pale ambapo imebainika kukiukwa au kupuzwa kwa maelekezo au maagizo yanayotolewa na Mamlaka halali, hatua zinazostahili kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizopo huchukuliwa. Kwa mfano, Juni, 1996 Serikali ililazimika kuvunja Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na mara kwa mara kusimamisha, kukemea na kufukuza watendaji wa ngazi mbalimbali katika Utumishi wa Serikali za Mitaa. Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 43(5) cha Sheria Na. 9 ya mwaka 1992 ya Fedha za Serikali za Mitaa, Baraza la Madiwani la Halmashauri linalo jukumu la kuhakikisha shughuli za Halmashauri zinatekelezwa na kumwajibisha mtendaji mkuu au mtumishi mwingine pale anaposhindwa kutekeleza wajibu wake.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inazo taratibu zilizokubalika kisheria katika kuwezesha mitiririko wa mawasiliano na utekelezaji wa mipango na maagizo ya Kitaifa hadi ngazi ya Vijiji. Taratibu hizo ni pamoja na kuwepo kwa miundo ya Wizara, Mikoa, Wilaya na Serikali za Vijiji, ambazo zina uhusiano wa kirasimu toka juu hadi chini unaoleta uwajibikaji. Utaratibu huu unahakikisha maelekezo ya Serikali yanawafikia wahusika, yanatekelezwa, yanafuatiliwa na yanatolewa taarifa. Aidha, upo pia utaratibu wa kupitisha maamuzi na maagizo kuanzia Baraza la Mawaziri kwenda Wizara husika, Mikoa hadi Wilaya, kwa maana ya Serikali na Halmashauri. Mfumo huu pia unasisitiza ufuatiliaji wa maagizo na utoaji wa taarifa. Vile vile, sheria mbalimbali zinazotungwa na Wizara na Halmashauri, zinalenga kusimamia utekelezaji wa sera, maagizo na mipango inayoandaliwa. Kupitia sheria zilizotungwa, miongozo na nyaraka mbalimbali za Serikali, wananchi wanazo haki zote kufuatilia na kuuliza au kwa upande wa Mabaraza ya Madiwani kumchukulia hatua mtumishi mzembe.

Mwisho ni mfumo uliopo kuanzia ngazi ya Taifa, Wilaya na hadi Vijijini. Mfumo huu unawawezesha viongozi hawa kutoa maelekezo na ufafanuzi wa miongozo mbalimbali na maagizo ya Serikali.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kusema kwamba hivi sasa Serikali inafanya jitihada kubwa kufanya maboresho na vile vile tunajua kwamba ushindani ni kichocheo kikubwa cha maendeleo. Je, huu si wakati muafaka kwa Serikali kufikiria kuweka utaratibu rasmi wa ushindani kati ya Vijiji na Vijiji na Wilaya na Wilaya ili kuweza kusukuma maendeleo kwa haraka zaidi? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, upo utaratibu wa kushindanisha Vijiji na Vijiji na ni utaratibu wa siku nyingi. Tatizo linalotokea ni kwamba, maeneo mengi Wilayani hawazingatii maagizo ya Serikali ya kufanya ushindani huu wa kimaendeleo, lakini tutaendelea kulihimiza kwa sababu ni jambo zuri na linafanyika katika maeneo mengi.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Serikali za Mitaa, swali hili na majibu hayo yalikuwa na msingi wa mtiririko (*Chain of Command*) na Waziri amekiri kwamba, kuna maagizo yanatolewa Kitaifa. Sasa *chain of command* kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, maafisa waliopo Serikali za Mitaa hawana maafisa wa ngazi za Kitaifa katika Serikali za Mitaa wanaotoka Wizara zingine. Sasa pamoja na kuwa Serikali ina macho kama chandarua, inaweza kuona kila mahali na maeneo yote na mahali popote, je, mnaweza mkaweka maafisa wa sekta mtambuka katika Wizara ya Serikali za Mitaa ili *chain of command* iende moja kwa moja hadi kumfikia afisa wa Serikali za Mitaa kwa utekelezaji sahihi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kwa sababu tu labda Mheshimiwa Pawa hakupata nafasi ya kuzungumza na sisi tukajaribu kumpa maelezo ya *set up* ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Ni jumuisho la wataalam kutoka sekta karibu zote na ndiyo wenye jukumu la kusaidia kusukuma maendeleo katika Halmashauri zetu.

Na. 71

### **Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi**

**MHE. PETER KABISA** aliuliza:-

Kwa kuwa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MEM) unaendelea vizuri kote nchini na unaendelea kupunguza idadi kubwa ya watoto kwenda darasa moja kutoka wanafunzi kati ya 80 na 100 na kufikia idadi ya wanafunzi 40 hadi 45 kwa darasa ifikapo mwaka 2005/2007 na kuendelea na kwa darasa la saba ni dhahiri kwamba wanafunzi wengi watafaulu kwa urahisi kuingia kidato cha kwanza wengi wao wakiwa na umri wa miaka 14 kwa wale watakoingia darasa la kwanza wakiwa na miaka saba:-

(a) Je, Serikali kwa kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa *ILO* unaokataza watoto wenye umri chini ya miaka 18 wasijajiwe kufanya kazi nzito, haioni kwamba kutakuwa na idadi kubwa ya watoto wa umri wa miaka 14 ambao kama hawakuchaguliwa kuendelea na masomo kwa sababu mbalimbali itabidi wajajiri wenyewe na hivyo kuvunja miiko ya Mkataba huo?

(b) Je, Serikali kwa kuheshimu Mkataba huo, haioni kwamba kuna haja ya kuunda sera mpya ya elimu yenye lengo la kumsomesha mtoto bure hadi kidato cha nne ili atakapomaliza awe na umri wa miaka 18 ambao utamwezesha kujitegemea na kujiajiri mwenyewe?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Peter Kabisa, Mbunge wa Kinondoni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali imeridhia Mkataba wa Kimataifa wa *ILO* kuhusu kutoajiri watoto wenye umri chini ya miaka 18 kufanya kazi nzito. Aidha, ni kweli pia watoto wengi humaliza elimu ya msingi wakiwa na umri wa miaka 14 na wengi hawachaguliwi kuendelea na masomo ya elimu ya sekondari kutokana na matatizo mbalimbali ikiwa ni pamoja na uwezo mdogo wa kifedha wa wazazi na nafasi chache katika shule za sekondari za Serikali. Kwa kutambua hilo, Serikali imeandaa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES 2004 - 2009) wenye lengo la kupanua na kuboresha elimu ya sekondari unaoanza kutekelezwa mwaka huu wa fedha. Katika mpango huo elimu ya sekondari itapanuliwa ili kufikia mwaka 2010 asilimia 50 ya watoto wanaomaliza elimu ya msingi waweze kupatiwa nafasi ya kuendelea na elimu ya sekondari. Aidha, inategemewa mafunzo ya ufundi kupitia *VETA* chini ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, yatapanuliwa ili wanafunzi wengi wanaomaliza elimu ya msingi, wapate nafasi ya kujifunza ufundi. Hatua hizi mbili zinazochukuliwa na Serikali zitapunguza kwa kiasi kikubwa watoto wanaobakia nyumbain baada ya elimu ya msingi. Lengo la Serikali ni kuendelea kupanua elimu ya sekondari baada ya mwaka 2009 mpaka iwe kwa watoto wetu wote.

(b) Mheshimiwa Spika, kumsomesha mtoto bure maana yake ni kutafuta vyanzo vingine vya kugharamia elimu ya mtoto huyo pasipo kumhusisha mtoto mwenyewe wala wazazi wake. Kwa kuwa elimu ya sekondari ina faida kwa mpokeaji wa elimu hiyo, inabidi mwenye uwezo achangie kulipia kwa sababu ina faida kwake. Hata hivyo, Serikali tangu mwaka 2003 imeanza kugharamia elimu ya sekondari kwa watoto 6,000 kwa mwaka wanaotoka kwenye familia maskini ili nao waipate. Katika MMES 2004 - 2009 bajeti ya mwaka huu kwa ajili hii itaongezwa mara dufu na aidha, Serikali inadhamiria kupunguza ada za sekondari kama nitakavyofafanua katika hotuba yangu ya bajeti. *(Makofi)*

**MHE. PETER KABISA:** Mheshimiwa Spika, kwa leo nimeridhika ahsante sana.

**MHE. DR. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Serikali ina mpango wa kusomesha watoto wote wafike sekondari na kwa kuwa wakati huo huo watoto wa kike wanaopata mimba kabla ya kumaliza sekondari wanafukuzwa. Je, ikiwa mpango huo ukikubalika watoto hao wanaopata mimba wataweza kuruhusiwa kumaliza masomo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, suala la kuruhusu watoto waliopata mimba waweze kuendelea na elimu kama kawaida ni jambo ambalo lipo katika uwezo wetu hapo tutakapokuwa tunaridhika kwamba maadili yetu katika jamii yanakubali na yanapenda hivyo. Kwa utaratibu wa sasa ambao nimeufafanua mara nyingi katika Bunge hili, kosa la kupata mimba shuleni ni uvunjaji wa maadili ambayo ni sababu mojawapo inayotaka mwanafunzi aachishwe shule. Endapo tutalionga badiliko lazima tujue kuna kiumbe wa pili amekwishakuja duniani ambaye kama tunataka yule mama yake arudi shuleni lazima pia tuweke utaratibu wa malezi kwa yule kiumbe wa pili. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda kufafanua kwamba, mimi kama Waziri wa Elimu, nasikiliza sana maoni, lakini maoni ya jamii huwezi kuyasikiliza kutoka kikundi kimoja cha vijana tu. Ningependa katika midahalo hiyo ya maoni siku nyingine wachukuliwe pia Masheikh, Wachungaji na Mapadri ili nao tupate maoni yao, kwa sababu ni sehemu ya uongozi wa jamii. *(Makofi)*

Na. 72

### **Ongezeko la Wanafunzi Wanaofaulu Mitihani ya Darasa la Saba**

**MHE. MUSA A. LUPATU** aliuliza:-

Kwa kuwa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi umeanza kuimarika kwa kiwango kikubwa cha ubora wa elimu itolewayo katika shule za msingi kote nchini na kwa kuwa katika azma hiyo uandikishaji wa watoto wenye umri wa kuanza shule umeimarika na wastani wa alama za kufaulu darasa la saba umepanda:-

(a) Kwa kuwa matokeo hayo mazuri yatasababisha miaka ijayo nchi yetu iwe imefuta ujinga wa kutojua kusoma na kuandika hivyo kuifanya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW) kupoteza sifa yake ya awali, je, ni nini mustakabali wa Taasisi hiyo?

(b) Je, Serikali imejiandaa vipi kukabiliana na ongezeko la watoto wanaofaulu kwenda sekondari, badala ya mtindo wa dharura kama ilivyotokea kwa watoto waliomaliza darasa la saba mwaka 2003?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimwa Musa Lupatu, Mbunge wa Korogwe Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimwa Mbunge kuwa, matokeo mazuri ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MEM) yameanza kuonekana kwa kiwango kikubwa cha ubora wa elimu itolewayo katika shule za msingi. Wanafunzi wanaofaulu mtihani wa darasa la saba wameongezeka kutoka asilimia ishirini na mbili mwaka 2000 hadi asilimia 40.1 mwaka 2003. Mojawapo ya mafanikio ya MEM 2002 - 2006 ni kuziba bomba linalotoa watu wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu, kwa kufanikisha uandikishaji darasa la kwanza wa watoto wote wa miaka saba kwa kila mwaka na kuhakikisha wanabakia shuleni mpaka wahitimu darasa la saba.

Mheshimiwa Spika, kuboreshwa kwa elimu ya msingi, hakupotezi sifa ya awali ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kwa sababu Taasisi hiyo haikuundwa kwa ajili ya kutoa elimu ya msingi kwa vijana nje ya shule na watu wazima wasiojua kusoma na kuandika tu, lakini pia TEWW ina majukumu ya kuendelea kutoa elimu ya kujiendeleza kwa mfumo usio rasmi. Aidha, TEWW hutoa elimu hiyo kwa njia ya Posta na madarasa ya jioni ya ana kwa ana. Kwa mfumo huu, mafunzo ya ualimu ya ngazi ya cheti na stahhada ya EWW hutolewa. Kwa sababu hiyo umuhimu na makusudio ya TEWW inayoendelea katika maisha yote (*Life Long Continuing Education*) yataendelea kuwepo.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kupita Wizara yangu imeanza kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MES) 2004 - 2009 wa miaka mitano kwa lengo la kupanua na kuboresha elimu ya sekondari ili kukabiliana na ongezeko la watoto wanaofaulu kuendelea na masomo ya sekondari. Katika kutekeleza mpango huo, Serikali itaongeza majengo muhimu yanayotakiwa kukamilisha shule zilizopo sambamba na kujenga sekondari mpya 1,500, kuongeza mikondo katika shule zilizopo, kuajiri walimu na kuongeza vifaa vya kufundishia na kujifunzia na ndiyo maana katika bajeti ya mwaka huu wa 2004/2005, zimetengwa shilingi bilioni 53 kwa ajili ya makusudio hayo ya kufanya hayo niliyoyaeleza. Aidha, mwaka huu Wizara yangu imekwishatoa vibali kwa shule mpya 90 za sekondari na kuongeza jumla ya mikondo 128 kwa madhumuni hayo. (*Makofi*)

**MHE. MUSA A. LUPATU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Namshukuru Waziri kwa majibu yake mazuri lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza, kwa kuwa ipo tofauti kubwa sana kati ya Mkoa na Mkoa kwa idadi ya shule za sekondari zilizopo. Je, katika mpango unaofuata wa MES, Serikali itatumia vigezo gani kuhakikisha kwamba usawa unapatikana katika mtawanyo wa sekondari zilizopo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kuwa kutakuwa na ongezeko kubwa la shule za sekondari, moja ya tatizo ambalo linatokea katika ubora wa elimu ya sekondari inayotolewa ni ukosefu wa mafunzo kwa walimu wakuu wa shule za sekondari. Je, Serikali inajiandaa vipi kuhakikisha kwamba walimu wakuu wa sekondari wanapata mafunzo ya uongozi na uendeshaji? (*Makofi*)

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, katika mpango huu wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari, mambo mawili yamelengwa kufikiwa. Moja, ni kufikia usawa wa utoaji wa elimu kwa jinsia zote na la pili ni utoaji wa elimu ya



sekondari kwa usawa kwa Wilaya na Mikoa yote yaani na vigezo hivyo vitatumika ili kuhakikisha kwamba hizo sekondari mpya zinakwenda katika maeneo ambako hazipo sekondari yaani *under-served areas*. Utaratibu wake Wizara inauandaa, tutaufafanua na Waheshimiwa Wabunge wanaweza kugawiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili kwamba, katika mpango huo wa MMES ni pamoja na kupanua kwa kiwango kikubwa sana mafunzo kwa ajili ya walimu wa sekondari, yaani wale wenye *Degree* za Chuo Kikuu na wale wenye *Diploma* na ndani ya mpango huo Vyuo vya Ualimu viwili vitabadilishwa kuwa Vyuo Vikuu Vishiriki vya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ili vitoe *Diploma* lakini pia vitoe *Degree* za Chuo Kikuu katika Vyuo hivyo. Kwa hiyo, mambo hayo yote yameshughulikiwa katika mpango. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ameahidi kufafanua zaidi katika hotuba yake ya bajeti, bora tusebiri hiyo. Sasa tuendeleo na maswali kwa Wizara ya Kilimo na Chakula.

Na. 73

### **Kilimo cha Mboga - Dodoma Vijijini**

**MHE. WILLIAM J. KUSILA** aliuliza:-

Kwa kuwa sehemu nyingi za Wilaya ya Dodoma Vijijini zinafaa sana kwa kilimo cha mboga kama vile nyanya, vitunguu, kabichi, mchicha, pilipili na kadhalika lakini hakuna mikakati yoyote ya kukiimarisha na kukiendeleza kilimo hicho:-

(a) Je, kwa nini Serikali haitilii maanani kilimo hicho katika Mkoa wa Dodoma hususan Wilaya ya Dodoma Vijijini?

(b) Je, Serikali itawasaidiaje vijana katika sehemu mbalimbali za Wilaya ya Dodoma Vijijini ambao wangependa kujishughulisha na kilimo hicho lakini wanashindwa kutokana na matatizo mbalimbali hasa ya ukosefu wa mitaji na maji kwa ajili ya umwagiliaji?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa William Jonathan Kusila, Mbunge wa Bahi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Kusila kwamba, Serikali inalipa suala la kilimo cha mboga na matunda umuhimu wa juu iwezekanavyo kwa kuzingatia mazingira ya Wilaya ya Dodoma Vijijini. Taarifa tulizonazo zinaonyesha kwamba, kilimo cha mboga na matunda kinafanyika kwenye Vijiji kumi na sita ambavyo vililima hekta 301 za mboga na matunda katika msimu wa 2003/2004. Vijiji hivyo vina visima vifupi 107, mabwawa matatu na chemichemi tatu.

Uzalishaji wa mboga na matunda katika Wilaya ya Dodoma umekuwa ukiongezeka kwa kasi nzuri katika miaka mitatu iliyopita. Katika mwaka wa 2001/2002, inakisiwa kwamba, Wilaya hiyo ilizalisha tani 3,362 na tani 3,790 katika mwaka wa 2003/2004. Hili ni ongezeko la asilimia 31 katika miaka hiyo mitatu.

Aidha, Wilaya ina vikundi sitini vilivyoanzishwa kuzalisha mboga na matunda kwenye maeneo yasiyokuwa na chemichemi. Vikundi ishirini kati ya hivyo vinaendelea kujishughulisha na kilimo hicho kwa kutumia visima virefu 25 na pampu za miguu 29.

Katika mwaka wa 2003/2004, hatua nyingine zinazochukuliwa na Serikali, ni pamoja na ukarabati wa Bwawa la Buigiri ambalo litawapatia wananchi maji ya kumwagilia eneo lenye ukubwa wa hekta 55 na kunyweshea mifugo. Ukarabati wa bwawa hilo unakisiwa kugharimu shilingi bilioni 238.9.

Chini ya Progamu Shirikishi Jamii ya Umwagiliaji Maji Mashambani, Mradi wa Umwagiliaji wa Mtitaa unakarabatiwa kwa gharama ya shilingi bilioni 326 na ukarabati utakapokamilika eneo lenye ukubwa wa hekta 106 litamwagiliwa maji. Aidha, programu hiyo imechimba visima vifupi tisa katika vijiji saba, kisima kimoja kimoja kwenye vijiji vya Mpwayungu, Mtitaa, Uhela, Chipanga na Bahi na visima viwili viwili kwenye vijiji vya Chali na Chikopelo. Visima vingine 53 vilikwishachimbwa katika Vijiji vya Chipanga, Chali na Chikopelo.

Programu Maalum ya Uhakika wa Chakula (*Special Program for Food Security*) imechimba visima vifupi vinne na kutoa pampu ndogo za mkono 19 kwa wakulima katika Vijiji vya Chalinze, Chipanga na Bahi.

Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la *World Vision*, inafanya uchunguzi wa uwezekano wa kujenga bwawa katika kijiji cha Chipanga litakalotumika kumwagilia maji mashamba ya mpunga na bustani za mboga.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuwezesha vijana kupata mikopo ya kuendesha shughuli zao za kujijaji. Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, hutoa mikopo midogo midogo kwa madhumuni hayo na Halmashauri za Miji na Wilaya zimeagizwa kutenga asilimia kumi ya mapato yao kwa ajili ya kuvikopesha vikundi vya wanawake na vijana. Chini ya utaratibu huo, katika mwaka wa 2002/2003, Wilaya ya Dodoma ilitoa mikopo kwa vikundi sita vya vijana yenye jumla ya shilingi milioni 1.7 kwa ajili ya kilimo cha mboga.

**MHE. WILLIAM J. KUSILA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Sasa hivi nimefurahishwa sana na majibu ya sehemu (a) ya swali langu. Serikali inatoa tamko kwamba inatilia maanani kilimo cha mboga mboga katika Wilaya ya Dodoma Vijijini. Lakini sikuridhishwa na jibu la sehemu (b).

Kwa kuwa tatizo kubwa linalowakabili vijana katika Mradi huu wa Kilimo cha mboga mboga zaidi ni tatizo la maji na kama Mheshimiwa Naibu Waziri alivyosema

katika jibu la sehemu (a) ya swali langu ni vijiji 16 tu kati ya vijiji 128 vya Wilaya hii ambavyo kilimo cha mboga mboga kimeimarika kwa sababu vina maji. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, atakubaliana nami kwamba namna pekee ya kuwasaidia vijana katika kilimo hiki ingelikuwa ni kuhakikisha kwamba kuna malambo katika vijiji vyote 128 vya Wilaya ya Dodoma Vijijini? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, napenda nikubaliane naye kwamba, katika Wilaya ya Dodoma Vijijini na karibu Mkoa mzima hauna tatizo la upatikanaji wa maji. Sasa kwa ufinyu wa bajeti uliopo, tulichoweza kufanya ni hicho. Laiti tungeweza kuwa na uwezo mkubwa zaidi tungependa kufikia azma hiyo. Lakini pamoja na hayo, tunamwomba Mheshimiwa William Kusila, ajaribu kuvuta subira, kwa sababu mwaka huu kuna mipango ambayo itahusu vilevile Mkoa wa Dodoma na penginepo na Wilaya ya Dodoma Vijijini itahusishwa.

Na. 74

### *Ngono Project*

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA** aliuliza:-

Kwa kuwa kilimo cha umwagiliaji ni muhimu katika harakati za kupambana na umaskini vijijini na kwa kuwa Serikali ilionyesha nia ya kufufua *Ngono Project* pamoja na kuweka miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji katika mabonde mbalimbali Mkoani Kagera.

Je, Serikali imechukua hatua zipi za kufufua *Ngono Project* na kuweka miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji katika Mkoa huo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Diodorus Buberwa Kamala, Mbunge wa Nkenge, kama ifuatavyo:-

Mwaka 1956, Serikali ilifanya upembuzi yakinifu wa Bonde la Mto Ngono kwa kutumia Kampuni ya *Sir Alexander Gibb and Partners Africa* na kubaini kuwa, Bonde hilo lina eneo lenye ukubwa wa hekta 21,000 linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji maji mashambani.

Aidha, upembuzi yakinifu huo ulibaini kuwa pamoja na kuendeleza kilimo, Bonde la Mto Ngono lingeweza kuendelezwa kwa manufaa makubwa zaidi kwa Taifa kwa kujenga mabwawa makubwa mawili. Bwawa moja kwa ajili ya kuzalisha umeme na bwawa lingine kwa ajili ya kudhibiti mafuriko ambayo mara kwa mara yanaathiri makazi ya wananchi na shughuli zao za maendeleo, kikiwemo kilimo. Mwaka 1975, gharama za kuendeleza bonde hilo zilikadiriwa kuwa shilingi milioni 192.5, sawa na dola za Kimarekani milioni 27.5. Gharama hiyo ilikuwa kubwa kuliko uwezo wa Serikali.

Serikali imekuwa inafanya juhudi za kuendeleza mradi wa umwagiliaji wa Ngoni, hususan kupitia Mpango wa Ushirikiano wa Matumizi ya Maji ya Mto Nile (*Nile Basin Initiative*). Mpango huo unaojumuisha nchi kumi ambazo mto Nile unapita ikiwemo Tanzania. Aidha, Mpango wa *Nile Basin Initiative* unaandaa Mradi wa Uendelezaji wa Mabonde ya Mto Mara na Kagera utakaojumuisha miradi ya kilimo cha umwagiliaji maji mashambani.

Ripoti ya Mkandarasi aliyefanya upembuzi yakinifu katika mabonde ya mito ya Mara na Kagera, Kampuni ya *M/S SWECO and Associate* ya Sweden Novemba, 2003, inaonyesha kwamba, kuna uwezekano wa kujenga bwawa moja moja katika kila nchi za Maziwa Makuu na kuendeleza skimu ndogo za kilimo cha umwagiliaji maji mashambani katika mabonde ya mito Mara na Kagera. Serikali inachunguza uwezekano wa kuingiza ujenzi wa skimu ya umwagiliaji ya Nkenge katika Mradi wa Kuendeleza Mabonde ya Mito ya Mara na Kagera. Nitamjulisha Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, skimu zitakazotekelezwa katika mradi huo mara uchambuzi utakapokamilika na kufikia hatua ya utekelezaji.

Aidha, Mpango Kamambe wa Taifa wa Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani tayari umechambua skimu zote zilizopo katika Mkoa wa Kagera, zikiwemo skimu zilizoko kwenye Bonde la Mto Ngoni. Skimu hizo ambazo zinahitaji kujengewa miundombinu ya umwagiliaji maji mashambani ni kama ifuatavyo: Mwiruzi yenye ukubwa wa hekta 300 katika Wilaya ya Ngara, Busaka, Chato/Itare na Buzirayombo zenye jumla ya hekta 425 katika Wilaya ya Biharamulo na Kagenyi, Kijito cha Mwisa, Kijumbura na Buyaga zenye hekta 310 katika Wilaya ya Karagwe. Skimu nyingine ni Kyota na Ruhanga zenye ukubwa wa hekta 400 katika Wilaya ya Muleba.

Bonde la Mto Ngoni linajumuisha skimu za Kyakakera hekta 3,000, Nkenge hekta 2,600 na Kajunguti hekta 3,800 ambazo ziko katika Wilaya ya Bukoba Vijijini.

Katika mwaka wa 2003/2004, Serikali imetumia shilingi milioni 20 kukarabati sehemu ya skimu ya umwagiliaji ya Nkenge na kufanya eneo linalolimwa sasa kuwa hekta 32. Halmashauri za Wilaya katika Mkoa wa Kagera zinashauriwa kuchambua skimu zilizotajwa na kuzijumuisha katika Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya ili ziombewe fedha.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pia namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

(a) Kwa kuwa inaonekana mipango imekuwepo tangu mwaka 1956 kabla hata mimi sijazaliwa na hadi sasa Mheshimiwa Naibu Waziri anaendelea kutueleza mipango. Je, ni lini anaweza akawaeleza wananchi wa maeneo hayo kwamba sasa tunatoka kwenye mipango tunakwenda kwenye utekelezaji?

(b) Kwa kuwa ulikuwepo mpango wa *Kagera Water Basin* ambao hivi sasa haijulikani kama unaendelea au umekufa na haijulikani ni nani alichukua mali hizo. Je, Serikali inaweza ikatoa tamko lolote juu ya *Kagera Water Basin*? (Makofi)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo ni kuwa sasa hivi kinachofanyika ni kuhakikisha ile mipango inatekelezeka kwa kupata fedha. Sasa Wizara inafanya kila inaloweza kupata Wahisani wale wa siku zote kwa miradi mingine nchini.

La pili, kuziomba au kuzihamasisha Halmashauri za Mkoani Kagera kuhakikisha kwamba wanaweka miradi hiyo katika bajeti zao ili iweze kutekelezeka.

Mheshimiwa Spika, sasa kuhusu mipango ya *Kagera Water Basin* iliyokuwepo huko nyuma, lazima nikiri kuwa kwa sasa mkazo mkubwa zaidi upo katika *Nile Basin Initiative*, kwa maana kuwa hizo nchi 10 zina miradi ya uhakika zaidi ya utekelezaji. Kwa sababu tatizo kubwa siyo kutokutaka, lakini tatizo kubwa ni ufinyu wa bajeti na siyo miradi ya Kagera tu ni ya nchi nzima.

Kwa sababu kama nilivyosema tuna *Master Plan ya Irrigation* ya nchi nzima, lakini tunashindwa kuitekeleza kwa sababu uwekezaji katika miundombinu ya *irrigation* inagharimu fedha nyingi sana. Hapa nina *figures* chache kidogo zinazoonyesha.

Na. 75

### **Vita Dhidi ya Wapiga Debe - Vituo vya Mabasi**

**MHE. MGANA I. MSINDAI** aliuliza:-

Kwa kuwa tarehe 7 Novemba, 2003 Serikali ilitamka Bungeni azma yake ya kujizatiti katika kupambana na tatizo la Wapiga Debe kwenye vituo vya mabasi na kwamba mapambano hayo yatawahusisha wadau mbalimbali hususan wamiliki wa mabasi, madreva, makondakta, mamlaka ya leseni za magari Mikoani na wananchi kwa ujumla:-

(a) Kwa kuwa mpaka sasa ni muda mrefu umepita tangu Serikali itoe tamko hilo, je, Serikali imefikia hatua gani katika zoezi zima la kupambana na Wapiga Debe hao ambao wamekuwa kero kubwa sana kwa wananchi na ni mafanikio gani yamepatikana hadi sasa?

(b) Je, Serikali imewashirikishaje wadau hao juu ya tatizo hilo?

(c) Je, tangu Serikali itoe tamko juu ya kupambana na Wapiga Debe hao ni madreva wangapi wameajiriwa na kupatiwa mafunzo na wamiliki wa mabasi toka Chuo cha Taifa cha Usafirishaji au Vyuo vingine vinavyotambulika na ni makondakta wangapi wamepewa mafunzo ya kuwahudumia wasafiri na uvaaji wa sare zao na kwamba jambo hilo linatekelezwa vipi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMABO YA NDANI YA NCHI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Serikali imejizatiti katika kuondoa kero ya Wapiga Debe kwenye vituo vya mabasi. Hatua zinazochukuliwa zinawahusisha wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Vyama vya Wamiliki wa Mabasi kwa mfano, *DARBOA*, Chama cha Umoja wa Madreva na Makondakta, Mamlaka za Leseni za Magari Mikoani, Baraza la Taifa la Usalama Barabarani, Chama cha Huduma za Wasafiri na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kero ya Wapiga Debe ni kubwa kwani miongoni mwao ni vibaka na waporaji wa mizigo ya abiria. Hivyo, Jeshi la Polisi limekuwa likiwasaka na kuwakamata. Baada ya tamko la Serikali la Novemba, 2003, Wapiga Debe mbalimbali wamekamatwa na kufunguliwa mashtaka. Hivi sasa wanafanya kazi hiyo kwa kujificha kwa vile wanafahamu wapo katika hatari ya kukamatwa.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Dar es Salaam ndio wenye tatizo kubwa la Wapiga Debe kuliko mahali popote pengine nchini. Katika jitihada za kumaliza tatizo hilo katika Mkoa wa Dar es Salaam, hatua zifuatazo zinachukuliwa hasa katika kituo kikuu cha Mabasi cha Ubungo:-

(i) Wakala wa mabasi sasa wanatoa ajira ya kudumu kwa wakataji tiketi na si zaidi ya watano kwa kila kampuni, vilevile wanawapa sare na vitambulisho. Abiria sasa wanatakiwa wakate tiketi katika ofisi za makampuni ya mabasi zilizoko nje ya kituo. Hatua hii imepunguza vurumai za wapiga debe kugombea abiria ndani ya kituo.

(ii) Wamiliki wa mabasi wameanzisha utaratibu wa mikataba ya ajira kwa madreva na makondakta, pia wamewapa sare. Kwa kuwa madreva wana uhakika wa mishahara kila mwezi, hawahitaji tena msaada wa Wapiga Debe. Aidha, sare za madreva, makondakta na wakataji wa tiketi, zinawatofautisha na Wapiga Debe, hivyo ni rahisi Polisi kuwabaini na kuwakamata Wapiga Debe; na

(iii) Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, kwa msaada wa Benki ya Dunia, kuanzia mwaka 2005 itaanzisha utaratibu wa mabasi makubwa kutoa huduma katikati ya Jiji (*Bus Rapid Transit*). Chini ya utaratibu huu, vituo rasmi vitajengwa na kila kituo kitakuwa na msimamizi, na abiria wataingia kwa foleni. Hatua hii itawaondoa Wapiga Debe wote Jijini. (*Makofi*)

Aidha, katika kipindi cha 2002/2003, Chuo cha Usafirishaji kimeendesha kozi 44 za madreva wa mabasi, zenye jumla ya madreva 800. Idadi hii ni ndogo kwa kuwa huko nyuma haukuwepo mkataba wa wamiliki wa mabasi kuwasomesha madreva na makondakta wao. Hivi sasa mkataba huo unaandaliwa. Madreva wanaosoma hivi sasa

wengi wao wanasomeshwa na Chama chao cha Umoja wa Madreva na Makondakta (UWAMADAR). Napenda kukipongeza chama hiki kwa hatua hii ya kimapinduzi. (Makofi)

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kwa kweli sasa hivi Ubungo ndiyo kituo kikuu ambapo wapigakura wetu wote kutoka katika Mikoa mbalimbali wanafikia na kwa kuwa hata watalii wanaotumia mabasi wanafikia hapo. Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kuongeza Askari wa kuangalia hao vibaka wasiwasumbue abiria ikiwa ni pamoja na Askari wa *CID*?

**NAIBU WAZIRI WA MAMABO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, kituo cha mabasi cha Ubungo ndicho kituo kikubwa hapa nchini na ni kweli kinahudumia mabasi ya ndani ya nchi na ya nje ya nchi na wageni wengi wanapitia pale. Kwa kuzingatia hali hiyo, hivi sasa pale tumeshajenga kituo kikubwa cha *Grade B* cha Polisi ambacho kinahudumia kituo hicho cha mabasi na kinafanya kazi vizuri kupambana na Wapiga Debe na hoja kwamba tuongeze Askari ni pendekezo zuri, tutalitazama katika mpango mzima wa kuajiri Askari wa Jeshi la Polisi wa mwaka hadi mwaka. Kwa hiyo, kituo kile tutakipa kipaumbele kwa sababu kwa kweli kinatoa taswira ya nchi yetu.

Na. 76

### **Upungufu wa Askari Polisi**

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO** aliuliza:-

Kwa kuwa katika bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ya mwaka 2003/2004 Serikali ilibainisha kwamba kuna upungufu wa Askari Polisi katika Jeshi hilo na kwamba uwiano uliopo kati ya Askari na raia ni 1:1500; na kwa kuwa kigezo cha Kimataifa cha uwiano baina ya Askari na raia ni 1:400 na 1:700; na kwa kuwa kutokana na ukweli huo ni kwamba itachukua muda mrefu kwa Jeshi la Polisi kufikia uwiano huo wa Kimataifa na wakati huo huo wimbi la ujambazi na ajali mbalimbali zinazidi kuongezeka nchini:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha Jeshi hilo ili kukabiliana na wimbi la uhalifu na ni kwa kiwango gani mikakati hiyo imeanza kutekelezwa?

(b) Je, ni Wananchi na Askari wangapi wameuawa kutokana na matukio ya ujambazi na ajali mbalimbali nchini kuanzia mwaka 1995 hadi sasa na Serikali imejifunza nini?

**NAIBU WAZIRI WA MAMABO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, Mbunge wa Liwale, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika kuliimarisha Jeshi la Polisi kukabili na wimbi la uhalifu, Serikali ina mpango wa kuweka uwiano mzuri baina ya idadi ya Askari na raia kutoka uwiano uliopo sasa wa Askari mmoja kuhudumia raia 1,200 hadi kufikia uwiano wa Askari mmoja kuhudumia raia 700. Ili kufikia uwiano huu, Serikali inatekeleza mpango wa kuajiri Askari wapya kila mwaka kwa kadri ya hali ya bajeti, pia Serikali ina mpango wa kuliongezea Jeshi la Polisi nyenzo za kufanyia kazi kila mwaka, hasa magari na vifaa vya mawasiliano.

Katika kutekeleza azma hii, bajeti ya Jeshi la Polisi katika mwaka huu wa fedha imeongezeka kwa takriban asilimia 30 yaani kutoka shilingi bilioni 51.2 za mwaka 2003 hadi shilingi bilioni 70.7 za mwaka 2004/2005. Aidha, mwaka ujao wa fedha katika fedha tutakazozomba katika Bunge hili tunatarajia bajeti ya Jeshi la Polisi itaongezeka kwa asilimia 25.

(b) Mheshimiwa Spika, jumla ya wananchi 802 na Askari 18 waliuawa kutokana na matukio ya ujambazi kuanzia mwaka 1995 hadi sasa. Aidha, wananchi 15,815 na Askari 66 wamepoteza maisha kutokana na ajali mbalimbali. Kutokana na hali hii ya ujambazi, Serikali imejifunza kuwa suala la kupambana na ujambazi ni la kudumu na hivyo Serikali itaendelea kuboresha utendaji kazi wa Jeshi la Polisi kwa kuliongezea vitendea kazi na kuboresha mazingira yao ya kazi, hii ni pamoja na kuwajengea Askari Polisi nyumba za kisasa. Vilevile Serikali itaendelea kuwahamasisha wananchi washiriki katika ulinzi wa maeneo yao wakisaidiana na vyombo vya dola.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kujua kwa nini inapotokea ghasia wanatumika Askari wa *FFU* wa kiume kuwadhibiti akinamama badala ya kutumika Askari wa kike kuwadhibiti akinamama?

(b) Kutokana na hali halisi ya Jimboni kwangu Liwale kuwa na eneo kubwa, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba Liwale wanahitaji kupata mafuta ya kutosha ya kuweza kudhibiti eneo hilo na pia gari imara kutokana na barabara mbaya na kwa vile kuna wanyama wakali?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika Kikosi cha *FFU* na Jeshi zima la Polisi, hakuna ubaguzi kati ya wanaume na wanawake. Akinamama vilevile wamo katika Kikosi cha *FFU* na wanafanya kazi vizuri tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la (b) nakubaliana naye kwamba, Wilaya ya Liwale ni moja ya Wilaya zenye maeneo makubwa kama zilivyo baadhi ya Wilaya vilevile hapa nchini. Kwa hiyo, maombi ya Mheshimiwa Mbunge ya mafuta na gari ni halali. Naomba itakapofika zamu ya bajeti ya Wizara yetu basi atusaidie kuipitisha kwa



sababu ndani ya bajeti hiyo ndiyo tutapata uwezo wa kufanya hayo ambayo anayaomba tuyafanye.

Na. 77

### **Kuungua Moto Majengo ya Serikali**

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa si jambo la kushangaza kusikia kwamba nyumba zimeungua moto kutokana na hitilafu ya umeme kama ilivyotokea kwa jengo la Benki Kuu, jengo la Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, *NASACO*, jengo la Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, nyumba za watu binafsi na majengo mengine yanaendelea kupata mikasa hiyo:-

(a) Je, tatizo hilo linatokana na mgao wa umeme wa *TANESCO* au ufungaji wa nyaya ndani ya majengo hayo au kuchakaa kwa nyaya?

(b) Je, Serikali ina utaratibu gani wa makusudi wa kutatua tatizo hilo ambalo sasa limekuwa sugu?

(c) Je, mpaka sasa Serikali imechukua hatua gani za makusudi katika kulidhibiti tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuna vyanzo mbalimbali vya moto unaotokea na kuunguza nyumba zikiwemo nyumba za Serikali au majengo ya Serikali. Vyanzo hivi vinasababishwa na ama kutokuwa na uangalifu wa matumizi ya moto ndani ya nyumba, uchakavu na matumizi mabaya ya vyombo vitumiavyo umeme kama vile pasi, majiko ya umeme, majokofu na viyoyozi. Aidha, hitilafu za umeme zinazosababishwa na ama mfumo mabaya wa mtandao wa nyaya za umeme ndani ya nyumba (*Poor Wiring System*) au umeme unaozidi viwango vinavyokubalika kwenye umeme wa *TANESCO (Over Voltage)* pia unaweza kusababisha moto. Kutokana na hali hiyo ndio maana baada ya tukio la moto, uchunguzi hulazimika kufanyika ili kubainisha chanzo halisi cha moto na mapendekezo ya hatua za kuchukuliwa kutolewa.

Mheshimiwa Spika, udhibiti wa utendaji wa makandarasi wa umeme upo kwa kutumia Sheria ya Umeme na Bodi ya Leseni za Umeme, pamoja na Msajili wa Makandarasi. Pamoja na sheria hizo, wananchi wanashauriwa waepuke kutumia mafundi, kwa jina maarufu wanaitwa “Vishoka”, wasiotambuliwa rasmi na *TANESCO*. Vilevile *TANESCO* hawapaswi kumuunganishia mteja umeme bila kujiridhisha kama

Michoro na utandazaji wa nyaya ndani ya jengo au nyumba umezingatia viwango vinavyohitajika.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa Serikali imekwishaunda Wakala wa Serikali wa Ukaguzi kwa maana ya usalama wa wafanyakazi. Wakala huyu pamoja na mambo mengine ni mkaguzi wa mifumo ya umeme katika majengo na mahali pa kazi. Aidha, Wakala hufanya shughuli hizo kupitia wakaguzi binafsi pale inapobidi. Hii itasaidia kugundua hitilafu mbalimbali katika ufungaji wa nyaya kabla hatari yoyote haijatokea na kufanya marekebisho. Aidha, kipo kitengo cha moto Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, ambacho kinahusika pia na ukaguzi wa majengo ili kugundua na kushauri kuondolewa kwa hatari zinazoweza kusababisha moto.

Mheshimiwa Spika, uchunguzi wa moto uliotokea kwenye majengo aliyoyataja Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, haukubaini kuwa umeme ndio moja kwa moja uliosababisha moto. Kwa mfano, moto ndani ya jengo la Wizara mbili, Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo pamoja na Wizara ya Nishati na Madini ulioanzia ghorofa ya saba ulisemekana ulitokana na hitilafu kwenye kiyoyozi pamoja na kuwa na nyaya ambazo hazikuwa barabara.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa mara nyingi tunasoma kwenye magazeti kwamba chanzo ni umeme na bahati mbaya Wizara haijakanusha kwamba chanzo si umeme na kwa kuwa katika jibu lake Mheshimiwa Naibu Waziri hajasema Wakala huu umeanza lini. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kuiomba *TANESCO* ilipe gharama zote siyo tu kwa nyumba zilizoungua na vyombo vilivyoharibika badala ya kuwasumbua?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, wakati natoa jibu la msingi nilisema kwamba, mara nyingi baada ya ukaguzi kufanyika unaohusisha sehemu tatu, Zimamoto, Polisi na *TANESCO*, imebainika kwamba, matatizo ambayo yametokea ni ya umeme ndani ya nyumba. Lazima tutofautishe baina ya umeme unaokuja hadi unapoingia kwenye nyumba na umeme ndani ya nyumba. Wajibu wa kuhakikisha kwamba umeme ndani ya nyumba ni salama ni wajibu wa yule mwenye nyumba kwa mujibu wa sheria zinazozingatia masuala ya usambazaji umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu kusumbuliwa, fidia hulipwa pale inapobainika kwamba hitilafu hiyo imesababishwa na umeme wa *TANESCO* moja kwa moja unaotoka nje. Katika Sheria inayozingatia usambazaji wa umeme upo wajibu na haki ya *TANESCO* kwa upande mmoja, lakini pia upo wajibu na haki wa wale ambao wanaunganishiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, katika kipindi cha mwaka mmoja na hii ni kuonyesha kwamba watu hawasumbuliwi, ila pale inapobainika kwamba hapa haki imedhihirika wanalipwa, katika kipindi cha mwaka mmoja pamekuwa na malipo zaidi ya shilingi milioni 16 ambazo *TANESCO* imelipa kwa watu ambao wameathirika na moto ambao umeonekana kwamba umesababishwa na wao wenyewe *TANESCO*. (*Makofi*)

**Umeme wa Gesi kupelekwa Lindi na Mtwara**

**MHE. ABDILLAH O. NAMKULALA** aliuliza:-

Kwa kuwa umeme wa gesi ya Songo Songo utapita katika Mji wa Nangurukuru na kwa kuwa umeme huo ni wa uhakika kuliko wa *Generator*:-

(a) Je, Serikali inaona ugumu gani kuuchukua umeme wa gesi ya Songo Songo kutoka Nangurukuru na kuupeleka Lindi hatimaye Mtwara?

(a) Kwa kuwa umeme wa gridi umefika Morogoro na kwa kuwa Mkoa huo umepakana na Mkoa wa Lindi hasa katika Wilaya ya Liwale, je, kuna kikwazo gani kwa umeme huo kupitishwa kwenye Wilaya ya Liwale kutokea Mkoa wa Morogoro na hatimaye kufikishwa Lindi na Mtwara?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mbunge wa Mtwara Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Serikali imesema mara nyingi hapa Bungeni na imetoa taarifa hapa Bungeni na mwisho hivi karibuni wakati najibu swali la Mheshimiwa Mohamed Abdalaziz, Mbunge wa Lindi Mjini, Serikali imeona kwamba, Mradi wa *Mnazi Bay* ndio wenye matumaini ya kuipatia miji ya Lindi na Mtwara umeme katika kipindi kifupi kijacho. Vinginevyo ingebidi kuwa na mradi mpya wa kupanua kituo cha kuweka mitambo mikubwa ya *MW 15* na kujenga laini ya kilovoti 132 kutoka Somanga Funga hadi Mnazi Mmoja Mkoani Lindi pamoja na kujenga kituo cha kupunguzia nguvu za umeme. Pia inabidi au ingebidi kuwa na gridi ndogo ya kuunganisha Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma, kwa kutumia umeme wa chanzo cha gesi ya Songo Songo,

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Mkoa wa Morogoro unapakana na Mkoa wa Lindi na kwamba gridi ya Taifa imeishia Mahenge, umbali wa kilometa 170 Kaskazini Magharibi mwa Mji wa Liwale, Mkoani Lindi. Hata hivyo, Miji ya Mahenge, Liwale na Lindi imetenganishwa na Hifadhi ya Wanyamapori ya *Selous* na matawi ya Mto Rufiji. Mandhari hayo husababisha ujenzi wa miundombinu ikiwemo ya umeme kuwa wa gharama kubwa na Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori pia inakataza ujenzi wa nyaya hizi juu ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, ili kuweza kuipatia miji ya Lindi na Mtwara umeme katika gridi ya Taifa huko Kihansi, inabidi laini itakayokidhi mahitaji ya umeme kwa miji iliyo mbali kwa zaidi ya kilometa 150, sharti iwe ya msongo wa *132 KV*. Inabidi pia kiuchumi miji ya Lindi, Mtwara, Mtama, Newala, Nachingwea, Tandahimba, Ruangwa

na Liwale, sharti iunganishwe kwenye laini mpya itakayojengwa na laini ya umeme itakayojengwa kukatiza Hifadhi ya Taifa ya *Selous*, sharti ipitishwe chini ya ardhi (*Armoured Cable*) kwa usalama wa Wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, inabidi kujenga pia laini ya *KV 132* kama nilivyosema awali pamoja na vituo vidogo vidogo kutoka Kihansi hadi Mnazi Mmoja Lindi umbali wa kilomita 400 hivi. Pia inabidi kuunganisha kama nilivyosema miji ambayo nimeitaja kukarabati njia ya umeme kati ya miji ya Lindi na Mtwara kwa *66 KV* na kujenga laini kati ya Mji wa Mtwara na Masasi. Mradi wa aina hiyo utagharimu karibu Dola za Marekani milioni 42.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia uchambuzi wa gharama, upatikanaji wa fedha na upatikanaji wa uwekezaji, muda unaohitajika kukamilisha maandalizi ya mradi na utatuzi wa athari za mazingira kutokana na mfumo niliouelezea ndiyo maana kama nilivyosema awali, Serikali iliamua kutekeleza mradi wa umeme utokanao na gesi asilia ya *Mnazi Bay*.

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza.

- (i) Huu uchimbaji wa gesi ya *Mnazi Bay* tunaoungojea utanza lini?
- (ii) Wenye dhahabu wana mrabaha na wenye wanyama wana mrabaha, je, sisi wenye gesi mpango wa mrabaha ukoje?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, wiki iliyopita nilijibu hapa Bungeni kuhusu kuanza kwa Mradi wa *Mnazi Bay*. Nilisema na napenda nirudie kwamba, mradi huo utanza rasmi Julai, 2004 kwa maana kwamba, mkataba baina ya Serikali na upande wa wawekezaji ulisainiwa hivi karibuni na ifikapo Julai wanatarajiwa waanze kazi baina ya Julai na Desemba ya kutathmini au kuhakiki kiasi cha gesi iliyopo katika visima vile na endapo uhakiki huo utatupa matokeo mazuri, basi mwanzoni mwa 2005 kazi ya ujenzi itanza kwa maana ya kujenga mitambo na mfumo mzima wa umeme.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la mrabaha, napenda niseme kama ifuatavyo: Kwanza, tumekuwa tukisema mara kwa mara hapa Bungeni kwamba, suala la mrabaha unaolipwa kwa raslimali hizi za nchi unalipwa kwa Serikali Kuu na unakwenda kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na kutokana na Mfumo wa Serikali tuliokuwa nao hapa Tanzania, fedha hizi hugawanywa au hutolewa kama matumizi kwa Mikoa na Wilaya mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, lakini pia napenda niongeze kwamba, masuala haya ya madini na raslimali hizi hususan suala la madini ambalo amelitolea mfano Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, kama ambavyo tumesema hapa Bungeni, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshaunda Kamati ya kutathmini mambo yote yanayohusiana na masuala ya madini.

Mheshimiwa Spika, naomba tufanye subira ili Kamati ile ikamilishe kazi yake iwasilishe Serikalini na Serikali itathmini halafu itoe taarifa muafaka. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha, sina matangazo ya vikao vilivyopangwa kwa leo. Lakini napenda kuwajulisha Waheshimiwa Wabunge yafuatayo: Ratiba ya leo nilishaelezea tangu jana haina mabadiliko. Nilisema wamebaki Waheshimiwa Wabunge wachache ambao wangechangia asubuhi hii kwa kweli ni watatu tu. Walioomba kuchangia walikuwa 91 jumla yao, lakini hawakusema wote kwa sababu mbili. Moja, wako walioondoa majina yao walingoja Wizara moja moja zile zilizowahusu zaidi. Lakini pili wako wengine walioitwa na hawakuwepo Bungeni wakati wanaitwa. Sasa katika hali ya maombi mengi namna ile, tulitumia kanuni ya asiye kuwepo na lake halipo. *(Makofi/Kicheko)*

Nitumie nafasi hii kueleza ratiba ya kesho Jumamosi. Hatuna semina kama tulivyokwisha kueleza lakini iko semina ya aina nyingine. Tutaanza na matembezi ya kilomita 3 yatakayoanza saa 1.00 asubuhi. Lakini Waheshimiwa Wabunge, kama ratiba zilivyokwisha kugawiwa zinavyoonyesha, tunategemewa tufike kule uwanjani saa 12.30 asubuhi ili matembezi yaanze saa 1.00 asubuhi kuanzia Uwanja wa Michezo wa Jamhuri kutoka pale hadi kufika hapa Ofisi za Bunge.

Kila Mbunge atakayeshiriki atadhaminiwa shilingi 5,000/= na *Tanzania Breweries Limited* kwa kila kilomita atakayoshiriki. Kama atashiriki zote tatu basi shilingi 15,000/=. Sio zake yeye fedha hizi zitatolewa kwa Taasisi mbili zinazohudumia watoto yatima hapa Dodoma. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, mahudhurio mazuri ya Waheshimiwa Wabunge yatawezesha kutunisha zaidi mfuko huo kwa faida ya watoto yatima. Sasa mara baada ya kufika viwanja vya Bunge hapo nje mambo yatakuwa kama ifuatavyo: Kutakuwa na uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, atakayeizindua ni Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Vile vile kutakuwa na uzinduzi wa Sera ya Taifa ya Menejimenti ya Maafa mzinduzi mwenye jukumu hilo ni Mheshimiwa Waziri Mkuu vile vile. Halafu kutakuwa na uzinduzi wa Tovuti ya Ofisi ya Waziri Mkuu ni yeye mwenyewe atafanya shughuli zote hizo na kwa hiyo ndiyo atakuwa mgeni rasmi katika kipindi hicho. Ndiyo nikasema tumehesabu kama ni semina kwa Wabunge, kwa hiyo, masharti ya kawaida ya semina yatatekelezwa. *(Makofi)*

Halafu jioni kuanzia saa 12.00 kutakuwa na tafrija rasmi iliyoandaliwa na *Bunge Sports Club*, ambayo ina madhumuni ya kuhitimisha mjadala wa Bajeti. Lakini *Bunge Sports Club* wamedhaminiwa na *Tanzania Breweries* hiyo hiyo ndiyo watakaolipia gharama za burudani ya jioni. Kwa hiyo, kutakuwepo kama kawaida vinywaji, vitafunwa na burudani ya muziki ikiongozwa na *OTTU Jazz Band* na Ndala Kasheba na *One Stars* na zawadi mbalimbali zitatolewa na Mashirika ambayo yamepangwa kwa Waheshimiwa Wabunge watakaostahili kupewa zawadi hizi.

Kwa kuwa shughuli zote zinaongozwa na *Bunge Sports Club*, basi mgeni rasmi katika shughuli hiyo ya jioni atakuwa Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club*.

Mwisho wa matangazo, tunaendelea na *Order Paper*, Katibu. (*Makofi*)

## HOJA ZA SERIKALI

### **Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2003, Mpango na Mwelekeo wa Mwaka 2004/2005 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2004/2005**

(*Majadiliano yanaendelea*)

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami nichangie kidogo kuhusu hoja hizi mbili za Waziri wa Fedha na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji.

Mheshimiwa Spika, lakini awali ya yote ningependa kuungana na wenzangu walionitangulia, kuwapa pole sana Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na dada yake Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na baba yao.

Mheshimiwa Spika, pia ningependa kuchukua nafasi hii kumtakia Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa apone mapema, arudi atuongoze hapa nyumbani. Pia ningependa kuchukua nafasi hii kumtakia afya njema Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, apone arudi ili aendelee na kikao hiki.

Mheshimiwa Spika, bajeti hii imekuja wakati muafaka na mimi nasema naiunga mkono mia kwa mia. Naiunga mia kwa mia kwa sababu kwa kweli inatupa mategemeo mazuri hasa sisi Chama Tawala. Nadhani Watanzania wote wanaonisikiliza wataungana na mimi kusema hii ni bajeti ya kuondoa umaskini. Ina lengo kubwa la kuwanyanyua wale walalahoi wanaoitwa walalahoi kwa kuwaongezea kipato angalau kwa kuboresha kilimo. Mimi ni Mbunge wa Musoma Vijijini na wapiga kura wangu wote wanaishi kwenye hali duni sana. Nadhani watafarijika kwa kuona hatua iliyochukuliwa na Serikali kuwanyanyua huko waliko.

Lakini nitakuwa nadhani nimepotoka nikiacha kuzungumzia maeneo machache ambayo hayakuzingatiwa. Kwanza ni elimu. Nampongeza Waziri wa Elimu kwamba amejaribu kuboresha elimu kwa kuongeza idadi ya Shule za Msingi. Nampongeza sana. Idadi ya shule kijijini kwangu inaongezeka, jimboni kwangu inaongezeka. Lakini ongezeko hili sio la kuridhisha ukichukua *National Standards*. *Standard* ya majengo haikuongezeka imeporomoka hata kwangu. Ukichukua mfano wakati wa Wakoloni, shule za msingi zilikuwa zinaendeshwa na *Native Authority*, ndiyo shule nilizosomea mimi na ndiyo shule aliyosomea Mheshimiwa Waziri wa Elimu, *standard* ilikuwa nzuri. Shule zinazojengwa chini ya Mpango wa MEM sio nzuri, za ovyo. Za ovyo kabisa, hazikupimwa na wataalamu. Sasa unaposema tunasonga mbele mimi nadhani kusema kweli *in terms of national standard* tunashuka chini. Sasa nikimnukuu Waziri wa

Mipango anasema: “Nia ya Serikali ni kuboresha mazingira ya shule.” Mimi nilishangaa unaboreshaje mazingira ya shule ambapo mazingira ya shule yanaporomoka! (*Makofi*)

Unapotengeneza chakula Tanzania kuna chombo maalum kinaitwa *National Bureau of Standards*, lazima utengeneze chakula kinafanane ama kinalingane na viwango tulivyoviweka. Lakini kwa elimu hakuna viwango tulivyoviweka vya madaraka tuliyoyajenga, hakuna. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, nachukua *Oysterbay Primary School*, iko pale ilijengwa na Wakoloni, mazingira yake ni bora. *Next* pale wamejenga shule nyingine inayofanana fanana na boma la ng’ombe pale pale. Sisi Viongozi tunapita pale na ukiangalia unaona aibu. Wakoloni miaka 40 walijenga *Primary School*, Waziri wa Elimu miaka 40 baadaye amejenga shule hapo hapo haifanani na ile. Sisi tunasema kwa kujidai kweli eti tunaboresha mazingira ya elimu, nadhani tunadanganyana kwa kweli. Wakati umefika tuanze kubuni *National Standard* ya majengo ya *Primary Schools*. Tusipofanya hivyo katika hii *crop village* nadhani hatuwezi kufika tunakokwenda. Huu ndio mchango wangu wa kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili, nasikitishwa sana kusikia eti Serikali inakusanya kodi nyingi sana. Mimi hapo kwa kweli sikubaliani na usemi huo. Ninasema hivyo kwa sababu zifuatazo: Kila kijiji tunachokwenda tunakuta Watanzania wanajenga shule kwa nguvu zao wenyewe na wanaungwa mkono na Serikali kwa ubia fulani. Serikali inatoa mchango kwa zile shule. Kwa hiyo, mchango wa Serikali ni mkopo waliopata kwa wafadhili. Wamepewa fedha kama mkopo, zikifika Tanzania zinapelekwa kwenye *Local Government* wao wanazisambaza hizo fedha. Zikifika huko wananchi wanaunganisha na mchango wao wanaanza kuzifanyia kazi. Lakini wanapokwenda kununua mabati yale mabati yanatozwa kodi ya *VAT*. Lakini hii *grant* inatozwa kodi fedha zinarudi wapi? Zinarudi Serikalini. *TRA* inakusanya zile fedha asilimia 20, unawanyang’anya hawa Watanzania asilimia 20 kwa njia ya kodi ya *VAT* kwa mabati, misumari, sementi na kadhalika. Hii ni sawa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kila Mbunge hapa anayaona haya. Hata Waziri wa Fedha anayaona hapa. Kila shule iliyojengwa na Watanzania unatoza kodi, hiyo ni kweli au hiyo ni safi? Mtawarudishia lini Watanzania asilimia 20 mliyowatoza kwa hizo shule walizojijenga? Nataka nipate jibu leo kutoka kwa Waziri, zitarudi lini? Nitatoa mfano, Wajapan wamejenga Dar es Salaam pale Shule za Msingi. Hizo shule hawakutozwa kodi ya asilimia 20. Wao wamejenga na *material* ambayo ni *excuse*, haina kodi. Wao ni wawekezaji, lakini Watanzania walio wengi eti sio wawekezaji kwa zile shule. Je, hiyo ni sawa? (*Makofi*)

Halafu Serikali inatuambia eti wamekusanya kodi nyingi. Kutoka wapi? Asilimia 20 ukitoa bajeti ina-*collapse*, kwa haya majengo yote yaliyojengwa. Ita-*collapse*. Sasa tutasema kitu gani? Wataniambia ndiyo kuna *exemption*. *Exemption* eti kuna schedule kwenye ile *VAT* inasema kama umeleta mali ya kujenga shule utapata *exemption*. Mimi nimejaribu kuomba *exemption* kwangu, mimi ni msomi najua sheria ya kodi vizuri sana, nimejaribu nimekwama kwa shule zangu zote pale Musoma. (*Makofi*)

Kuna Watanzania wengine pale kwangu tunatengeneza *windmill* ya kusukuma yale maji kwa kujitegemea sisi wenyewe. *Windmill* tumeagizia kutoka Nairobi lakini ikifika mpakani wanasema tulipie kodi, sasa ile *windmill* ni ya maendeleo Vijijini? Kwa hiyo, naambiwa ile *windmill* ikija pale ni lazima uifungue, ukiifungua vipande vipande utaiweka kwenye boksi. Ikifika mpakani wanasema hiyo sio *windmill* maana sasa ime-*seize* kuwa *windmill*? Sasa utaingizaji nchini, utaileta kwenye gari ipi? Hii Sheria gani ya *TRA*, Waziri hutatusaidia hata kwa hilo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimesema naunga mkono bajeti lakini nadhani ukweli ningesema nisingeunga mkono. Lakini nadhani *point* niliyoisema ni kwamba, rekebisheni kabisa kabisa. Ondoa kodi kwa wananchi wanaojenga shule kwa kujitolea. Ondosheni hiyo kodi, *encourage* watu watoe *donation* kwenye mashule. Nawaombeni sana tufanye marekebisho hayo.

Tatu na mwisho, upande wa madini. Nasikia eti madini mapato yanazidi kuongezeka, mimi nadhani yanapungua. Pale kwangu kuna mgodi wa *Buhemba Mines*, sijui pale ni wabia au kampuni, sijui. Wamejenga shule pale Butiama karibu na kaburi pale eti pamejengwa *in exchange for* maji waliyochukua pale, ovyo ile shule haina umeme. Eti ni msaada wao lakini wanachimba tani za dhahabu kutoka Buhemba wanatuachia mashimo. Nakuomba Waziri sijui ni Waziri wa Madini, nadhani anayehusika, hawa ni wezi wako pale tu. Pale ni wezi tu. Hata ile asilimia 5 hawatoi. Ukiwauliza wanasema aah! Hili ni wanajeshi, mali ya wanajeshi, siyo wawekezaji. Sasa wale watu wa Buhemba wafanye nini mnawanyang'anya kabisa madini yao angalau kuwapa hata shule mnakataa kuwapa, hiyo ni sawa? (*Makofi*)

**WABUNGE FULANI:** Sio sawa. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Nawaombeni waitoe ile shule maana sio shule ni dharau kwetu pale kwa watu wa Butiama, ni dharau. Namwomba Waziri wa Elimu awanyime kibali cha kufungua hiyo shule maana haifai na wapewe adhabu kwa kufanya kitendo cha ovyo namna ile. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa machache niliyoyasema, naunga mkono hoja lakini wafanye mabadiliko haya. Ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. BALOZI AHMED HASSAN DIRIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza niruhusu nitoe shukrani zangu nyingi sana kwako kwa kunipa nafasi kabla mjadala huu haujafungwa ili niweze na mimi kutoa mchango wangu.

Kwanza, napenda niungane na wenzangu kwa kutoa pole kwa ndugu yetu Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na dada yake Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kupoteza baba yao. Mungu amlaze mahali pema na ndiyo kazi ya Mwenyezi Mungu. Nilipomwandikia Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda alisema: "*Inna Lilahi Waina ilaihi Rajyuun*". Maana yake yeye ndiye anayeamua na yeye ndiyo mwenye kuchukua. Mungu atawapa moyo mkubwa wa kustahimili haya yaliyotokea. *Amin*.



Pia niruhusu nitoe pole kwa Mheshimiwa Anne Malecela, kwa mikasa iliyotokea wakati anakuja Bungeni. Lakini pia niwape pole wale wote ambao wamepata mikasa mbalimbali wakati wanakuja hapa pamoja na kijana wetu, Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere.

Mheshimiwa Spika, lakini pia niruhusu nimpongeze Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Baraza la *African Union*. Lakini kule wanamwita *Madam Presidia* na watu wetu hapa walifikiri labda *President* wa *African Union*. Lakini nafikiri ni kutokufahamu ile ni lugha ya Kifaransa tu, lakini ni Spika.

Mheshimiwa Spika, pia niruhusu niwashukuru na niwapongeze sana Mawaziri wetu wawili, waliotoa hotuba zao zenye mwelekeo kwa maana na mwelekeo wa kuwapa Watanzania matumaini. Ninaamini hotuba hizi zimeleta mwamko mpya katika kuangalia maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini kabla sijaingia katika mada hasa ninayotaka kuzungumzia, ambayo ni ya kilimo inayochukua watu wengi, nilitaka kukumbusha kupitia kwako katika Bunge hili kuwa Wachina katika mwaka 1978 walipokuwa wanaingia katika *economic reforms*, Dang Xiaoping, ambaye ndiyo mtaalam mkubwa na ndiye aliyeibadilisha China kufika katika hali hii iliyokuwepo alisema kitu kimoja kuwaambia Wachina. Aliwaambia Wachina kuwa: “*to be rich is glorious*”, maana yake kuwa na utajiri kama mwanadamu ni jambo kubwa na zuri.

Hakusema hilo kuwa alitaka Wachina *1.4 billion* wabadilike siku moja, lakini ile wenyewe wanaita *wakeup call*, maana yake kubadilisha mawazo ya Wachina kwa muda waliokuwa katika Siasa ya Ujamaa waliyokuwa nayo. Sasa katika kubadilisha hilo Dang aliwaambia kuwa, *to be rich is glorious*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusoma hii nilikuwa nikijiuliza kwamba, sisi Watanzania tumekuwemo katika mfumo wa hodhi na tumekuwa katika mfumo wa kujitegemea na tumekuwa katika mfumo wa kushirikisha Wananchi wetu katika maendeleo yetu, lakini katika maendeleo haya na dunia hii inavyozunguka na *globalization*, tumejenga *mindset* za watu wetu namna gani, tunakwenda pamoja au tunakwenda msege mnege?

Kikwetu msege mnege maana yake mnakwenda huku mnayumba. (*Kicheko*)

**MHE. BALOZI AHMED HASSAN DIRIA:** Hilo ndiyo nilikuwa najiuliza, kwa sababu kama *mindset* zetu haziko pamoja, kwa kweli hatutaweza kujenga ile Wachina wanaita *culture* mpya hii katika vichwa vyetu. Bila ya kujenga hilo na *mindset* zetu zikakubali kama ulimwengu umebadilika na unakubali kama hii *globalization* hatuwezi tukaikimbia, basi tuna maana kubwa sana kabisa ya kwenda pamoja, lakini siyo wengine wanakwenda huku, wengine wanakwenda kule, halafu mnafikia katikati mnaanza kuonyeshana vidole. Lazima *our frame of mind, our mindset has to remain*

katika *decision*, tulizichukua wenyewe za kuingia katika mfumo huu wa sasa ambao ni wa kiliberali wanaita *liberal system*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa tukikubali hilo, unajiuliza pia katika mfumo huu na katika dira yetu ya 2025 nini *priority* yetu zaidi? Tumekwenda kwenye mkutano wa *Global Summit* wa *millennium*, vimewekwa vigezo fulani vya kuondoa umaskini katika nchi au katika ulimwengu *by the year 2015*. Lakini ukiangalia huku kwetu na vigezo vilivyowekwa katika *World Summit*, utakuta sisi bado hatukufikia hata robo, bado watu wetu wanaishi chini ya *one dollar a day*.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nikitazama hapa nikaona kama *population* yetu ni kubwa sana, inashindwa katika kujipatia chakula *three square miles a day* ambayo Wajapan wanasema *it is one of the most important basic needs* katika maisha ya mwanadamu. Lakini watu hao hao sisi Watanzania tuna *4.62 million smallholders* (wakulima wadogo wadogo) na hilo ndiyo nataka kulizungumza zaidi. Kila mmoja ana eka 0.2 au 2. Hawa ndiyo wanaotulisha sisi na ndio wanaotuvisha sisi kutokana na *foreign exchange earning* inayotoka katika kuuza mazao ya wakulima. Kwa hiyo, katika Taifa la *35 million people* wanalishwa na kuvishwa watu wa Mijini na hawa *4.62 million people* kwa kupata *foreign exchange earning* za wakulima. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa nchi yoyote ikiwa inajua kama *basic framework* yake ni kilimo, basi *investment* ya kilimo ndiyo iwe kubwa. Hamuwezi mkasema mtaondoa umaskini wakati kilimo hamjafikia hata *10 percent* ya bajeti yenu! Ulimwengu unataka ufikie kilimo *10 percent of the budget*. Sisi tunawashauri *SADC* wafanye hivyo, lakini tunatoa *around 29.1 billion* kwa kilimo, *are we serious?*

**WABUNGE FULANI:** *No!*

**MHE. BALOZI AHMED HASSAN DIRIA:** *Are we really fighting poverty?*

**WABUNGE FULANI:** *No!*

**MHE. BALOZI AHMED HASSAN DIRIA:** Sasa ninajiuliza, kwa nini tunafanya hivyo? Ni lazima tukubali kwamba tofauti yetu sisi na wakubwa hawa walioendelea katika kilimo ni *technology* na *commercial farms*. Lakini leo Tanzania huwezi kuzungumza juu ya *commercial farms*.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana na ninamsifu sana Rais wetu; Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa kwenda China na kuwaambia Wachina: “Njoooni mu-*invest* katika kilimo.” Yaani wa-*invest* katika *commercial farms* ili tuweze kushindana katika maendeleo ya ulimwengu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, binafsi nasema kwamba, kubwa zaidi ambalo wale wanatushinda ni teknolojia. Hiyo ndiyo tofauti yetu kubwa na *developed countries*. Lakini sisi tuna ardhi ya kutosha, kwa hiyo, lazima tungejitahidi kufanya biashara na kulima kwa nguvu sana katika Tanzania na hiyo ndiyo itakayotuongoa katika umaskini.

Themanini katika mia ya watu wetu wako mashambani! Umaskini mkubwa uko huko, lakini hakuna *infrastructure*, hakuna kusaidiwa *inputs*, hakuna kuambiwa na kuelezwa kutokana na *Extension Officers* nini wapande katika sehemu fulani. Kwa hiyo, tunababaika katika ardhi yetu wenyewe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyezi Mungu ametupa maji, ametupa mito, ametupa mvua, ametupa akili, ametupa watu na ametupa nia. Sasa hayo yote tuliyonayo tukiyachanganya pamoja na *investment* hii tukageuza nchi yetu tukaingia katika *Green Revolution*, basi tutabadilika nchi hii na umaskini tutaupiga vita. Lakini *investment* inakwenda leo hapa, kesho pale, keshokutwa pale, hatuwezi kutoka katika umaskini huu ikiwa hatuja-*invest* zaidi katika ukulima au tutaendelea kuvishwa na kulishwa na *4.62 million people* wenye eka 2 kila mmoja? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kwamba, nchi hii Mwenyezi Mungu anatupenda sana na ataendelea kutupenda. Tumekuwa katika usalama kwa muda wa miaka 40, nchi zilizotuzunguka sisi ni nane na wote hawa wana uhusiano mzuri sana na sisi na tumewasaidia katika ukombozi wa nchi zao. Ingekuwa nchi yoyote nyingine na usalama tulio nao, basi binafsi nasema tungetumia *geographical proximity* yetu tukafanya biashara na watu hawa. Tumewasaidia, wanatutambua, wanatuelewa, lakini tumekuwa maskini kwa ajili ya kugombania Afrika. Leo itakuwaje biashara yetu na nchi nane zilizotuzunguka sisi haifiki hata *five percent*? Tunapanga nini sisi! Wakati huo huo, wale *South Africa* tuliwasaidia trade yao yote katika *SADC* ni *15 percent*, wamelishika soko. Sisi tuko hapa na huko kwenye *SADC* hatuna hata *3 percent*! Ni lazima tujiulize haya maswali, tujiulize kuna nini? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, wenzetu wanaotusaidia (*Donor Countries*) na wanaotupenda wanatuambia: “Miaka 40 ya mshikamano nchini mwenu na miaka 40 ya kukusaidieni, lakini bado mmebakia *listless developing country*, kuna nini huko?” Sasa wao wanatuuliza sisi tunapotoka nje kuna nini huko? Labda rafiki yangu Waziri atatupatia majibu kwa sababu tuna ardhi, tuna watu, tuna maji, tuna *minerals* na tuna madini. Sasa kilichobakia ni kitu gani tusi-*takeoff* sisi hapa? (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Spika, watu wa ulimwengu wanatuambia kuwa *more than a third of Tanzanians can not satisfy their basic needs*. Maana yake *one third* ya Watanzania milioni 35 hawana *three basic needs*. Wengine wanasema *18 percent can not afford food required for health living*. Unachukua unakula tu, lakini chakula chenyewe hakikutii nguvu. Kule kwetu Unguja wanasema unakula makapi ya kuokota. Ni kujaza tumbo usije ukaanguka, lakini nguvu hupati. (Kicheko)

Mheshimiwa Spika, wanasema *53 percent of rural people have no excess to water*. 53 katika mamia hakuna maji...

(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)

**MHE. BALOZI AHMED HASSAN DIRIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (Makofi)

**MHE. BALOZI GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami nichangie katika Hotuba hii ya Bajeti na Mpango wa Maendeleo ya Nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijazungumza mengi ningependa niwape pole wafiwa, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda na ndugu yake Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, kwa kupotelewa na mzazi wao na pia Mheshimiwa Parmuk Singh Hoogan kwa kufiwa na binti yake. Ninapenda pia niwape pole waliopata ajali katika sehemu mbalimbali, tunashukuru Mungu kwamba, amewanusuru maisha yao, tuko nao na wale ambao bado wanaumwa kama Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, tunamwomba apone haraka.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge na kwa kupitia kwao, Wananchi wote wa Tanzania, ambao katika kila sehemu ninayopita wameendelea kunipongeza kwa nafasi hii ambayo nimechaguliwa kuongoza Bunge la Afrika la nchi 53. Wadhifa huu nimeuchukua kwa unyenyekevu kwa kujua kwamba, maandalizi niliyopata kutoka katika nchi yangu ukiunganisha na vipaji nilivyonyavyo, ndiyo yameniwzesha kufika hapa nilipo. Nashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimefarijika pia baada ya kufika katika Bunge hili nikatambua kuna Mtanzania mwingine mwanamke, Rosebud Kurwijila, ambaye anaongoza moja ya Kamisheni ya Umoja wa Afrika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninataka kuanza mazungumzo yangu kwa kusema kwamba, Tanzania haina uhaba wa watu wenye uwezo. Tatizo tulilionalo ni kuwatambua, kuwaenzi na kuwatumia. Hilo ndilo tatizo kubwa. Watanzania wengi walioko nje ya nchi wanafanya kazi nzuri, ukiwakuta kule unashangaa kama huyu ni Mtanzania ambaye sisi tulikuwa hata hatumjui. Kwa mfano, Rosebud Kurwijila kumbe anatoka kijijini kwangu, hata sikuwa namfahamu. Lakini inaelekea CV yake ilipofika kule ilitisha na alichaguliwa bila yeye kuwepo. Kwa hiyo, wapo wengi Zanzibar, Mafia, Kibaha, Morogoro, Rufiji na kila mahali wapo na hii ndiyo raslimali ya kwanza ya nchi yetu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, napenda nianze kwa kuipongeza Serikali. Upo wakati tunasahau, hasa sisi Wana-CCM hii ni Serikali yetu. Uwezo wa kuiunda na kuitengeneza tunao. Mimi kama mwalimu *by profession*, ni dhambi kubwa kama mtu akifanya vyema kutompa *tick*. Sisi tunatumia alama mbili *X* na *V (tick)*. Pale anapofanya vizuri unaweka tiki, pale anapofanya vibaya hata akiwa mwanao wa kuzaa unaweka nini?

**WABUNGE FULANI:** *X*.

**MHE. BALOZI GETRUDE I. MONGELLA:** Hivyo, mimi ninaanza na hii tiki na ni *psychological*. Mtu akifanya vizuri ukaanza kumwambia mabovu unamkatisha tamaa. Kwa hiyo, niwaambie kwanza yale mazuri.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Chama cha Mapinduzi tungekuwa mpirani tungeingiza magoli mengi tu na nadhani tukifika mwakani tutakaposimama kwenye ulingo tuna sababu ya kujivuna kwa baadhi ya mambo ambayo tumeyafanya. Tumefuta kodi, tumeanzisha mradi mzuri tu wa elimu (MEM), tutakwenda kwenye MMES, tumejenga Shule za Msingi kwa ku-*mobilize* Wananchi, tumetengeneza barabara, tumeweka uwazi pesa siku hizi tunapata kutoka kwa Waziri moja kwa moja yaani tunajua pesa gani imekwenda wapi, tunajenga visima vya maji na kadhalika. Kuna vitu vingi ambavyo ni lazima tutembeke kufua mbele. Hizo ni tiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukiwa mwalimu mzuri usisahau kuangalia *crosses* ili uweze kumsaidia huyo mtu kujijenga vizuri zaidi. Kwa hiyo, nakuja kwenye *crosses*, lakini nataka niziweke katika mantiki ambayo nadhani itatusaidia kwenye maendeleo ya nchi hii. Nchi hii tuko katika jamii ya Watanzania kwa hiyo ni lazima tuangalie mahitaji ya Watanzania. Lakini tupo pia katika jamii ya Afrika Mashariki, kwa hiyo ni lazima tujenge uchumi utakaoweza kushindana katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Sisi pia ni Wanajumuiya wa Nchi za Kusini mwa Afrika, lazima tujenge uchumi utakaoweza kutupa nafasi nzuri katika Jumuiya ya Kusini mwa Afrika. Sisi ni Wanajumuiya wa Afrika nzima, ni lazima uchumi wetu ulenge pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, juzi tulipokuwa tunatoka Libya tukiwa na Mheshimiwa Remidius Kissassi, Mbunge wa Bunge la Afrika, tulikwenda kwa shughuli za Bunge letu. Wakati ndege inaanza kutua walisema sasa tunakaribia kutua, nikatazama nje, tulikaa safu moja na Mheshimiwa Remidius Kissassi, nilipotazama nje nikamwambia Mheshimiwa Remidius Kissassi, hee, haya ni matusi. Akaniuliza kitu gani Mama Mongella? Nikasema unaona kulivyo kwa kijani? Kule ni jangwa, watu hawana maji, watu ni wachache, wana mafuta tu! Sasa mimi nikasema hivi tukiweka pamoja dhahabu, almasi, ardhi, maji safi yasiyo na chumvi ya maziwa matatu na mito, hatuwezi tukafanya wanachokifanya wale kwa mafuta tu? Hivi mafuta na dhahabu kipi ambacho kina bei? Nikasema, hapa kuna kasoro. (*Makofi*)

**WABUNGE FULANI:** Kubwa.

**MHE. BALOZI GETRUDE I. MONGELLA:** Hiyo ni *cross*. (*Kicheko/Makofi*)

Kwa hiyo, hiyo ni *homework* kwa Serikali ambayo ndiyo inatusaidia kupanga. Sisi walimu ukishaweka *cross* mtoto unamwambia kasahihishe. Naomba Serikali ikasahihishe ile *cross* tuweke *tick*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika jangwa lile wameweza kukusanya maji kuwekwa kwenye bwawa moja na wanayasafirisha nchi nzima. *Types* zile ni *diameter* ya mita nne wanasafirisha na sasa wanataka kusambaza, wana mwelekeo wanajua wanachokifanya kila dakika. Sasa mimi natoka Ukerewe, bado tunachota maji ya ndoo. Maji ya kutoa tu ndani ya bwawa alilotupa Mungu ukasambaza ndani ya Wilaya nzima tumeshindwa!

Mheshimiwa Spika, ninajua Waziri wa Maji ni makini, hilo suala atalisahihisha. Kutoa tu kwenye bwawa bado! Afadhali hata Dodoma unapaswa kuyatafuta, lakini na Dodoma yapo chini ndiyo yaliyotumika Libya kuweka lile bwawa, yapo chini mita kidogo tu. *Level* ya maji hapa ni ndogo. Sasa tukiweka akili yetu pamoja na tukifanya ile *combination* ya kusema hivi kama wa mafuta tu wamefika hapo, sisi wenye dhahabu, almasi, minofu ya samaki na gesi ya Songo Songo tunashindwa nini? Kwa hiyo, tukae chini, tuwaheshimu wataalam wetu tulionao katika nchi hii, tuwaenzi, wanaweza wakaifanya hiyo kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kulisemea ni kwamba, nadhani tuna tatizo la uwezo wa kufikiri na kubuni na tusipoambizana kweli haitusaidii. Nasema mimi leo nazungumza kama mwalimu, mwanafunzi nikizungumza naye namwambia una tatizo la kuumba 'O' hachukii. Tuna tatizo la kufikiri na kubuni na haya makaratasi tuliyonayo hapa nina mashaka kama yote tumeyabuni sisi. Ninataka nisahihishwe kama mipango yetu ya maendeleo tumeibuni sisi. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijamaliza muda wangu, kuna masuala mengine yanatusumbua bila sababu. Hapa tunazungumza mambo mengine ambayo ni ya kukubaliana tu kama waungwana. Hivi mrabaha una tatizo gani? Mrabaha wa watu wa dhahabu na madini mengine una tatizo gani ndugu zangu? Mrabaha wa wanyamapori upo, mrabaha wa chokaa upo, mrabaha sijui wa vitu gani upo. Vitu ambavyo mtu yeyote hata mwananchi wa kawaida akitusikiliza tunalalamika juu ya mrabaha atasema hivi hawa Wabunge vipi, wanashindwa mrabaha wa dhahabu wanaweza mrabaha wa chokaa! (*Makofi*)

Mimi natoka katika eneo ambalo linachangia kwa asilimia kubwa sana minofu ya samaki. Kwa nini Wananchi wale wanaoshinda majini, wanalala majini, wanapoteza maisha yao wasipate mrabaha wa mali yao? Ni kwa nini hiyo *retention* isiwafikie wao? Wao wamekulia majini, wameolewa majini, wanaishi majini, wananyimwa tu *retention* ya kuweka pale waweze kuendeleza shule zao, watoto wao waweze kusoma, kwa nini? Kwa suala hilo tunajitakia matatizo. Tunataka tuwachanganye akili Wananchi kama kuna tatizo. Mimi tatizo la mrabaha silioni, *unless there is a hidden agenda*. Kama hakuna kitu hapa katikati, mrabaha wa madini hauna matatizo hata kidogo.

Ndugu zangu walioko Serikalini tunaomba mlitatie hilo, sisi twende kwa usalama, twende kwenye uchaguzi wetu salama tuendeleo na amani yetu wa chokaa wapate, wa dhahabu, almasi na vitu vingine wapate, wa samaki wapate na kila mtu apate. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nadhani baada ya kusema hayo, mambo ya mrabaha yasifanywe kama vile kuna mizengwe mizengwe, kwa nini watu wasipate? Kwa nini tusiimarisha kuondoa umaskini kwa kuwapiga jeki na mali waliyonayo miaka yote? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda niishie na nimalizie kwa kusema kwamba, kama tutataka kusonga mbele, lazima tuimarisha wafanyakazi. Serikali ilishatoa ahadi ya

wafanyakazi kufikia mshahara wa kima cha chini Sh. 80,000/= na iende kwa awamu ya mwaka 1995/96, 1996/97, 1997/98 na 1998/99, lakini hatujafanya. Tukienda kwa kasi hii haitatekelezwa mpaka 2008, tutakuwa tumekiuka ratiba yetu ya utekelezaji. Katika kuleta maendeleo ni lazima uzingatie maamuzi yako na yaende kwa ratiba ndiyo tunapata maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunajenga Shule za Sekondari, tunajenga Shule za Msingi, lakini hatutaki kuwarudishia walimu *allowances* zao. Hawa ndiyo wasimamizi wakuu wa MEM, ndiyo wame-*supervise* ujenzi wa shule hizi. Pale mlipokuta walimu wazuri na madhubuti kama katika Wilaya ya Ukerewe, shule zimejengwa vizuri. Ndugu yangu huyu hapa Mheshimiwa Esther Nyawazwa alikuwa kule, alifikiria Ukerewe ni kama tunajenga Vyuo Vikuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, walimu wale ndiyo walikuwa pale siku zote unawakuta wanasimamia ujenzi wa shule hizi japo wachache wamedokoa na ningepomba Serikali iwe macho, wale wote wanaodokoa hela za Serikali wafungwe. Kila siku wakitudokolea, *DEDs*, waweka hazina eti tunaambiwa Madiwani ndiyo tuwashughulikie, kwa nini Serikali isishughulike? Fukuzeni tulateeni watu wengine. Wapo vijana wanatangatanga wamemaliza Chuo Kikuu hawana ajira. Tulateeni hao vijana, wale kama wamechoka waondoke, wanasumbua watu wa *Local Government*. Akimaliza kuchafua Ukerewe anapelekwa Misungwi, akitoka Misungwi atapelekwa Kongwa, wanazungushwa tu wanakuwa *recycled!* Toeni watu wanaorudisha nyuma maendeleo. Serikali yetu ni makini, walioko pale mbele wamejitahidi katika Wizara mbalimbali, wanaowarudisha nyuma ndiyo wale watendaji katika *Local Government* na sisi Wabunge kama Madiwani, hatupendi kugombana na wale mnaotuletea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga hoja mkono. (*Makofi*)

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ABDULKARIM E.H. SHAH:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua nafasi hii kuungana na wasemaji waliopita kuwapa pole Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na baba yao. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi, *amin*.

Pia napenda kuwapa pole wenzetu Mheshimiwa Anne Kilango Malecela na Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa masaiibu yaliyowafika, Mwenyezi Mungu atawaponyesha haraka.

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumpongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba, kwa bajeti nzuri inayotoa fursa kubwa katika jitihada zetu za kuinua uchumi na kuondosha umaskini.

Nimefarijika sana baada ya kuipitia bajeti ya mwaka huu wa fedha na kuona kwa mara ya kwanza Serikali imeanza kutilia mkazo sekta ya uvuvi katika jitihada za kuinua uchumi na kuondosha umaskini hasa kwa jamii za wavuvi ambao kwa bahati mbaya ndio

maskini zaidi. Kwa kuwa sekta hii ni muhimu sana katika jitihada zetu za kuinua uchumi na kuondosha umaskini na mimi naamini hivyo, napenda kujua je, sekta hii imeliingizia Taifa kiasi gani cha fedha katika kipindi cha mwaka 2002/2003?

Mheshimiwa Spika, naamini kuwa Taifa letu lingeweza kupata fedha nyingi zaidi kama tungeweza kudhibiti kikamilifu shughuli na mazao yatokanayo na uvuvi pamoja na kuziba mianya inayoweza kutoroshwa kwa mazao hayo nje ya nchi kupitia kwenye mipaka yetu na hasa kwenye bahari kuu ambako kuna taarifa za utoroshwaji mkubwa wa mazao hayo. Kwa kuwa tumedhamiria kwa dhati kuinua uchumi wetu na kuondosha umaskini kwa wananchi wetu, basi Serikali na wananchi wote kwa ujumla hatuna budi kuhakikisha udhibiti wa raslimali zetu kikamilifu ili zituletee maslahi zaidi.

Mheshimiwa Spika, hili litawezekana pale tu ambapo tumeweka miundombinu inayohitajika.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa kukosekana miundombinu husika kama vile Bandari ya Uvuvi (*Fishing Port*) na meli za kisasa za kufanyia doria na udhibiti katika bahari kuu, huenda ikawa ni sababu kubwa sana ya Serikali kushindwa kudhibiti ipasavyo raslimali za bahari.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Fedha na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, hawaoni kuwa sasa ni wakati muafaka wa sehemu iliyokuwa ikitumiwa na Shirika la Uvuvi la Tanzania (*TAFICO*), itumiwe na Serikali ili kupanuliwa na kuanzishwa kwa Bandari ya Uvuvi ili kuhifadhi samaki kabla ya kusafirishwa kwenda nje ya nchi?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa na bandari ya uvuvi (*Fishing Port*), Serikali kupitia Wizara zinazohusika zitaweza kupata takwimu za uhakika za kiasi cha samaki kinachovuliwa na kusafirishwa nje ya nchi kutoka katika bahari kuu, Serikali itapata mapato zaidi ya ushuru wa mazao husika kwani kutakuwa na udhibiti zaidi, mamlaka tofauti kama vile Bandari na Taasisi nyingine zitapata mapato kwa kutoa huduma husika na pia Wananchi wengi zaidi watapata ajira kwa kuajiriwa moja kwa moja au kuajiriwa katika taasisi zinazotoa huduma katika meli hizo.

Mheshimiwa Spika, vile vile Wakulima wetu wa mboga mboga na bidhaa nyingine pia wanaweza kupata soko la mazao yao kwa kuzihudumia meli zitakazokuja kuleta samaki au kutia nanga katika bandari hizo, huenda ikawa chachu ya kufunguliwa viwanda vingi vya kusindika minofu na hivyo kutoa ajira kwa watu wengi zaidi. Taasisi za utafiti na Vyuho Vikuu pia zinaweza zikapata baadhi ya viumbe adimu na hivyo kusaidia utafiti Tanzania.

Mheshimiwa Spika, utaona kuwa kwa Serikali kuamua kulirudisha eneo hilo na kufanya bandari ya uvuvi, inaweza ikawa chachu ya mambo mengi katika kuinua uchumi na kuondosha umaskini.



Serikali pia inaweza ikatumia baadhi ya Bandari zake kama Tanga, Mtwara na Zanzibar, kuanzisha Bandari ya Uvuvi ili kuiwezesha Serikali kupata mapato zaidi na kutoa ajira kwa wananchi wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tunazungumzia kuondosha umaskini ni lazima basi Serikali ifikiri ni jinsi gani itawezesha kupatikana kwa ajira kwa Mheshimiwa Spika, hili litawezekana pale tu ambapo tumeweka miundombinu inayohitajika.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa kukosekana miundombinu husika kama vile Bandari ya Uvuvi (*Fishing Port*) na meli za kisasa za kufanyia doria na udhibiti katika bahari kuu, huenda ikawa ni sababu kubwa sana ya Serikali kushindwa kudhibiti ipasavyo raslimali za bahari.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Fedha na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, hawaoni kuwa sasa ni wakati muafaka wa sehemu iliyokuwa ikitumiwa na Shirika la Uvuvi la Tanzania (*TAFICO*), itumiwe na Serikali ili kupanuliwa na kuanzishwa kwa Bandari ya Uvuvi ili kuhifadhi samaki kabla ya kusafirishwa kwenda nje ya nchi?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa na bandari ya uvuvi (*Fishing Port*), Serikali kupitia Wizara zinazohusika zitaweza kupata takwimu za uhakika za kiasi cha samaki kinachovuliwa na kusafirishwa nje ya nchi kutoka katika bahari kuu, Serikali itapata mapato zaidi ya ushuru wa mazao husika kwani kutakuwa na udhibiti zaidi, mamlaka tofauti kama vile Bandari na Taasisi nyingine zitapata mapato kwa kutoa huduma husika na pia Wananchi wengi zaidi watapata ajira kwa kuajiriwa moja kwa moja au kuajiriwa katika taasisi zinazotoa huduma katika meli hizo.

Mheshimiwa Spika, vile vile Wakulima wetu wa mboga mboga na bidhaa nyingine pia wanaweza kupata soko la mazao yao kwa kuzihudumia meli zitakazokuja kuleta samaki au kutia nanga katika bandari hizo, huenda ikawa chachu ya kufunguliwa viwanda vingi vya kusindika minofu na hivyo kutoa ajira kwa watu wengi zaidi. Taasisi za utafiti na Vyuho Vikuu pia zinaweza zikapata baadhi ya viumbe adimu na hivyo kusaidia utafiti Tanzania.

Mheshimiwa Spika, utaona kuwa kwa Serikali kuamua kulirudisha eneo hilo na kufanya bandari ya uvuvi, inaweza ikawa chachu ya mambo mengi katika kuinua uchumi na kuondosha umaskini.

Serikali pia inaweza ikatumia baadhi ya Bandari zake kama Tanga, Mtwara na Zanzibar, kuanzisha Bandari ya Uvuvi ili kuiwezesha Serikali kupata mapato zaidi na kutoa ajira kwa wananchi wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tunazungumzia kuondosha umaskini ni lazima basi Serikali ifikiri ni jinsi gani itawezesha kupatikana kwa ajira kwa vijana wetu ili kuitumia nguvu kazi iliyopo kwa manufaa zaidi na hili huenda likawa ni moja kati ya mambo tunayoweza kufanya.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo iliweza kuwasaidia wakulima walio na uwezo wa kati kuwatolea ruzuku kwa matrekta aina ya *POWERTILLER* kwa asilimia hamsini. Matrekta hayo yalipokuja yalikuwa yanauzwa shilingi milioni tano, hivyo wakulima hao waliweza kuyapata kwa kulipa shilingi milioni mbili na laki tano na Serikali kutoa ruzuku ya milioni mbili na laki tano iliyobaki.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano huo, naamini kabisa kuwa pia Serikali inaweza kwa kupitia Wizara husika (Wizara ya Maliasili na Utalii), kupitia Idara yake ya Uvuvi, kuwasaidia wavuvi wa Ukanda wa Pwani ya nchi yetu hususan wavuvi wa Mafia, kwa kutoa ruzuku pia kwa vifaa vya uvuvi kama mashine, nyavu na vyote vinavyohusika na shughuli za uvuvi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda pia kuishauri Serikali ianzishe mfuko maalumu kwa ajili ya kuwasaidia wavuvi wadogo wadogo kama inavyofanya kwa mazao au sekta nyingine zilizokuwa muhimu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo pia nisiache kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa ushindi wa kishindo na Chama cha Mapinduzi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, sina budi baada ya kusema hayo, kuunga mkono hoja hizi mbili kwa asilimia mia moja.

**MHE. COL. FETEH SAAD MGENI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa sina budi kutoa shukrani zangu za dhati kwa kupata nafasi hii ya kuchangia machache katika bajeti hii. Aidha, nazishukuru Wizara zote mbili yaani Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsihaji na Wizara ya Fedha, kwa hotuba zao nzuri na za kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, naipongeza bajeti hii kwa vile imeelekea zaidi kwa wananchi kwa nia kuu ya kupunguza umaskini. Aidha, imepunguza ushuru kwenye maeneo ya *passport*, leseni ya biashara na kadhalika. Naipongeza sana kwa mpango mzuri wa kupanua nyanja mbalimbali za uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kufikiria na kusaidia wastaafu waliolipwa kwa mkupuo na sasa kuanza kulipwa tena pensheni zao, hiyo itasaidia kupunguza umaskini kwa baadhi ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, cha kutahadhari ni kuzidi kuangalia kwamba bado bajeti ni tegemezi kwani bado tunategemea msaada kutoka nje na mikopo, jambo ambalo ni hatari kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ni vema tukapania kikweli kweli katika kutumia raslimali yetu ya ardhi kwa kilimo cha kisasa. Aidha, tuitumie isapavyo bahari yetu ya Hindi na Ziwa letu la Victoria katika uvuvi wa kitaalamu.

Mheshimiwa Spika, endapo tutazitumia vizuri raslimali hizo ambazo ni utajiri mkuu aliotupa Mwenyezi Mungu, tutafaidika. Lazima tuimarisha viwanda ya minofu ya samaki, tuimarisha kujenga viwanda vya nafaka na kuimarisha kujenga viwanda ya madini, ambapo nchi yetu ni tajiri katika malighafi ya madini mbalimbali. Kuendelea kutumia umeme kwa mitambo ya mafuta kwa kweli ni kuendelea kujiua kiuchumi. Nadhani umefika wakati sasa kutumia nishati yetu ya gesi pamoja na makaa ya chuma na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, upoteaji wa fedha nyingi nao pia unaangamiza sehemu kubwa ya uchumi wetu. Ninaomba sana tuwe wakali sana kwa upotezaji wa fedha za Taifa, lazima kwa kila mhusika aangaliwe vizuri na kurejesha fedha ya Serikali. Lazima tuelewe kwamba, wale wafadhili wetu tunawavunja moyo na si rahisi kutuelewa.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kuwapongeza tena Mawaziri wote wawili, pamoja na watendaji wao wote, kwa kazi nzuri waliyoifanya. Naipongeza bajeti ni nzuri na inaonyesha matumaini makubwa ya kujinasua katika uchumi endapo tutapania kikweli kweli kuitekeleza.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa, naunga mkono kwa dhati hoja zote mbili zinazohusu bajeti. Ahsante.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa bajeti nzuri ambayo kweli lengo lake ni kuwapeleka Watanzania mbele kwa kuongeza kipato hasa cha wakulima.

Mheshimiwa Spika, niendeleo kumpongeza kwa kutoshusha bei ya malighafi ya mafuta ya kula kwa ajili ya wakulima wetu wa alizeti.

Mheshimiwa Spika, pamoja na bajeti nzuri, isiposimamiwa na kupelekwa kwa walengwa, uzuri wote wa bajeti hautaonekana.

Mheshimiwa Spika, lengo zuri la kuwaondolea umaskini wananchi wetu ni kupitia njia bora za kilimo, barabara nzuri Vijijini na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, sasa umefika wakati wakulima wetu waanze kupata mikopo kutoka Benki kupitia Mashirika kama *PASS* ambalo linawasaidia wakulima kupata mikopo toka *CRDB*. Mikoa ya Morogoro na Iringa wakulima wamefaidika sana kupitia shirika hili, tunaomba mashirika mengine kama hili yaanzishwe ili kuwakomboa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuondoa kero kubwa ya pensheni kwa wastaafu. Sasa naomba mfikirie kuongeza mishahara ya watumishi na wale wa kima cha chini wafutiwe kodi.

Mheshimiwa Spika, nashauri mapato ya Halmashauri yaangaliwe upya maana mpaka sasa vyanzo vyao vingi vimechukuliwa na Serikali Kuu. Kama uwezekano upo, Serikali Kuu ianze kukusanya na kugawa asilimia kwenda Wilayani.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003 wakati wa bajeti, Mheshimiwa Waziri aliahidi kunitafutia jenereta kubwa kwa ajili ya Hospitali ya Iambi Inkungi ambayo inapanuliwa na wafadhili na mpaka sasa umeme wa Gridi ya Taifa haujafika.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na watendaji wengine wote.

**MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba Wizara ishirikiane na Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo ili kutenga fedha za Mradi wa Maji wa Mbwinji ambao unatazamiwa kutoa huduma za maji kwa ajili ya Miji ya Nachingwea na Masasi.

Mheshimiwa Spika, pili, naomba Shilingi milioni 45 zilizokatwa kwenye kasma ya maji ya Nachingwea Mjini wakati wa bajeti ya ziada zirudishwe ili tukamilishe mradi.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuchukua fursa hii kukipongeza Chama changu cha Mapinduzi, kwa ushindi mkubwa uliopatikana katika uchaguzi mdogo uliofanyika Bariadi Mashariki. Pia nampongeza Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kurudi tena Bungeni.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Kwanza kabisa maoni yangu yatahusu uundaji wa Kamati za Ukaguzi wa Fedha za Serikali. Mimi ningeshauri katika kuleta ufanisi zaidi ni bora kutafuta Wakaguzi kutoka kampuni binafsi tena kutoka katika Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki, namaanisha Kenya na Uganda ili kupata hali halisi ya ukweli na kuondoa hali ya kulindana.

Mheshimiwa Spika, pengo la kujitegemea ni kubwa hivyo tunapaswa tutumie zaidi Wachumi wetu na pia tutumie njia ya kuwashirikisha wananchi wetu walio wengi katika kuboresha na kukuza uchumi wetu kwa kasi. Hii ni pamoja na kuwashirikisha wasomi wanaomaliza Vyuo Vikuu na Vyuo vya Elimu ya Juu kwa kuwapa mikopo ya kuingia katika soko la uzalishaji badala ya kutegemea soko la ajira ambalo halina uhakika katika karne hii.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 23, mimi sikubaliani na lugha iliyotumika kwamba ufanisi na nidhamu vimeongezeka, baadaye tukaelezwa kwamba miradi ya Serikali inakwama kwa utekelezaji mbovu na kutokuwepo kwa mahesabu sahihi wakati wote. Kwa nini katika majukumu ya Serikali kama uwajibikaji haupo, uaminifu haupo, ufanisi na nidhamu utatokea wapi. Hivyo bado watendaji wakuu warekebishe makosa hayo ndipo hatua za maendeleo zitapatikana haraka na kwa kasi inayolengwa.

Mheshimiwa Spika, bado tuna kazi kubwa ya kujitegemea na bajeti yetu kuwa tegemezi, nahisi kutokana na hilo lazima tukae na wataalam wetu tuandae programu

maalum ya kilimo cha kisayansi. Uchumi wa nchi ya China upo katika hali nzuri sana, pamoja na kwamba idadi ya nchi hiyo ipo juu duniani lakini wameweza kubadili uchumi wao haraka sana na kuweza kujitegemea na kusaidia Mataifa mengine duniani. Hii inatokana na kilimo cha kisayansi na watu kufanya kazi kwa bidii na uhakika.

Mheshimiwa Spika, Balozi Sato, alipotuaga Watanzania wakati alipomaliza kufanya kazi Tanzania alisema: "Watanzania uchumi wa nchi hii utabadilika ghafla pindi tu mkitumia ardhi yenu nzuri mliyonayo." Hivyo, maneno kama hayo tunapaswa kuyanukuu kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, katika dunia hii ya leo, umeme ni uchumi hivyo suala la mkaa wa mawe lizingatiwe kwa kufanyiwa kazi. Ahsante.

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 18 suala la *NEPAD* limetajwa. Katika habari hiyo imeelezwa kwamba, nchi 15 zimejiunga na mpango wa *Peer Review Mechanism*, lakini haikuelezwa kama Tanzania imeshasaini au la. Najua kwamba Tanzania bado haijajiunga, kwa nini? Kama tunajivunia Utawala Bora na misingi mizuri ya kusimamia uchumi, sasa tunaogopa nini kuwa-reviewed? Aidha, bado hatujasaini *AU Convention on Corruption* kwa nini? Tunaogopa nini kama tunadai rushwa nchini inadhibitiwa?

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 27 - 28, suala la mipango ya nchi za *SADC* kukabiliana na upungufu wa chakula limezungumzwa. Ninashauri kuwe na uratibu wa karibu wa kutekeleza mipango hiyo, la sivyo, tutajikuta tunaitisha mkutano mwingine wa Wakuu wa *SADC* kabla haya yaliyoamuliwa hayajatekelezwa. Suala la *Food Security* ni very critical.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 42 - 43, kuna huu mpango wa *Creation of Comprehensive Urban Land Property Register for Economic Empowerment of Residents in Unplanned Settlements in Dar e sSalaam*. Ninaisifu sana programu hii, ni muhimu sana katika kukomboa watu maskini, wenye nyumba maeneo yasiyopimwa Mijini. Lakini hatukuwa na haja ya kumngojea Bwana Hernando De Soto aje atufundishe. Wengine kwa miaka kadhaa tumekuwa tukilizungumzia suala hili Bungeni ingawa tulikuwa tunaliita *Regularization of Property Rights*. Aidha, *UCLAS* wameshatekeleza mradi huu huko Mwanza - Isamilo na Ibungulo, hivyo tuna uzoefu na wataalam. La muhimu kweli hizo bilioni 3.2 zitengwe.

Mheshimiwa Spika, nilipochangia kwa mdomo kuhusu kunyang'anya mapato Serikali za Mitaa, sikuwa na maana kodi/ushuru wa kero usiondolewe, lakini badala ya kutoa ruzuku kufidia, Halmashauri hizi zingepewa vianzio mbadala ili ziwajibike kukusanya mapato na kutumia. Kwa mfano, ushuru wa leseni wote (unaoitwa wa Kitaifa na Kimataifa), ungeachiwa Halmashauri zikusanye badala ya Serikali Kuu. Aidha, Kodi ya Viwanda (*Land Rent*), ingekusanywa na kubakizwa yote kwenye Halmashauri badala ya asilimia 80 (Dar es Salaam ni 100) kupelekwa Wizara ya Ardhi.

**MHE. MASOUD ABDULLA SALIM:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda na Mheshimiwa Basil Mramba, Manaibu wao na wataalam wao, kwa kuleta mbele yetu hoja za bajeti zao.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nataka nianze na suala zima la elimu, taratibu za elimu ya lazima kuishia Darasa la Saba ni tatizo kubwa kwani vijana wanapomaliza masomo yao hayo huwa ni wadogo sana kiumri na huwa hawana la kufanya hivyo kubakia vijiwani, kujitumbukiza kwenye uvutaji wa bangi na hata madawa ya kulevya na hatimaye maambukizo ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna idadi kubwa ya wanafunzi waliomaliza Darasa la Saba ambao hawataleta mapinduzi yoyote ya maendeleo, ninaishauri Serikali, Elimu ya lazima iwe la Darasa la Kumi na Mbili (*Form IV*), angalau umri huu utawawezesha kupambanua mambo ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, walimu nao ni vema wawezeshwe vizuri juu ya kuangalia upya mishahara yao kwani kiwango cha sasa ni kidogo mno hasa ukutilia maanani Walimu wengi hufanya kazi nje ya Wilaya zao na hata Mikoa yao. Ni vema Serikali ikawakopesha vipando vya usafiri kama vile pikipiki, lengo ni urahisishaji wa kufika kazini mapema na kwa wakati. Katika hali ya kuboresha maisha ya walimu wetu ni vema Serikali ikawakopesha vifaa vya ujenzi kama bati, saruji na ni vema mikopo hiyo iwe ya bei nafuu. Usumbufu wa kufuatilia mishahara Wilayani ni vema urekebishwe kwani wakati mwingine walimu hubakia Wilayani siku mbili na hii inachokesha sana.

Mheshimiwa Spika, kilimo kama uti wa mgongo wa uchumi wetu lakini bado kilimo kimebakia ni sekta iliyokuwa haijapewa umuhimu unaostahili. Umaskini umekithiri Vijijini kutokana na ulimaji wa kilimo cha kubahatisha kisichokuwa cha kitaalam.

Mheshimiwa Spika, tatizo la mbolea kuwafikia wakulima limepelekea kwa kiasi kikubwa, kupungua kwa mavuno ya mazao ya biashara na ya chakula. Mbolea ambayo Serikali iliahidi kupeleka Wilayani haikupeleka kwenye maeneo mengi ya Wilaya na Wilaya zilizopata mbolea ilikuwa ni ndogo sana, chini ya asimilia 50 ya mahitaji. Naishauri Serikali kupeleka mbolea Mawilayani haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nchi yetu ilikumbwa na uhaba wa mvua (ukame), hivyo ni vema Wizara husika kupitia wataalam wake, kuanza kutoa elimu juu ya uvunaji wa maji ya mvua pale ambapo mvua hunyeshwa au vinginevyo ili kuhifadhi na kutafuta njia ya kuyatumia kwa kuleta ufanisi zaidi katika kilimo. Ninaishauri Serikali kuangalia upya kilimo cha umwagiliaji maji kwani Tanzania ina mabonde mengi yanayofaa kwa kilimo hicho na yanayotumika kwa umwagiliaji ni kasoro ya 10%. Hili likitekelezwa tutaondokana na aibu ya kukosa chakula na kubaki ombaomba.

Mheshimiwa Spika, maafisa ugani wawezeshwe ili wafanye kazi vizuri zaidi, ni vema Serikali ikaangalia upya mishahara na marupurupu pamoja na kuwapatia vipando vya usafiri, pikipiki na vyombo vingine vya usafiri.

Mheshimiwa Spika, rushwa bado ni kero na ipo ila tu Serikali ifahamu rushwa inapofanyika baina ya mtoaji na mpokeaji inafanyika kwa siri sana hivyo kauli inayotolewa na baadhi ya Viongozi wa Serikali kuwa utolewe ushahidi wa rushwa kama ipo, inaashiria bado Serikali haitaki kupambana na rushwa kwa dhati kabisa ila ni ubabaishaji tu kwani Serikali inafahamu mianya inayopelekea rushwa.

Hivyo, Serikali ni vema ikavitumia vyombo vyake kudhibiti rushwa, kukaa kitako bila woga kutoa taarifa kamili za rushwa hata kama kuna wakubwa basi kuwe na uwazi wa utambuzi wa watu hao.

Mheshimiwa Spika, ushahidi wa rushwa ni jinsi baadhi ya watu walivyojilimbikizia mali isivyo halali juu ya kipato chao.

**HAMISI J. NGULI:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kuchangia hoja yangu, naomba niwapongeze sana Mawaziri wote wawili kwa kazi yao nzuri ya kusimamia uchumi wetu ambao sasa unatuletea matumaini makubwa ya kukua.

Mheshimiwa Spika, bajeti hii ni nzuri na sasa ina mipango ya kumwondolea mwananchi umaskini wa kipato. Tatizo langu katika bajeti hii ni kodi ya ukodishaji wa ardhi ya kutumia kwa kilimo. Nashukuru kuwa kodi hiyo ilipungua toka shilingi mia sita kwa eka mwaka 2003 na kuwa shilingi mia mbili na kumi kwa eka. Lakini je, wakati sasa tunataka kilimo kiendelezwe na tunaweka mazingira mazuri ili wananchi wengi wapende na wawekeze katika kilimo, kuna haja gani ya kuendelea na kodi hii ya ardhi? Sidhani kama hata Serikali inapata fedha ya kutosha na hivyo kuifanya kodi hii kama chanzo cha mapato.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri wa fedha aiondoe kodi hii au kama haiwezekani kuondolewa kabisa basi ibaki kiasi kidogo kitakachovutia wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja zote mbili.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Spika, moja ni kuhusu mgao wa asilimia 4.5 kwa Zanzibar. Iko haja ya Serikali ya Tanzania kuangalia upya mgao wa misaada kutoka nje hasa kwa upande wa Serikali ya Zanzibar na hasa kwa kuzingatia umaskini wa Serikali ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, pili ni kuhusu nyongeza ya fedha kwa vyombo vya ulinzi. Tunaitahadharisha Serikali juu ya nyongeza ya bajeti kwa vyombo vya dola isije ikatumika katika kuwadhibiti na kuwanyanyasa Wapinzani wakati wa uchaguzi mkuu wa nchi mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, tatu ni kuhusu huduma ya *TRA* kwa Zanzibar. Serikali kupitia Wizara ya Fedha, iangalie upya utendaji wake wa kazi katika shughuli zake za ukusanyaji wa mapato kwa upande wa Zanzibar kwani kumekuwa na malalamiko mengi kwa wafanyabiashara wa Zanzibar kuhusu utendaji kazi wa *TRA* Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, tatu ni kuhusu uwekezaji katika sekta ya madini. Madini ni sekta muhimu katika nchi nyingi duniani ambayo huingiza fedha za kigeni. Hapa petu sekta hii haionekani kuwa na umuhimu sana katika maendeleo ya nchi yetu. Sasa ni wakati muafaka wa Serikali kuliangalia suala hili la madini kwa undani zaidi ili liweze kuleta tija kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ya Tanzania kupitia *TACAIDS* kufikiria kuwasaidia watoto yatima ambao wameachwa na wazazi wao ambao wamekufa kwa Ugonjwa wa UKIMWI.

**MHE. STPHEN M. KAHUMBI:** Mheshimwa Spika, wakati nikichangia asubuhi niliweka mezani tarifa tatu: Kwanza, malalamiko ya Ndugu Maulidi N. Rayega, ambaye anadai kulipwa fedha kwa bima zake tatu zilizoiva lakini *NIC* wanaonekana kuzembea. Pili, malalamiko ya Bibi Agness S. Mkemwa, aliyerejeshwa kazini kwa amri ya Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, lakini Uongozi wa *TRA* ukafanya vinginevyo. Tatu, malalamiko ya Bibi Phillipina Ngowi, aliyeahidiwa kupatiwa ufumbuzi wa tatizo lake tangu 15 Juni, 1998.

Tulizungumza na Ndugu Kitilya aliyenieleza kuwa anazo kesi saba za aina ya Bibi Mkemwa na akadai kuzishughulikia kwa pamoja. Wafanyakazi hawa wawili hawashtaki lakini wanaomba usaidie menejimenti iweze kuwarejesha kazini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ASHA A. NGEDE:** Mheshimiwa Spika, bajeti hii ya Wizara ya Fedha ambayo ni nzuri na ya aina yake kwa ubora ni katika suala la mgawanyo wa fedha kwa mwaka 2004/2005, katika sehemu ya kumi na mbili ukurasa wa 40 kuhusu fedha zaidi kwa chakula cha dharura endapo hali ya hewa itakuwa mbaya pamoja na kugharamia Mfuko wa Hifadhi ya Chakula (*SGR*).

Mheshimwa Spika, hakuna fungu la maana katika bajeti hii kama fungu hili la chakula cha dharura. Bila ya chakula hakuna binadamu anayeweza kufanya shughuli yoyote awe mwanafunzi, mkulima, mwalimu, mwanasiasa, daktari na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia Aprili, 2004, Bunge liliongeza siku zake za kukaa hapa Dodoma kwa ajili ya kupitisha bajeti ya njaa na hivyo ilibidi pia Bunge litumie fedha zaidi wakati ingekuwa imetumika fedha hiyo kwa ajili ya mambo mengine kwa ajili ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuchangia kifungu cha kumi na moja ukurasa wa 40. Ninaipongeza Serikali kwa kuongeza fedha kwa ajili ya vyombo vya ulinzi na usalama. Ni ukweli usiopingika kwamba, vitendo vya ujambazi vimeongezeka na vitendo vingine vya uhalifu. Hii inaonyesha Serikali inavyojali wananchi wake kwa usalama na pili Serikali inaonyesha jinsi gani inavyojiandaa kwa uchaguzi wa mwaka



2005 kwa sababu sio vyama vyote vyenye ustaarabu na hivyo basi inabidi Serikali kujiandaa kwa kuimarisha vyombo vya usalama.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchangia kuhusu pesa za UKIMWI. Pesa za UKIMWI hata Vyama vya Siasa pia vilipewa na hivyo ni mategemeo yangu, Vyama vya Siasa ndio vingekuwa vya kwanza kufanya marejesho na hasa Vyama vya Upinzani ili kuonyesha kweli wana dhamira ya kuipinga Serikali iliyopo madarakani.

Mheshimiwa Spika mwisho naunga mkono hoja.

**MHE. SAMWEL M. CHITALILO:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Fedha na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, kwa kutayarisha hotuba zao kwa umakini hasa ukizingatia bajeti ya mwaka huu inamlenga mtu wa hali ya chini.

Mheshimiwa Spika, ninayo machache ya kuzungumzia au kushauri katika bajeti hii. Pamoja na bajeti kuwa nzuri, amani nchini mwetu kiasi kikubwa imekwishaondoka hasa kwa maisha ya raia. Ukiangalia matukio ya ujambazi yanaongezeka kila kunapokucha.

Mheshimiwa Spika, ninapoandika hapa, ninayo masikitiko makubwa hasa kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani. Jimboni kwangu Buchosa watu wengi hujishughulisha na uvuvi. Lakini kila mara wamekuwa wakikurupushwa ziwani saa za usiku hata mchana, hunyang'anywa vifaa vyao vya uvuvi kwa nguvu. Nimekuwa nikilalamika mara kwa mara hapa Bungeni, lakini sipati msaada wa kutosha katika jambo hili. Ni juzi tu majambazi yalivamia na kupora *outboard engine*, mtumbwi na nyavu na tendo baya zaidi wakachukua mtu mmoja kati ya wafanyakazi watatu ndani ya mtumbwi na wakamtosa ziwani katika Kisiwa cha Maisome huku wamemfunga mikono nyuma na kumpotezea maisha yake. Matendo ya namna hii yamekuwa ya kila mara, je, kilio hiki nimpelekee nani?

Naomba kupitia bajeti yako, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, uwashauri hawa watu wa Wizara ya Mambo ya Ndani, watenge pesa maalum na kuweka doria katika maeneo haya ya Buchosa katika Visiwa vya Zilagula, Iyozu, Nyamango na Maisome na visiwa vyote vilivyopo Buchosa kwani vyote vinakaliwa na wavuvi. Wavuvi hawa wa Buchosa huzalisha zaidi ya tani hamsini za samaki kwa siku na uongeze Pato la Taifa katika uchumi.

Mheshimiwa Spika, naandika maneno haya nikithibitisha kuwa, amani Buchosa hakuna na maaskari walioko katika vituo vidogo vya Bupandwa na Nyakaliro mbali na maeneo ya wavuvi hawana silaha hata moja bali wana sare za Polisi tu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja zote mbili kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. ESHA H. STIMA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nachukua fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wawili, Mheshimiwa Basil P. Mramba na Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, kwa hotuba zao nzuri, walizowasilisha Bungeni tarehe 10 Juni, 2004. Mipango imeonyesha Dira ya Maendeleo kwa wananchi wa Tanzania hali kadhalika bajeti ya mapato na matumizi imeridhisha wananchi walio wengi. Kwa hali hiyo naunga mkono hotuba zote mbili mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kuhusu masuala ya kuboresha upande wa kilimo tuwe na kilimo cha umwagiliaji katika Mikoa yenye mito mikubwa, maziwa makubwa na madogo na mabonde, ili kukidhi kipato kidogo cha nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pili, ujenzi wa barabara, reli, mahitaji ya mawasiliano na nishati ni ufunguo wa maendeleo kwa wananchi wote, kwa hiyo, bajeti kubwa zielekezwe kwa Wizara husika ili zikamilishe shughuli hizo na wananchi waondokane na umaskini, vifo na elimu duni.

Mheshimiwa Spika, tatu, usimamizi wa madini ni dhuluma tupu kwa Mikoa yenye madini kwa sababu hawapatiwi huduma za kijamii kwenye Wilaya husika. Serikali irekebishe masharti inayotoa kwa wawekezaji wanaochimba madini yote nchini ili kuwepo na mwanja wa kutoa huduma kwa Halmashauri zetu na isiwe huduma katika eneo la machimbo. Kwa sababu kipato cha madini kinatumika kwa maendeleo ya nchi nzima, kwa nini Wilaya zenye madini zisifaidike na madini yao?

Mheshimiwa Spika, nne ni kuhusu UKIMWI. Serikali haijaamini kama ni janga kubwa na kwamba yote yanayopangwa hayatakuwa na mtu wa kuyatekeleza. Mipango ya kuteketeza janga la UKIMWI iko wapi? Fedha za kupambana na UKIMWI zimetengwa wapi?

Mheshimiwa Spika, naomba Waheshimiwa Mawaziri wafuatilie utekelezaji wa kazi kwa watendaji wao kama wanavyosimamia uandikaji wa hotuba nzuri wanazowasilisha Bungeni.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huu mdogo, narudia kusema kwamba, naunga mkono hoja zote mbili mia kwa mia.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika kwa kuwa Shirika la Elimu (*TES*), lilingia kwenye utaratibu wa *Voluntary Liquidation* na kwa kuwa shirika hilo liliacha/lilishindwa kufanya kazi kwa muda mrefu:-

Kwanza, je, Shirika hilo lilikuwa na madeni kiasi gani hadi lilipoingia kwenye utaratibu wa *Voluntary Liquidation*?

Pili, kwa kuwa shirika hilo lilikuwa na mali nyingi, hasa nyumba na *godowns* katika maeneo mbalimbali nchini na kwa kuwa mali hizo zilifanyiwa tathmini kupitia Chuo cha Ardhi mwaka 1992 na mali hizo sasa zimeuzwa chini ya bei iliyokuwa kwenye

tathmini. Je, Wizara inaweza kueleza ni hasara kiasi gani imepatikana kutokana na mali hizo kuuzwa kwa bei ya chini?

Tatu, je, kama imeuzwa kwa bei ya chini kuliko tathmini ilivyoonyesha nini kimesababisha hali hiyo?

Nne, je, kwa vile mgogoro wa wafanyakazi umedumu muda mrefu kwa madai ya kutaka kulipwa *golden hand shake* na kwa kuwa tuna taarifa kuna mashirika yamelipwa *golden hand shake* bila hata kuwa na Mkataba wa Hiari, Serikali inaweza kuliarifu Bunge hili ni mashirika mangapi yamelipwa bila Mkataba wa Hiari na ni kwa msingi upi Serikali imeshindwa na au imekataa kuwalipa wafanyakazi 117 wa *TES*, ubaguzi huu umesababishwa na nini?

Tano, tuna taarifa kuwa wafanyakazi hao waliondolewa kwa utaratibu usio wa kawaida wakati wamelinda eneo hilo kwa karibu mwaka mzima wakingojea ufumbuzi wa matatizo yao. Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu hali hiyo, ikizingatiwa kuwa Shirika liko chini ya *LART*?

Mheshimiwa Spika, nategemea kupata majibu ya kina, vinginevyo nitatumia utaratibu wa vifungu na hata kuleta maelezo binafsi (*Adjournment Motion*) ili kupata ukweli hasa kuhusu tatizo la wafanyakazi hawa ambao kwa dhahiri inaonekana wamedhulumiwa na kunyanyaswa baada ya kuhudumia Taifa lao, wengine kwa zaidi ya miaka thelathini.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DR. WILLIAM F. SHIJA:** Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 45 - 46 kuhusu marekebisho ya kodi kwa wakulima na wafugaji wadogo wadogo, nashauri uandaliwe Waraka mapema iwezekanavyo ili pasitokee kutofautiana baina ya maamuzi ya Bunge na matendo ya Halmashauri nchini.

Mwaka 2003, kama alivyosema Waziri wa Fedha kwenye hotuba yake kwamba: “Napenda kukumbusha kwamba, Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji, zina fursa ya kutoza kodi na tozo zilizo rodheshwa katika Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa kufuatia marekebisho yaliyofanywa mwaka 2003. Ninachosisitiza ni kwamba, kero ya kusumbua wanawake wauza mboga, ndizi, nyama, vitumbua na maandazi, lazima iondoshwe kabisa na Halmashauri zifuatiliwe katika kutii sheria na utaratibu huu.” Eneo hili linagusa watu wengi sana na ni nyeti.

Mheshimiwa Spika, narudia, Waraka unaohusu jambo hili uandaliwe mapema ili Waheshimiwa Wabunge tuondoke nao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja zote mbili.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, naomba kwa dhati kabisa, yafanywe mapitio ya Mikataba ya Madini. Hii ni kwa sababu ukweli

unaonesha faida ipatikanayo ni ndogo kuliko mategemeo ya wananchi. Aidha, ni bora uwepo uwazi zaidi juu ya uwekezaji wa sekta hii ili hii dhana ya baadhi ya watu kukatiwa kitu kidogo ifutike. Ni ukweli ulio wazi kuwa, *royalty* tupatayo haitoshi.

Mheshimiwa Spika, hili suala la mafuta hapa nchini likoje? Upo mgongano wa fikra kuwa mafuta yapo au hayapo! Ni bora Serikali itoe tamko na ufafanuzi mkubwa juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Taifa letu zaidi ya kueleza kwa ujumla juu ya gawio la asilimia 4.5 kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, lakini hatupati ufafanuzi juu ya kiasi gani cha gawio hilo kimefika SMZ katika kipindi fulani. Naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, alieleze Bunge kuhusu gawio kwa SMZ kwa misaada na mikopo kwa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika. *TTCL* ilipobinafsishwa waliahidi kuweka laini karibu milioni mbili kwa mujibu wa makubaliano ya Mkataba. Lakini hawakufanya hivyo, matokeo yake wenye simu za mikononi wameibuka wengi na wenye kampuni hizi wanajikusanyia faida kubwa wakati watu walio wengi wangeweza kunufaika na *TTCL* kama mtandao wake ungeenea hapa nchini. Ni vyema basi Serikali ikaliangalia suala hilo.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru na ninaunga mkono hoja zote mbili. Ahsante.

**MHE. BAKAR SHAMIS FAKI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nachukua nafasi hii kuwapa mkono wa pole Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na baba yao mpenzi. Mungu ailaze pema roho ya marehemu, *amin*.

Mheshimiwa Spika, nitaanza kuchangia hoja ya Waziri wa Fedha kwa kusema kwamba, Watanzania wamechoshwa na lugha nzuri inayotumiwa na Viongozi katika kufanikisha haja zao.

Mheshimiwa Spika, sote ni mashahidi kwamba, tunapopitisha Bejeti, huonekana mambo yaliyomo katika maelezo ni mazuri tu lakini utekelezaji na usimamizi haupo, ambapo hili linaashiria mapungufu makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa ninavyoona mimi, Bajeti ya safari hii zaidi imeegemea sana upande wa siasa kuliko katika kuleta maendeleo. Nasema hivyo kwa sababu itakuwaje vyombo vya ulinzi viwekewe fedha nyingi zaidi hasa hasa ukizingatia kwamba, kutakuwa na Uchaguzi Mkuu mwakani (2005)? Huku ni kuifagilia CCM na kumdhaliisha Mpinzani.

Mheshimiwa Spika, haijaonyesha umakini katika kuondoa umaskini, kwani bado yapo manung'uniko mengi yanayoashiria kwamba, Serikali haijatoa msisitizo kamambe kuhusiana na suala zima la kutoa mbolea, pembejeo na mahitaji mengine kwa wakulima. Kama kweli Serikali inayo nia ya kuondoa umaskini, lazima iangalie upya suala la kuwapatia wakulima mbolea na pembejeo na kutilia maanani suala la kuondokana na ukulima wa majembe ya mkono.

Mheshimiwa Spika, Tanzania inapoteza fedha nyingi sana katika Sekta ya Madini. Ipo haja ya Serikali kuona kwamba, hii asilimia tatu inaongezeka angalau kufikia asilimia 20 kwa kuzingatia kwamba, baadhi ya nchi hapa Afrika kima chao ni zaidi ya 30%.

Mheshimiwa Spika, suala la rushwa (ufisadi), bado halijapigwa vita kama inavyostahili. Hapa pana nini, kwa nini Serikali haioni haja ya kulishughulikia suala hili ipasavyo? Malalamiko yapo kutoka kwa kila kundi la jamii ya Tanzania. Hivi Serikali inaweza kulieleza Bunge ni watu wangapi wametuhumiwa kuwa ni mafisadi na ni wanagapi wameshughulikiwa na kwa namna gani? Hebu Serikali jisafisheni, kuweni wakweli, msitake Waheshimiwa Wabunge wawataje wakati yote mnayafahamu.

Mheshimiwa Spika, bado uchumi wa nchi yetu ni tegemezi kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo, Serikali ione kwamba, sasa umefika wakati wa kuondokana na hili. Kwa kuwa utegemezi wa zaidi ya asilimia 40 ni hatari sana. Kwa hiyo, juhudi maalum lazima zichukuliwe.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**MHE. PROF. HENRY R. MGOMBELO:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze mchango wangu kwa kutoa rambirambi na pole kwa Waheshimiwa Wabunge wote, waliopata matatizo mbalimbali tangu Mkutano wa Kumi na Tano.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kuchaguliwa tena kuwa Mbunge wa Bariadi Mashariki.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja zote zilizo mbele yetu. Mchango wangu utakuwa katika kuboresha utendaji.

Mheshimiwa Spika, ili tuondokane na umaskini, juhudi zetu lazima ziende kwenye Sekta ya Kilimo, maana ndiyo sekta inayowahusisha Watanzania wengi. Tuondokane na utegemezi wa mvua maana nchi yetu imejaliwa na Mwenyezi Mungu kwa kuwa na mabwawa mengi, maziwa mengi na mito mingi. Vile vile tuna mabonde mengi ambayo tukiyatumia vizuri yanaweza kutulisha na kupata ziada ya kuuza nchi za nje. Kwa kweli ni aibu kuwa na upungufu wa chakula katika nchi yetu!

Mheshimiwa Spika, suala la dawa katika hospitali zetu ni la muhimu sana, hususan kwa wazee wetu. Hivi sasa wazee wetu ambao wanatakiwa kupewa dawa bure hawapewi kwa kisingizio kuwa hamna dawa, zimeisha! Serikali ilianganalie suala hili kwa umakini ili wazee wetu wapate matibabu yanayotakiwa. Siyo siri kuwa dawa za Serikali zinauzwa kwenye maduka binafsi. Nashauri kuwa pale inapowezekana, dawa za Serikali ziwekewe alama maalum kwa mfano, *T.G. (Tanzania Government)*.

Mheshimiwa Spika, gharama za umeme hasa kuunganisha ni kubwa sana, kiasi ambacho wananchi wengi hawawezi kumudu, jambo ambalo linasababisha kumalizika kwa misitu. Tuliangalie suala hili kwa umakini sana kwa maana ya kupunguza bei hizi.

Mheshimiwa Spika, sisi wananchi wa Tabora tunasubiri kwa hamu uanzishwaji wa Kituo cha Televisheni ya Taifa (TVT) mwaka huu. Naomba Serikali ituambie ni mwezi gani huduma hii itafika Tabora ili tujiandae kikamilifu?

Ninashauri zoezi la kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano (TCRA) lifanywe kwa uhakika ili Mamlaka hii iweze kushughulikia mambo ya kuanzisha Vituo vya Redio na Televisheni, vinavyosubiriwa kwa muda mrefu kama vile *CG FM Radio* na *Voice of Tabora* vya Tabora na kadhalika. Vile vile Mamlaka hii itashughulikia suala la gharama za kuunganisha simu za makampuni ya simu ili ipelekee upunguzaji wa gharama za simu.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti hii zimewekwa fedha za kuwalipa wale ambao ajira zao zitakoma, nashauri kuwa zoezi hili lifanywe kwa uwazi na mashauriano na wafanyakazi. Mashirika kama *THA*, *TRC*, Shirika la Posta na kadhalika ni nyeti sana na yanahitaji uangalifu mkubwa katika zoezi zima la kuyarekebisha.

Naiomba Serikali ikamilishe mapema zoezi la kuwapa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam yale majengo ya Kampuni ya Simu yaliyoko Chuo cha Posta Dar es Salaam. Majengo haya yamekaa bila kutumiwa kwa muda mrefu, kiasi ambacho yanaweza kuharibika. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kitayatumia majengo haya kwa manufaa makubwa ya Taifa letu kwa kufundishia wanafunzi wa uhandisi, kufanya utafiti na shughuli za ushauri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hizi mbili.

**MHE. REMIDIUS E. KISSASSI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kuwapa pole Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan na Mheshimiwa Mwaka Abraham Ramadhani, kwa misiba iliyowakuta ya jamaa zao, Mwenyezi Mungu awape subira. Vile vile napenda kuwapa pole Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere na Mheshimiwa Estherina Kilasi, kutokana na ajali za magari.

Ninapenda kuchangia machache katika hotuba nzuri zilizotolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na Waziri wa Fedha. Kutokana na mbinu na mikakati mbalimbali iliyoelezwa ya kukuza uchumi, mimi naiomba Serikali kufikiria mambo yafuatayo ya nyongeza:-

(a) Ujenzi wa Barabara Kuu za Kitaifa na Mikoa, kwa vile zinaigharimu Serikali fedha nyingi sana, napendekeza makandarasi wale wazuri, wenye sifa za ujenzi bora wa barabara, ambao wapo nchini kwa mfano, *NCC - Ahsleef* na kadhalika, basi waendeleo kupewa barabara nyingine wazijenge kwa *Negotiation Basis*. Hii inasaidia kupunguza urasimu mrefu wa kuitisha tenda upya, kupunguza gharama, kwa vile

*Mobilisation Costs* (15% - 30%) zitapungua sana na barabara nyingi zitajengwa kwa haraka zaidi na kwa bei nafuu na kadhalika.

(b) Napendekeza Mradi Maalum wa Kuchimba mabwawa na malambo nchi nzima ili tuondokane na aibu ya kutegemea kilimo cha mvua tu na ukiwepo ukame kidogo tu basi njaa au balaa linatokea. Nchi yetu imejaliwa mito, maziwa na mabonde, tuyatumie vizuri. Ni aibu kuwa mvua nyingi zinazonyesha zinaishia baharini.

(c) Sheria za uwekezaji katika madini ziangaliwe upya kwani zimekuwa zikiwanufaisha zaidi wageni kuliko wananchi. Wabunge washirikishwe kikamilifu kwenye hili kwa sababu kuna tuhuma kuwa baadhi ya Watendaji wameshiriki katika kuweka taratibu mbovu zinazotuumiza hivi sasa. Mfano, masuala ya *Tax Holidays*, *Capital Allowance*, fedha za madini ziwekwe katika mabenki yetu na wawekezaji wawe *encouraged* kukopa humu nchini, *Production Sharing Agreement and Windfall Profits* na *Royalties* na kadhalika.

(d) Kutokana na upandaji mkubwa wa bei za mafuta ya dizeli na petroli duniani umeathiri moja kwa moja bei hizo hapa nchini kwetu. Upandaji huu si mzuri hata kidogo hasa kwa vile una *direct effects* kwa walaji/watumiaji wa mazao na huduma. Hivyo ni muhimu sana Serikali ifanye *intervention* kwa mbinu yoyote ile ili wananchi wasiumie sana. Hivyo, naishauri Serikali iunde chombo ambacho kitadhibiti upandaji huu wa bei za mafuta la sivyo maumivu kwa wananchi wa kawaida yatakuwa makubwa mno.

Mheshimiwa Spika, naziunga mkono hoja zote mbili.

**MHE. ZAHOR JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naiomba Serikali kupitia upya mfumo mzima wa ubinafsishaji. Zoezi hili limelalamikiwa na Watanzania wengi na mimi pia naamini kuwa tuna upungufu mkubwa unaoleta wasiwasi kwa Watanzania wote. Hivyo ni vyema tukaangalia upya utiaji dhamana wa mashirika tunayobinafsisha, tunayempa kuendesha taasisi hiyo baada ya ubinafsishaji, mahusiano yake na jamii ya Kitanzania, matokeo ya ajira kwa Watanzania ukilinganisha na kabla ya ubinafsishaji, aina ya *technology* mpya itakayotumika, ajira mpya na tija kwa Taifa. Nina wasi wasi kuwa, upimaji wetu sio endelevu au tathmini sio sahihi na sio wazi kwa wananchi na matokeo yake ni kutoamini kuwepo kwa tathmini sahihi au dhana za kuwepo kwa rushwa hivyo ni lazima wananchi waondolewe hofu yao juu ya mali za Taifa lao zinavyotumika na watakavyofaidika nazo.

Mheshimiwa Spika, mwananchi wa kawaida kijijini anaposikia kuwa uchumi wa Taifa unakua, hujenga matumaini kuwa huenda ugumu wa maisha anaokabiliwa nao utapata ufumbuzi. Lakini katika mfumo wa kuwaendeleza Watanzania kiuchumi kwa sasa ni ndoto za mchana, uhalisi wa maendeleo ya Mtanzania utakuja pale Serikali itakapoanzisha mfumo wa kuiendeleza ardhi ili iweze kutumika kwa *irrigation* na baadaye kuiuza au kuikopesha kwa wananchi waiendeleze na pia kwa kuwakopesha mifugo, kazi za mabwana shamba zibakie ni kuendeleza na kusimamia kilimo na ufugaji

bora. Kinyume na hivyo, kuhimiza wafugaji na wakulima katika hali ya kilimo na ufugaji wa sasa ni kupoteza wakati na ni sawa na kuhimiza kazi ambayo haina tija.

Katika Hotuba ya Waziri wa Fedha, katika ukurasa wa 39, Mheshimiwa Waziri, amesisitiza kuendeleza utaratibu wa kuipatia SMZ, 4.5% ya jumla ya misaada inayopata Tanzania, hii ni kwa misaada ambayo haikujifunga moja kwa moja na miradi maalum. Hata hivyo, *percent* hii wakati ilipowekwa ilikuwa ni ufumbuzi wa muda tu kwa vile kwa wakati huo hapakuwa na utaratibu wowote hivyo, inashangaza na kusikitisha kuona kuwa ufumbuzi huo wa muda umeendelea kuonekana kuwa ndiyo ufumbuzi wa tatizo au kuendelea kuiacha hali ilivyo kwa kisingizio cha kusubiri maamuzi ya Kamati ya Shellukindo. Ni vyema Serikali ikafanya uchambuzi wa kina wa kiuchumi ili kupata *right figure or percentage* kwa tatizo hili.

Kwa vile Tanzania imepata mwelekeo ambapo huenda tukafanikiwa kuwa na mafuta lakini kilichojitoleza ni mvutano kati ya Serikali zetu mbili wa namna zitakavyofaidika na raslimali hiyo endapo itapatikana. Lakini msingi wa tatizo hili umeanzia katika upatikanaji wa gesi ambayo imeshafika Dar es Salaam na SMZ haijui chochote kuhusu Mradi huo. Hivyo ndiyo sababu SMZ imetaka kujua ni vipi itafaidika na Mradi huo iwapo utakuwa na mafanikio. Hivyo, siyo vyema kwa Serikali kujificha kwenye vivuli vya kisingizio na badala yake Serikali zetu mbili zikae pamoja na kujadili ufumbuzi na ufanisi wa miradi hii muhimu kwa Taifa.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kuwapongeza Mawaziri wote wawili, kwa namna walivyowasilisha hotuba zao.

Kutokana na Hotuba ya Waziri wa Fedha, ukurasa wa 39, namnukuu: “Bajeti imeendelea kutenga asilimia 4.5 ya mapato yatokanayo na misaada (*grants*) isiyo ya miradi kwa ajili ya bajeti ya Serikali ya SMZ. Utaratibu huu utaendelea hadi hapo mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha (*Joint Finance Commission*), yatakapopatikana.” Mwisho wa kunukuu. Ninapenda kuifahamisha Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni Serikali yenu ya CCM na kwamba, iko katika hali mbaya sana kifedha kiasi kwamba, hata mishahara ya wafanyakazi wake inapatikana kwa tabu sana na haipatikani kwa wakati unaotakiwa. Kwa hiyo, hiyo Tume ambayo mnaisubiri, iharakisheni ili muweze kuwasaidia na wao katika misaada hii zaidi.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine ambayo napenda nitoe dukuduku langu ni pale Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliposema kwamba: “Kutokana na ongezeko la matukio ya ujambazi nchini, maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka ujao (2005) na vitendo vingine vya uhalifu, Bajeti ya mwaka 2004/2005 imeongeza mgao wa fedha kwa vyombo vya Ulinzi na Usalama.” Siku zote kitu kizuri hakichanganywi na kitu kibaya na kitu kizuri ukikichanganya na kitu kibaya nacho huwa kibaya na ndiyo maana wahenga wakasema Lila na Fila hazitengamani. Kwa nini nimesema hivyo? Haiwezekani kuwa fedha za majambazi na wahalifu zichanganywe na uchaguzi hata siku moja, uchaguzi ni kitu cha kawaida na hata yakitokea matatizo yanakuwa ya kiuchaguzi au tuseme safari hii makosa ya uchaguzi yatahusishwa sawa na ujambazi na uhalifu?



Ninapendekeza uchaguzi uwe huru na wa haki na kwa kuviongezea vyombo vya Ulinzi na Usalama fedha ni dhahiri kuwa uchaguzi huo Serikali itauangalia sana kwani uchaguzi wa nchi hii sehemu kubwa unakosa kuwa huru na wa haki kwa kuingiliwa na vyombo hivi vya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kuna mambo mengi sana ya kuchangia lakini kwa kuwa wachangiaji tuko wengi, mimi naomba nipatiwe majibu kwa hayo machache tu maana hata haya machache huenda nisipate majibu.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kidogo katika hoja hizi mbili za Waziri wa Fedha na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji. Kwanza, niwapongeze Mawaziri wote wawili, pamoja na Wataalam wao kwa bajeti zao walizozia ndaa vizuri, ingawa kuandaa ni jambo lingine na utekelezaji ni jambo lingine.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kuanzisha Benki ya Wakulima, kwanza nalipongeze suala hili kama litafanikiwa kuanza.

Mheshimiwa Spika, kama utakumbuka ndani ya Bunge lako ulizuka mjadala mkali kuhusu suala la *NMB* isiuzwe bali igeuzwe iwe Benki ya Wakulima. Sababu zilizotolewa ni kuwa Benki hiyo iko mpaka vijijini. Lakini suala hilo lilipingwa, leo hii Serikali inakuja na hoja ya kuanzisha Benki ya Wakulima. Ni kwa nini tulikataa wazo hilo wakati tunajua kuanzisha Benki itatugharimu pesa nyingi na sidhani kama Benki hizo zitafika kwa walengwa vijijini? Pamoja na kuanzisha Benki hizo, Wizara imetenga Shilingi ngapi kwa ajili ya kuanzisha Benki hiyo ya Wakulima na majengo gani yatatumika hasa kule vijijini ambako ndiko waliko hao wakulima wadogo wadogo ambao wanahitaji huduma hiyo ili waweze kujikwamua kwenye lindi hili la umaskini? Pia ningependa nielezwe kuhusu riba itakuwa ni kiasi gani?

Suala la pili, ni kuhusu zao la biashara. Ningependa kujua ni mikoa mingapi na wilaya ngapi ambazo zimeshachagua zao la biashara na chakula na ni Shilingi ngapi zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo? Tatu, ni lini Tanzania itaanza rasmi kilimo cha umwagiliaji maji mashambani?

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la rushwa ni tatizo ambalo lipo katika nchi yetu na kama hatutakuwa tayari kulifanyia kazi au kupokea mawazo ya Wabunge na Watanzania na yafanyiwe kazi, rushwa itaendelea kuwepo. Hatuwezi kusema rushwa imepungua wakati kuna vilio vya Viongozi wa Dini, Watanzania wote wanalia juu ya rushwa. Tufanyie kazi suala hili ili nchi yetu iwe mfano katika nchi nyingine za Afrika na dunia nzima.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. BUJIKU K.P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, natoa pole kwa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na baba yao mpenzi. Mwenyezi Mungi aipe roho ya marehemu pumziko la milele, *amin*.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Waziri wa Fedha, Manaibu Waziri wote wawili na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, kwa kazi nzuri mliyoifanya kwa kipindi cha fedha kinachomalizika na kwa hotuba nzuri na inatoa matumaini ya maendeleo kiuchumi na teknolojia ya nchi yetu ya mwaka 2004/2005. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, hotuba inapokelewa vizuri sana katika Jimbo langu kwa niaba yao. Pokeeni pongezi na shukrani zao.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie fursa hii, kuwapa moyo wa kutokukatishwa tamaa na michango ya kiupinzani ya baadhi ya wachangiaji. Binadamu na nafsi yake ni kama ulimwengu mdogo, haiwezekani jambo moja hata likiwa zuri namna gani likaridhisha wote. Mheshimiwa Waziri na Wizara yake wanaendelea kutumia michango mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge kama fursa nzuri ya kuboresha zaidi bajeti za miaka ijayo kila wakati uwezo, utamaduni na mazingira ya Taifa yatakapokuwa yanaruhusu.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa MEM unafanikiwa sana kutokana na ushirikiano mzuri kati ya Wizara ya Elimu na Utamaduni na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ni muhimu zaidi Wizara ya Fedha nayo ikashirikiana. Uzoefu huu uendelee kutumika na kuboreshwa kwa ufanisi wa mipango ya usoni kwa ajili ya maendeleo ya watu na wananchi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, ninawatakia kila la kheri watumishi wote wa Wizara ya Fedha na wadau wote wa bajeti hii ili mafanikio yanayotarajiwa yaweze kufikiwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, pamoja na kuwatakia wote maisha mema ni vyema tukawatakia maisha marefu hata wale wasiotutakia mema nao waishi maisha marefu ili kupitia Bajeti kama hizi waendeleo kushuhudia mafanikio yetu.

**MHE. ALLY A. KARAVINA:** Mheshimiwa Spika, ninaanza kwa kuwapongeza Mawaziri wote wawili, Waziri wa Fedha na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, kwa kazi nzuri waliyoifanya pamoja na Wasaidizi wao kwa jitihada zao za kuleta bajeti inayoaanza ku-*address* matatizo ya sekta kiongozi na wananchi walio wengi nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo, ushauri wangi ni kwamba, ili kutoa sura ya kilimo cha wananchi walio wengi na kwa maana ya kuondoa umaskini wa njaa, ambalo ndiyo tatizo la msingi la umaskini wote, inabidi bei ya pembejeo na hasa mbolea iwe chini sana na isiruhusiwe kupanda kwa muda mrefu ili kila mtu alime chakula na kuzalisha ziada. Asilimia 40 ya wakulima wa Jimbo langu walilima lakini hawakupata

mazao kwa sababu hawakutumia mbolea. Bei ya mbolea ikilindwa kutokana na *monopoly profits* za *cartels* za wauza mbolea nchini, wananchi watafaidika na bei nafuu hata kabla ya ruzuku ya Serikali (ambayo si muhimu tu bali ni lazima kama tunataka kuondoa umaskini).

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, bei ya *Ammonia* leo hii 18 Juni, 2004 ni Sh. 7,000/= kwa mfuko wa kilo 50. Kuubeba kutoka Bandari ya Dar es Salaam kutaongeza gharama kufikia kati ya Sh.9,000/= mpaka Sh.9,500/=, ajabu ambayo haieleweki kunatokea nini kati ya Bandari ya Dar es Salaam na maduka ya mbolea Mijini, kwani mbolea inapanda bei hadi kufikia Sh. 18,000/= mpaka Sh. 25,000/= kwa mfuko huo huo, zaidi ya asilimia mia moja ya *landed cost*. Hiki ni kitendo ambacho hakieleweki, *profit* za wafanya biashara binafsi ni kubwa sana, zinachangia kiwango kikubwa sana kudumaza kilimo na kuleta njaa nchini. Bila bei ya mbolea kushuka, hali ya bajeti hii haitaonekana ni ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *exchange rate*, nashauri ni lazima sasa *exchange rate to the Dollar is out of hand*. Lazima ishuke ili ku-*conserve our development gains*. Inachangia sasa hivi kwa *capital flight* kwa wananchi wanaotegemea kuuza mazao ya biashara, ni hasara tupu kwa sababu *high exchange rate* inafanya *exports* zote ziwe *cheap* na *imports* zote ziwe ghali.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja. Ninaomba nitoe dukuduku langu kwa machache kati ya mengi ambayo naamini yatafikiriwa katika majumuisho, kama ifuatavyo: Siungi mkono pendekezo la kuongeza ushuru katika vinywaji baridi, kutoka Sh. 37.50/= hadi Sh. 40/=.

Mheshimiwa Spika, vinywaji baridi ni vya kila mmoja.. Watu wazima wanatumia vinywaji baridi, watoto wanatumia vinywaji baridi, wake kwa waume wanatumia vinywaji baridi. Vinywaji baridi hupooza kiu na huburudisha kila mmoja, ni kinywaji cha watu wote. Wakulima wafanyabiashara, wafanyakazi, wavuvi, wafugaji wanakitumia. Waumini wazuri wa madhehebu yote wanatumia vinywaji baridi. Naomba ushuru ubaki kama ulivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, kuongeza ushuru kutatuathiri sisi watu wa Kagera sana, maana sisi hatuna kiwanda. Vinywaji kama soda husafirishwa kutoka Mwanza hadi Bukoba Mjini, Bukoba Vijijini, Muleba, Ngara, Karagwe, Biharamulo na zinauzwa kwa bei ile ile ya Mwanza na Dar es Salaam. Kiwanda kiangaliwe kisizidishiwe mzigo maana tutarudi kuubeba walaji. Wananchi wa vijijini nao waachwe wanywe soda kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, ongezeko la ushuru litaua soko la soda, badala yake litaongeza soko la *juice*. *Juice* zenyewe si za matunda ya kweli wala mazao ya nchi. *Juice* hizo ni mchanganyiko wa madawa ambayo yana ladha ya matunda fulani, lakini ukweli si matunda. Matunda ya kwetu yanaendelea kuoza kwa kukosa soko na viwanda vya kuyasindika. Kuongeza ushuru katika vinywaji baridi kwa njia nyingine kutaumiza

watu wote. Hata mgonjwa anaruhusiwa kunywa soda wakati amekunywa dawa. Vinywaji vikali mgonjwa aliye katika tiba akinywa ni sumu.

Mheshimiwa Spika, nimeandika yote haya ili ikubalike kwako kwamba, ushuru wa vinywaji baridi ubaki kama ulivyo.

Pili, Mheshimiwa Spika, napenda niseme kuhusu mafao ya wastaafu. Naomba wastaafu wanaorudishwa katika *payroll* wasiwekewe mizengwe. Ni wenzetu, wazee wetu, waliotumikia nchi kwa uaminifu nasi ndiyo tuliyoirithi. Naomba masharti yawe mepesi ili waanze kulipwa. Aidha, ninashauri malipo yawe ya miezi mitatu mitatu badala ya miezi sita sita.

Mheshimiwa Spika, tatu na mwisho kwa hoja hii, napenda kujua Serikali inasimamia vipi suala zima la pensheni za wale waliofanya kazi kwenye Mashirika ya Umma (*PPF*). Wakati wenzao wanashughulikiwa na wanarekebishiwa mafao yao, wale wa *PPF* wamebaki pale pale. Nashauri hili liangaliwe, iwapo *PPF* haiwezi kuwarekebisha, Wizara ya Fedha ione uwezekano wa kubeba mzigu huo. Lengo ni kuona kuwa wastaafu wetu wote wanaangaliwa kwa karibu katika msingi wa kuthamini mchango wao na kuwapa moyo wale walio kazini ili wajenge matumaini ya baadaye kwa kuchapa kazi kujenga Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, narudia kusema kwamba, naunga mkono hoja.

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kuchangia japo kwa maandishi hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuhusu Bajeti ya 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, hotuba ni nzuri, dhamira ya Serikali kuondoa umaskini ni nzuri, ila watekelezaji na wasimamizi wa dhamira hii nzuri ya Serikali hawatekelezi ipasavyo wala Hawasimamii ipasavyo. Baada ya agizo hili la Serikali kupitia hotuba ya Bajeti ya Waziri husika, wanadai haraka sana wapelekewe kanuni na mwongozo wa kuwawezesha utekelezaji wa haraka.

Mheshimiwa Spika, agizo la Serikali kupitia kinywa cha Waziri wa Fedha na Waziri Mkuu kwa Bajeti ya mwaka jana 2003/2004, imekuwa ni pigo kuu kwa ushuru/kodi zinazotowza kwenye masoko au magulio ya Mwika, Marangu Mtoni na Soko la Himo kiasi kwamba wananchi wanajiuliza; ni serikali gani hii au ni kwa vile Jimbo hili la Vunjo Mbunge wao ni wa Upinzani wa *TLP*?

Mheshimiwa Spika, agizo la Waziri wa Fedha na Waziri Mkuu linasema watakaotowza ushuru ni wale wote wanaonunua bidhaa kwa wingi kama vile mikungu ya ndizi, magunia mengi ya mahindi na nafaka kwa madhumuni ya kwenda kuuza nje ya eneo hilo kwa lengo la biashara ya kupata faida kubwa. Hali kadhalika kwa wale wanaoleta mazao hayo kwa wingi kuuzia sokoni hapo, watozwe ushuru. Hii ni vizuri.

Mheshimiwa Spika, agizo la Mawaziri hawa ni kwamba anayetandaza biashara yake hapo chini Asubuhi na kuanua jioni asitozwe chochote.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mara baada ya hotuba za Bajeti 2003/2004 hadi leo hii, ushuru unatozwa vibaya mno.

Kuanzia yule anayenunua kwa wingi au kuuza kwa wingi (in bulks) hadi yule bibi kizee kinachouza ugoro kwa kijiko cha chai. Aliyeleta nyanya au mchicha kwa kikapu na kuzipanga hapo chini kwa vifungu angalau apate Shilingi kumi za kununua kibiriti, pishi ya mafuta ya taa au ya kupikia, lazima atozwe ushuru wa shilingi mia moja na kulazimishiwa risiti au mtoza ushuru akifuatana na Mwanamgambo nyuma yake hadi anachukua mafungu mawili au zaidi na kumwambia kama anataka kuyakomboa aende Ofisi ya Kata akiwa na ushuru huo baada ya muda wa soko kumalizika:

- (a) Wauza mitumba, dengirizi, viatu, khanga wamachinga, maandazi, vitumbua, pipi, mafuta ya alizeti, maziwa mtindi.
- (b) Makibengia wa samaki, nyanya, vitunguu, karoti, pilipili hoho, kabeji, magadi, mizigo ya majani ya ng'ombe, kunde zote.
- (c) Zana za wahunzi kama vile majembe, rato, mundu, n.k.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufunga Bunge la Bajeti 2003/2004, maagizo ya Waziri wa Fedha na Waziri Mkuu yalikuwa kwamba Waheshimiwa Wabunge waende kwenye maeneo yao waelimishe na waelekeze walengwa ni kipi kitozwe kodi na kipi kisitozwe kodi. Matokeo yake Mkurugenzi, Mwenyekiti wa Kanseli na Afisa Masoko Wilaya ya Moshi walienda kwa Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya kuwaeleza kuwa Mbunge wa Vunjo Mheshimiwa Major J.J. Makundi amewakataza watu wote wasilipe ushuru. Mkuu wa Mkoa alimwita Mheshimiwa Makundi kwenye Kamati ya Nidhamu ya Mkoa akadhamiria kumwambia *RPC* ampeleke mahabusu gereza la Karanga Moshi na badala yake alimwamuru *RPC* ampe Polisi wengi tu, ili Mheshimiwa Mbunge apite kila soko na kuwatangazia kuwa ushauri unaendelea kama kawaida kwa kuwa Serikali haijaleta fedha za fidia kwenye Kanseli na robo robo hii inayoletwa haitoshi kuendesha Kanseli ya Moshi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa urudishaji wa ushuru katika masoko ya Mwika, Himo na Marangu Mtoni chini ya Polisi wakiwa na Sare na bunduki kwa agizo la Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro; wananchi wanalia machozi ya maji kila siku ya soko kwa kunyanyaswa na Watoza Ushuru wakiambatana na Wanamgambo. Hakuna kinachobaki bila kutozwa ushuru. Tembelea mwenyewe kwa kushtukiza; na kila mwenye mapenzi mema na Serikali hii chini ya CCM atembelee masoko haya ayashuhudie hayo yanayowakatisha tamaa ya kuona kwamba Serikali hii inatenda visivyo.

Mheshimiwa Spika, leseni mbalimbali zimeondolewa kwenye Bajeti hii ya 2004/2005. Halmashauri kwa mtazamo wao wataona wamenyimwa njia nyingine ya kukusanya mapato ya Halmashauri. Ninamhakikishia Waziri wa Fedha kuwa

Halmashauri itatekeleza kinyume cha maagizo kama walivyopuuza amri ya utozaji wa ushuru masokoni na kujitengenezea *By Laws* kama ngao ya kujilinda agizo halali la Serikali.

Mheshimiwa Spika, ninamtakia Waziri wa Fedha mwisho mwema kwa manufaa ya Watanzania wote.

**MHE. PETER KABISA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Fais, Mipango na Ubinafsishaji na Mheshimiwa Basil Mramba, Waziri wa Fedha kwa mwaka huu wa fedha 2004/2005. Ni Bajeti safi kabisa na naiunga mkono kwa asilimia mia moja.

Lakini Mheshimiwa Spika, naomba kwa niaba ya wapiga kura wangu wa Kinondoni na mimi mwenyewe kuwapa pole familia ya Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda kwa kufiwa na baba yao mzazi. Mwenyezi Mungu ailaze pema roho ya marehemu peponi. Amina.

Pia Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Ndugu Danhi Makanga, kwa ushindi wake katika Jimbo la Bariadi hivi majuzi. Namtakia kazi njema humu Bungeni na Jimboni kwake Bariadi.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niwapongeze Mawaziri wote wawili, Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu, Manaibu Katibu Wakuu na Viongozi wao wote wa Mipango na Hazina na vile vile vijana wetu wa *TRA* kwa kazi nzuri wanayoifanya hasa kwa hii miaka miwili mfululizo. Hongera sana. Ni utendaji na usimamiaji mzuri.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru Serikali kwa uamuzi wake wa busara na hekima wa kuwafikiria tena wastaafu wake waliochukua *pension* zao kwa mkupuo na sasa kukubali kuwapa *pension* ya kila mwezi kuanzia Januari, 2005. Ni kweli hawa wa mpango wa mkupuo walikwisha malizana na Serikali. Lakini Mungu ameendelea kuwaweka kwa maisha marefu. Serikali imeliona hilo na sasa kuamua kulirekebisha.

Mheshimiwa Spika, kuna misemo ya Kiingereza isemayo: "*Something is better than nothing*". Yaani hawa wastaafu washukuru baada ya kumaliza "mkupuo" wao sasa Serikali imeamua kuwapa chochote, mpaka watakapoaga dunia. Fedha hizo watakapopewa 25,000/= ni ndogo sana kwa sababu ziko chini ya kima cha chini. Na huko sokoni fedha hazitatasha kwani hakuna soko la bei nafuu kwa wazee. Pia kumbuka huko mitaani wataendelea kununua vitu hivyo kulipa *interest tax* kama yule anayepata mshahara wa kima cha chini. Labda ndiyo usemi wa pili wa Kiingereza usemao: "*beggars can't be choosers*".

Mheshimiwa Spika, naomba kwa hekima na busara zile zile zilizowawezesha Serikali kuwarudishia hawa wastaafu *pension*, basi wafikirie kwamba katika ulimwengu wa sasa basi huyu mstaafu alipwe angalau kima cha chini cha mshahara wa chini Serikalini - mshahara wa sasa; na hii *pension* iwe inakuwa "*indexed*" *yearly* kwa kufuata

hali halisi ya maisha. Lakini niseme naishukuru Serikali kwa uamuzi huu kutupa wastaafu wa mkupuo wa awali, *pension* ya kila mwezi kuanzia sasa.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mramba, atakapokuwa anafanya majumuisho yake atusaidie tulio wengi kutoa ufafanuzi wa aya ya (30) kifungu (vi) ukurasa 24 wa hotuba yake kuhusu: “Kusimamia utekelezaji wa sera ya mikopo midogo midogo (*microfinance*) na mpango wa dhamana kwa wawekezaji Wadogo wadogo ili kuwezesha wananchi walio wengi kujiendeleza kiuchumi (biashara pia kujiajiri) kwa kujipatia mikopo zaidi kibenki”.

Mheshimiwa Spika, hawa wanaotajwa kwenye aya hii ni akina nani? Kwa sababu unapozungumzia “dhamana” tayari unamtambua mtu mwenye uwezo fulani kwa mfano ana nyumba yenye hati miliki au tayari ana biashara inayotambulika, hivyo kuwa na dhamana.

Lakini Mheshimiwa Spika, kwa Mkoa kama Dar es Salaam au niseme Jiji la Dar es Salaam - walengwa tunaowaombea mikopo na ajira ni wapangaji wa vyumba au chumba, ni walalahoi, ni wanavijiweni, na “*drop outs*” au vijana waliomaliza Darasa la VII au *Form IV* au *Form VI* hata Vyuo vya Ufundi au Chuo Kikuu. Hawa wote hawana uwezo kuwa na dhamana. Sasa nani mdhamini wao? Na hawa ndio wanaomba mikopo midogo midogo kutoka Wizara ya Kazi, Vijana na Michezo; Wizara ya Jamii, Jinsia na Watoto au kutoka Manispaa/Halmashauri zetu. Lakini kwa maana ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, hii aya inamlenga na inamsaidia nani? Kwa sababu tatizo la ajira ni zito mno. Lazima Serikali iliangelie hili kwa makini sana. Naomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, nimefurahishwa sana na uamuzi wa Serikali kumwondolea Bwana Mkuu wa Uti wa Uchumi wetu - Bwana na Bi Mkulima kodi za pembejeo., mbolea, trekta, na kadhalika, ili iwe kichocheo cha kulima zaidi.

Lakini Mheshimiwa Spika, Serikali isipoamua kwa makusudi kabisa, kwanza kupeleka vivutio huko vijijini ili vijana wetu wapende kuishi na kufanya kazi huko na pili kupeleka watu wabunifu au mawakala, waende na *tractors etc.*, za kuwakodishia wakulima hao ili badala ya kulipa *acre 1* walime *acres 20*; basi kilimo duni cha *1/2, 1 or 2 acres* kitashamiri, na *for another 45 years* tutakuwa pale pale.

Mheshimiwa Spika, kuna haja kabisa ya kufikiria “*big*” na kumwezesha huyu mkulima akodishe *tractor*, mbolea, Pembejeo, halafu apewe *1 or 2 years grant*; mwaka unaofuata anze kulipia deni lake. Hii itamfanya afanye kazi yake na vijana wake kwa ufanisi, bidii na kupenda “utajiri” atakaoanza kupata na kwa maana hiyo Taifa litaondokana na kilimo tegemezi au mazo tegemezi kwa maana ya kuagiza chakula nje.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine nasema hii Bajeti ni ya mwananchi wa kawaida na lazima ajifurahishe, binadamu hajakamilika. Lakini kwa kweli nawapongeza sana Serikali, Mawaziri wote na wote walishiriki, kutengeneza Bajeti hii. Naunga mkono mia kwa mia. Ahsante.

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie hotuba ya Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji na Wizara ya Fedha kwa pamoja kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, tafadhali niruhusu nitoe pongezi kwa Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji, Mheshimiwa Abdallah Omari Kigoda (Mb.), kwa hotuba nzuri aliyotoa tarehe 10/6/2004 juu ya mipango ya nchi yetu kiuchumi na kijamii kwa mwaka wa fedha 2004/2005. Pia nampongeza sana Katibu Mkuu wa Wizara pamoja na viongozi na wataalam wote wa Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji kwa kazi kubwa waliyoifanya kwa kutayarisha hotuna na mpango huu.

Pia Mheshimiwa Spika, naomba kwa unyenyekevu mkubwa nimpe pole Mheshimiwa Waziri Kigoda (Mb.) kwa msiba aliopata kwa kufiwa na baba yake. Nampa pole sana.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze kwa dhati Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba (Mb.) kwa hotuba yake nzuri ya Bajeti ya mwaka 2004/2005. Pamoja na Mheshimiwa Mramba (Mb.), nawapongeza Manaibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu (Mb.) na Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatibu (Mb.) - kwa hotuba hii yenye kina na mapana ya Bajeti hii iliyo mbele yetu kama hoja. Pamoja na viongozi hawa, nawapongeza sana Makatibu Wakuu wote, Manaibu Katibu Wakuu wote, viongozi wengine Makamishna wote, Wataalam na Watumishi wote kwa ujumla wa Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, Bajeti yetu ya mwaka 2004/2005 inatupatia mategemeo ya kukusanya asilimia 13.8 ya pato la Taifa na inatuweka tegemezi kwa asilimia 41. Ukilinganisha na mwaka jana 2003/2004, tumepiga hatua mbele kwa asilimia 20. Hii ni hatua nzuri na ninaipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Spika, Bajeti yetu ya 2004.2005 inaonyesha pesa nyingi zitapatikana na tungeweza kupunguza utegemezi hadi kufikia asilimia 34 dkama tangedhibiti matumizi vizuri zaidi. Eneo hili namwomba Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango usimamizi imara.

Mheshimiwa Spika, kwenye Bajeti ya mwaka 2003/2004, tulipewa ahadi kwamba ununuzi wa magari yenye thamani kubwa kama vile *Ma-landcruiser "VX"*, *Nissan Super* na kadhalika yaachwe kununuziwa. Machache yatakayonunuziwa yaishie kwa ngazi ya Waziri tu kuanzia juu - yaani wachache na wenye kuteuliwa. Lakini mpango huu inaonekana hausimamiwi vizuri. Kuna tatizo gani? Mpango wa kupunguza magari kwenye Wizara zote na vituo vya Serikali utekelezwe kupitia kwenye mfumo wa kuwakopesha magari watumishi wanaostahili gari. Kwani mpaka kufikia wakati huu, mpango ungekuwa umeanza kuonyesha mafanikio.

Mhe Spika, hapa naomba niipongeze TRA jinsi inavyopunguza gharama ya magari. Watumishi wanaostahili magari wamekopeshwa magari na wanayatumia.



Magari kwa matumizi ya Ofisi wananunua machache na ya gharama ya chini, lakini yanafaa sana kwa kazi yao - yaani aina ya *Nissan Station Wagon Standard* na *Landrover*. Na baada ya saa za kazi unayakuta yameegeshwa ofisini isipokuwa yale yaliyo kwenye zamu. Mtindo huu usukumwe kwenye Serikali yote na Tume zingine za Serikali.

Mheshimiwa Spika, eneo jingine ambalo tunaweza kupunguza matumizi ni jinsi tutakavyoziweka Ofisi zetu. Tununue samani (*furniture*) za bei nafuu na za kukidhi haja tu na si Vinginevyo. Ona mfano wa Ofisi za Balozi mbalimbali nchini hapa - k.m. Japan, India, Italy, *European Union* na kadhalika. Kikubwa kinachoonekana ni vitendea kazi bora, usafi zaidi. Zina samani (*furniture*) za bei nafuu na za kukidhi haja tu.

Mheshimiwa Spika, maeneo ni mengi ambayo matumizi yanaweza kupunguzwa ikiwa ni pamoja na safari zisizo za lazima, kupunguza semina na warsha na kadhalika. Ikiwezekana kuliondoa kabisa tatizo la Ofisa kusafiri kwa ndege na gari nayo anaiagiza imfuate aliko.

Mheshimiwa Spika, kodi ya *Hotel Levy* inayotozwa kwenye *Guest Houses* nchini si ya kimaendeleo (*Disincentive Tax*). Sheria inasema mwenye nyumba ya wageni (*Guest House/Hotel*) alipe asilimia 20 (20%) ya mauzo yake kwa mwezi kama kodi ya *Hotel Levy*. Utaratibu huu hauzungumzii matumizi kabisa. Kodi hii ukiilinganisha na Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) inayoagiza kukusanya asilimia 20 (20%) ya bei ya bidhaa au huduma kutoka kwa mteja atakayenunua bidhaa hiyo.

Mheshimiwa Spika, kodi hii ni kubwa mno. Asilimia 20 (20%) ya mauzo (*gross sales*) ni kama kusema unataka kumwondoa kabisa mwenye *Guest House or Hotel* kwenye biashara.

Mheshimiwa Spika, kama sheria ilivyo nashauri kiwango kiwe asilimia mbili au mbili na nusu ya mauzo. Tafadhali ichunguze kodi hii na sheria yake angalia inavyoagiza na bila shaka utakubaliana na mapendekezo yangu ili kuwaweka wafanya biashara hawa katika hali ya kulipa kodi hii. Halmashauri nyingi nchini zilipendekeza kodi hii ifutwe kwani zinapata taabu sana kuikusanya.

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Wizara ya Fedha kwenye juhudi zake za kudhibiti kodi kwenye bidhaa ya mafuta ya *petroli (petroleum products)*. Mpango wa kuweka *flow meters*, kuanzia mwaka huu ni mzuri.

Pia juhudi za kuweka vyombo vya usafiri majini (*speed boats*) kwenye Bahari ya Hindi na Ziwa Victoria nazipongeza sana, ni nzuri. Wasiwasi wangu uko kwenye wale ambao ni wapiga magendo hasa hasa (*smugglers*).

Mheshimiwa Spika, kwenye maeneo ya mipakani ambako ndiko wanapitisha magendo haya kwa kutumia magari ya *tanks*, kwa kutumia njia za panya; na kwa kutumia mitumbwi na kaluwa.

Hawa watu wametusumbua kwa muda mrefu sana. Kawaida ya watu hawa wanakuwa na ushirikiano na maofisa wetu wa kodi na dola. Naiomba Wizara inipatie maelezo ya kuridhisha na kunitoa wasiwasi kwamba itapambanaje na hali hii?

Mheshimiwa Spika, Bajeti yetu ya 2004/2005 imesisitiza sana namna ya kuwawezesha wenye biashara ndogo wakulima na wenye biashara za kati kwamba watafaidika kutoka kwenye vyombo mbalimbali vya fedha kwa kutumia fursa ya dhamana ya mikopo (*Credit Guarantee System*). Maelezo juu ya utaratibu huu hayajawa wazi na pia utaratibu wenyewe haujawa wazi.

Kwenye maelezo ya Waziri juu ya fursa hii nilitegemea Waziri atoa mifano ya namna unavyokwenda sasa. Maana mpango huu umeanza 2003/2004.

Pia tuelewe wazi kwa watu wa vijijini watafanyaje ili kupata fursa hii kwa mfano jamii ya wafugaji wa Kimasai au wakulima wa jamii ya Kisukuma kwenye maeneo ya Ng'wana mashimba na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara kwanza initoe hofu juu ya mpango huu kwa kueleza mwaka 2003/2004 umetekelezwaje kwenye mikoa, Wilaya, vijini na watu waliofaidika na mpango huu wa mikopo. Maelezo yalenge kwenye maeneo ambayo yatarahisha taratibu mgumu na masharti ya vyombo vya fedha kwenye kutoa mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba nipate maelezo kwenye mambo ambayo nimehoji kwenye maelezo yangu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja zote mbili.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, kwanza naungana na Wabunge wengi waliounga mkono Bajeti ya 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza *TRA* kwa kazi nzuri ya kukusanya mapato ya Serikali. Mapato yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka. Hii inaonekana kwamba uchumi wetu unakua. Pamoja na mapato kukua, kodi za wananchi zimeondolewa na kuwapunguzia mzigo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia baadhi ya miradi ambayo inafanywa na Serikali. Kuhusu suala la elimu, ni mradi mmojawapo wa kujivunia sana. MEM imekuwa ukombozi wa Watanzania wote Mijini na vijijini. Madarasa yameongezeka na shule mpya zimejengwa. Baada ya kuongezeka kwa uandikishaji, sasa Serikali inasaidia ujenzi wa sekondari - jambo ambalo litaongeza wanafunzi wengi kwenda Sekondari na kukua kwa elimu nchi nzima.

Jambo ya mawasiliano na miundombinu ni muhimu sana katika kuinua uchumi. Bila barabara, hata kilimo ni kazi bure. Napenda kuzungumzia ujenzi wa barabara inayojengwa toka Rombo hadi Kamwanga. Barabara hii inajengwa kwa kiwango cha

lami. Lakini barabara ikiishia Kamwanga, haina maana kama kuanzia Kamwanga kwenda Sanya Juu ni barabara ya moramu. Kwa nini isiunganishwe ili wakulima wote wafaidike na barabara hiyo inayozunguka Mlima Kilimanjaro?

Kisiasa barabara hii itaonyesha kugawa wananchi na wengine kuona wao hawajatendewa haki kwani barabara hiyo ni moja. Haifai kutengeneza eneo moja na kuacha eneo lingine. Barabara hiyo ni muhimu kwani inaunganisha Mkoa wa Kilimanjaro na Mkoa wa Arusha kuzunguka Mlima Kilimanjaro.

Pili, barabara hiyo inaunganisha Wilaya tatu - Wilaya ya Rombo, Wilaya ya Monduli na Wilaya ya Hai, Jimbo la Siha.

Mheshimiwa Spika, napendekeza barabara hiyo iunganishwe toka Rombo - Kamwanga Lerangwa, Ngarenairobi, mpaka kuunganika na Lami Sanya Juu. Barabara ya lami isipounganishwa, itabidi kiraka - ambacho hakina lami na kusababisha eneo ambalo halina lami kuharibika mara kwa mara.

Naomba kwa heshima na taadhima barabara hii iunganishwe, kwani barabara ya lami inatoka Hai kupitia Sanya Juu. Nyingine itatoka Rombo na kuishia Kamwanga. Kipande kitakachobaki ni ya moramu, sasa iunganishwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hizi, ahsante sana.

**MHE. AZIZA SLEYUM ALLY:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja zilizo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, natoa pole kwa yote yaliyowakuta wenzetu kwa kufiwa na kupata ajali.

Mheshimiwa Spika, naanza kuchangia katika hotuba hii kuhusu suala la Kiwanda cha Nyuzi Mkoani Tabora. Serikali itufafanulie kwa uwazi kuhusu kiwanda hiki ambacho kinaturudisha nyuma kimaendeleo ya vijana kukosa ajira. Naomba sana Mheshimiwa Waziri aliangalie hili kwa wakazi wa Tabora.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kilimo cha Tumbaku, tunashukuru mwaka huu wakulima wa tumbaku Mkoa wa Tabora wamefaidika na kilimo hicho, ila tu bei bado haipanda zaidi kwa ukosefu wa Kiwanda cha Tumbaku Mkoani Tabora. Kwani kukosekana kiwanda hicho mkoani hapo ndipo bei ya tumbaku inashuka kwa kuwa wanunuzi husafirisha kupeleka Morogoro, ambako hata kilimo cha tumbaku hawakijui. Je, Waziri hamwoni kuwa hamuwatendei wakulima wa Tabora haki, walime tumbaku na kiwanda kwenda kwa wasiolima tumbaku?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mikopo kwa Wafanya Biashara, nachukua fursa hii kuwapongeza akina mama wa Tabora wanaojishughulisha na biashara ndogo ndogo, kwani nina imani kwamba wanaendelea kujenga Taifa kuepukana na suala la umaskini. Lakini naomba sana Serikali iwaangalie na kuwasaidia sana kwa ushirikiano wao.

Mheshimiwa Spika, akina mama na akina baba wengi wanaendelea na mikopo ya *Pride Tanzania*. Kwa hiyo, cha muhimu ni kwamba Serikali iwape moyo na *Pride* kuwakopesha *Pride*, na *Pride* kusimamia mikopo hiyo kwa wananchi ambao wameuweka utaratibu ambao wao wenyewe wanasimamia kwa kulipa deni hilo. Naipongeza sana *Pride* kwa kazi nzuri waifanyayo kwa kuwakomboa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Bajeti imekidhi haja za wananchi kwa kiwango kikubwa sana hasa wananchi wa chini kabisa pamoja na kuwa ni Bajeti yetu ni tegemezi. Lakini nina imani Bajeti hii kila mmoja ameifurahia sana. Mimi sina budi kuunga mkono Bajeti mia kwa mia.

**MHE. DK. THADEUS M. LUOGA:** Mheshimiwa Spika, hotuba zote mbili zimechambua kwa kina sana mambo yote muhimu ya maendeleo ya uchumi wetu pamoja na mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka 2003/2004 na mpango wa maendeleo wa mwaka 2004/2005. Naomba nichukue nafasi hii ya kuwapongeza Mawaziri wote wawili na Wasaidizi wao wote kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi kuanzia Julai, 2003 hadi Aprili, 2004 Serikali imefanikiwa kuvuka malengo kwa kukusanya mapato ya Serikali kwa kodi ya *VAT*, kodi ya mapato na ushuru wa forodha. Natumia nafasi hii ya kuipongeza sana *TRA* kwa mafanikio hayo. Hapo hapo inasikitisha kwa kipindi hicho hicho makusanyo ya mapato yasiyo ya kodi yanayokusanywa na Wizara, Idara mbalimbali pamoja na Mikoa yalikuwa chini ya malengo. Hii si dalili nzuri, inatakiwa ichunguzwe kwa kina ili sababu zifahamike kwa nini wamekusanya chini ya malengo. Inawezekana upo ubadhirifu wa mapato katika sehemu hizo zinazofanywa na wafanyakazi wa Wizara, Idara na Mikoa.

Mheshimiwa Spika, ni kweli jitihada inayofanywa na Serikali ya kupambana na Bajeti tegemezi kwa kuongeza mapato ya ndani inasaidia, lakini kwa kiwango kidogo. Kwa mfano mwaka 2002, pengo la Bajeti lilikuwa asilimia 47 na lilifidiwa na misaada au mikopo ya kutoka nje; na mwaka 2004 pengo limeshuka hadi asilimia 41. Sababu mojawapo ya kuwa na Bajeti tegemezi ni kuendelea kuwepo wananchi asilimia 80 wanaoishi vijijini na Mijini ambao ni maskini wa kipato, hivyo hawana uwezo wa kuchangia mapato ya Serikali. Kwa hivi Serikali ifanye jitihada kubwa ya kuwawezesha hao ili wapate uwezo wa kuchangia mapato ya Serikali yao. Bila ya kufanya hilo, upanuzi wa uwigo wa walipa kodi hautafanikiwa na hali ya Bajeti tegemezi haitakwisha haraka, bali itaendelea kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, upo mgongano wa matumizi ya maji kati ya shughuli za kilimo na uzalishaji wa umeme. Jambo linalofahamika wazi kuwa umeme unaweza kuzalishwa bila ya kutumia maji kama kwa kutumia mkaa wa mawe, gesi na njia nyingine kadha wa kadha. Lakini huwezi kuzalisha mazao ya kilimo bila maji, kwa hivi tunaweza kusema kuwa bila maji hakuna kilimo. Kwa hali hii naishauri Serikali ifanye hima kumaliza mgogoro huu wa matumizi ya maji kati ya kilimo na umeme. Maji yote hapa nchini yatumike kwa kilimo, viwanda, mifugo na kwa matumizi mengineyo. Hivyo, umeme uzalishwe kwa kutumia njia nyingine kama makaa ya mawe ya Mchuchuma,

gesi, jua, upepo na hata mafuta ya petroli. Hatua kama hizi zitasaidia sana uchumi wetu kukua kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa maamuzi ya kuwarudisha wastaafu kwenye orodha ya pensheni na hatua ya kuweka mita itakayosaidia kudhibiti ukwepaji wa kodi katika biashara ya mafuta ya petroli.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mbinga Magharibi na mimi mwenyewe, naunga mkono hotuba zote mbili mia kwa mia.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji na Waziri wa Fedha kwa kazi nzuri, na pole kwa majukumu mazito ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, imetokea nini katika Wizara ya Kilimo kuwa ipo nyuma kiutaratibu wa kuinua pato letu la Taifa? Mbona njaa ipo pale pale? Mbona hakuna msisitizo wa mtiririko wa jinsi ya kujiandaa kupambana na janga la njaa? Mbona hii Wizara ni moja ya *priority sector*? Zingine zimefanya vema e.g. Elimu, Barabara, Maji na Afya. Yenyewe Wizara ya Kilimo imerudisha nyuma maendeleo ya kilimo nchini!

Mheshimiwa Spika, imekuwaje katika kutoa *royalty* (mrahaba), Bajeti imejielekeza kwenye baadhi ya madini tu na kuacha madini ya dhahabu, almasi na *Tanzanite*? Inasikitisha Bajeti hii kubagua. Halmashauri zisipewe hizo pesa. Kwa kweli inabidi mikataba, sheria na kanuni hizo za fedha zitazamwe upya. Inawezekana tufike mahali tunakuwa na imani na Halmashauri zetu. Mbona fedha za Serikali asilimia 75 zinapelekwa kwenye Halmashauri?

Mheshimiwa Spika, kwa nini Mhakikimali wa Serikali hakagui mali ya Halmashauri? Sheria ije kuzitaka Halmashauri za Wilaya zipeleke kukaguliwa mali wao.

**MHE: DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Fedha - Mheshimiwa Mramba, Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji - Mheshimiwa Dr. Kigoda, Makatibu Wakuu, Mhasibu Mkuu wa Serikali pamoja na Watendaji wote walioshiriki katika kuandaa Bajeti hii nzuri iliyo mlenga mwananchi wa kawaida moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, ninawaombea Mungu awape nguvu na uwezo wa kutekeleza kama ilivyoandaliwa kwa maslahi ya Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kutoa mchango wangu, napenda nikiri kwamba naiunga mkono Bajeti kwa asilimia mia moja kwa mia moja.

Mheshimiwa Spika, sasa nianze kuchangia nikianza na ubadhirifu wa fedha za Serikali, ambao umekithiri hapa nchini. Watendaji wa Serikali wamekuwa hodari wa kutengeneza Bajeti za maeneo yao ya kazi, bali matumizi ni mabaya sana. Fedha nyingi

za Serikali zimekuwa zikitumiwa kwenye mambo ambayo siyo ya lazima. Mfano, safari nyingi, kuhamisha kutoka akaunti moja kwenda akaunti nyingine bila taratibu za kisheria, ama kucheza na kalamu - yaani udanganyifu.

Mheshimiwa Spika, viongozi wenye dhamana ya watu wakikemea, Serikali inamtoa Mtendaji huyo kutoka kituo A kwenda kituo B. Hivi ni wananchi wa eneo gani wanaopenda kupelekewa Mtendaji mbovu? Hakuna sababu, warudi kijijini wakalime.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie juu ya kupanda kwa bei ya sementi, bati na gharama ya umeme - ambavyo ni vitu muhimu sana kwa maendeleo ya Watanzania. Wakulima wanakazania kilimo na uzalishaji mali ili wapate fedha za kujenga nyumba bora na za kisasa na zenye umeme. Hivi mwananchi hata akijitahidi kuzalisha mali kiasi cha kutosha kwa bei hizi za juu, nyumba watajenga?

Mheshimiwa Spika, pamoja na sababu zote walizotoa za kupanda kwa bei ya sementi na bati, Serikali iangalie kila uwezekano wa kupunguza bei hizi ili mwananchi wa kawaida aweze kujenga nyumba bora na pia aweze kutumia umeme. Naomba nizungumzie juu ya suala la mishahara ya wafanyakazi. Serikali imekuwa ikitoa mishahara ya juu kwa watumishi wanaofanya kazi kwenye maeneo ya kushika fedha, kwa mfano *TRA* na *TANROADS* na kadhalika kwa lengo la kuwapunguzia tamaa. Hata mimi utaratibu huu naupongeza. Naiomba Serikali iwaangalie Watendaji wanaoshika fedha ambao ni wengi wakiwemo Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini, Hazina na Wahasibu walio chini yao.

Mheshimiwa Spika, nimetaja Watendaji hawa kwa vile sasa wanapokea fedha za miradi mbalimbali ambayo ina mamilioni ya fedha. Ni vigumu sana Watendaji hawa kutawala nafsi wakati vipato vyao ni vidogo. Napenda pia niikumbushe Serikali mazingira magumu anayopata Mwalimu wakati akiwa kazini, nikizingatia kuwa wanafunzi wanaowafundisha wako wenye maradhi ya kuambukiza, mfano *TB*, upele, mafua na kadhalika. Hata kitendea kazi chake kikuu yaani chaki, nacho ni tatizo. Wako walimu waliopata maradhi kutokana na chaki. Hivyo naiomba Serikali iwarudishie Walimu - *Teaching Allowance* ili iweze kuwasaidia katika matatizo wanayopata wakiwa kazini.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kuondoa kodi kwa waagizaji wa pembejeo na mbolea. Pamoja na unafuu huu, bado ninapata wasiwasi kwani wakulima walio wengi hawana uwezo wa kununua Pembejeo. Naitaka Serikali kupanga bei za kulima ili wale wachache wenye uwezo wa kununua pembejeo wasiwapandishie bei wakulima wasio na uwezo wa kununua Pembejeo. Mfano mzuri ni bei za nauli za daladala Dar es Salaam zinafanana kulingana na gharama ya mafuta. Hivyo, kuwe na usimamizi wa karibu juu ya bei za kulimiwa.

Mheshimiwa Spika, naendelea pia kuwakumbusha suala la malipo ya pensheni kufuata wastaafu Dar es Salaam. Hii ni kero. Wapo wastaafu wanaokufa kwa kugongwa na magari huko Dar es Salaam, kukaa huko miezi zaidi ya sita bila mafanikio. Naiomba

Serikali ipeleke huduma hii mikoani ili kuwapunguzia wastaafu gharama na usumbufu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuviweshia vyama vya ushirika. Tatizo litakuwa taaluma, wakulima wetu hawana. Naiomba Serikali kuwawezesha Maafisa Ushirika ili waweze kutoa elimu juu ya ushirika ili vyama hivi viweze kutoa huduma itakayowaletea faida. Vyama vingi zamani vilikufa kwa kuajiriwa watumishi wasio na uwezo.

Mheshimiwa Spika, nimalizie juu ya akina mama kuondokana na umaskini. Ni kweli wanawake sasa anatekeleza kwa vitendo suala zima la kuzalisha mali ili kuinua pato la familia zao. Tatizo ni masoko hakuna. Mfano, wanawake wa Singida wanasuka vikapo - bali soko hakuna. Naiomba Serikali kuviwzesha viwanda vidogo vidogo ili viweze kununua bidhaa hizi na kuuza kwenye masoko ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, narudia tena kuunga mkono Bajeti hii.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu pensheni, ni tofauti zipi kati ya fomula ya *pension* na ile ya *gratuity* kwa mtu anayepokea Shilingi 100,000/= na aliyefanya kazi miezi 60 hivi? Kwa nini wastaafu waliochukua wa mashirika ya umma hawamo katika zoezi la kurudishiwa katika *pension*? Idara ya *pension* inavyoimarisha kwa motisha na zana za kisasa ili wawe na motisha ya kusaidia vizuri wazee.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mabengi, je, tunajua historia ya mabengi haya ya kigeni - kabla hajaanza biashara nchini - *BoT* Kitengo cha *Banking Supervision* kinasaidi waje na nyenzo ili kifanye kazi vizuri?

Mheshimiwa Spika, kuhusu *TRA* Mikoani, wanafanya kazi nzuri. Lakini usalama wao ukoje hasa ukizingatia wafanye biashara wakorofi - wanalindwaje hawa *TRA* Mikoani? Mkoa wa Morogoro, *TRA* wapongezwe. Taarifa ya utendaji wao Julai hadi Septemba, 2003:-

<b>Lengo</b>	<b>Makusanyo</b>	
Mapato	1,678,246,467/00	2,465,227,886/00
<i>VAT</i>	2,136,233,625/00	2,613,662,487/85
<i>Customs</i>	222,400,000/00	30,535,000/00
	<hr/>	<hr/>
	<b>4,036,880,092/00</b>	<b>5,109,425,373/85</b>
	<hr/>	<hr/>

Hii ni juhudi kubwa kwa Mkoa *TRA*. Naomba sana hawa vijana wapongezwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Exchange Rates*, kwa nini tunapenda sana kupima Shilingi yetu na *USD* badala ya sarafu nyingine duniani, ambazo tunafanya nao biashara kwa wingi?

Mheshimiwa Spika, kuhusu wafanyakazi wa *E.A. Community*, ni nini hatima yao? Kiasi gani kililetwa katika kulipa wafanyakazi hawa Uganda, Kenya na Tanzania?

Mheshimiwa Spika, kuhusu madeni ya ndani, utaratibu gani wa kuyalipa madeni ambayo yamesha hakikiwa hasa:-

- (a) Wanaolisha Taasisi?
- (b) Walimu na watumishi wengine wanaodai mafao (*areas*) ya uhamisho na kupanda vyeo?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Makao Makuu Dodoma, mpango wa kuhamia Dodoma 2004/2005, zimetengwa shilingi ngapi? Zipi zenye gharama kubwa, silizohamia Dodoma au zilizobakia Dar es Salaam?

Mheshimiwa Spika, natoa hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na Watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *gender positions*, ni wanawake wangapi wanaoshika nafasi za juu katika Wizara ya Fedha? Si lazima kwa majina, idadi inafaa na maeneo ya nyadhifa za juu inatosha. Kuhusu vibali vya sukari na vyakula, wangapi walipewa vibali vya kununua chakula cha njaa tangu Septemba, 2003? Mchele wa *RTC Dar es Salaam*, Wizara ina mpango gani? Mchele wa *VIP* uliletwa kwa kusaidia njaa au kama *additional abdominal food shortage*?

Mheshimiwa Spika, uhusiano uliopo kati ya Wizara ya Fedha - Kitengo cha Maafa na Wizara ya Kilimo kuhusu uagizani, ununuzi na usambazaji wa chakula ukoje? Njia ipi Wizara ya Fedha inapendekeza ya kusaidia awamu hii na ya nne itakayoondoa manung'uniko ya vyakula nchini?

**MHE. STEPHEN M. KAHUMBI:** Mheshimiwa Spika, wakati nachangia Asubuhi niliweka mezani taarifa tatu:-

- (a) Malalamiko ya Ndugu Maulidi N. Kayega anayedai kulipwa fedha kwa Bima zake tatu zilizoiva, lakini *NIC* wanaonekana kuzembea.
- (b) Malalamiko ya Bibi Agness S. Mkekwa aliyerejeshwa kazini kwa amri ya Mheshimiwa Juma Kapuya, lakini uongozi wa *TRA* ukafanya Vinginevyo.
- (c) Malalamiko ya Bibi Phillipwa Ngowi aliyeahidiwa kupatiwa ufumbuji wa tatizo lake tangu tarehe 15/6/1998.



Tumezungumza na Ndugu Kitilya anayenieleza kuwa anazo kesi saba (7) za namna hii ya Bibi Mkemwa na akadai kuzishughulikia kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi hawa hawashtaki, lakini wanaomba wasaidiwe ili menejimenti iwarejeshe kazini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RAMADHANI H. KHALFAN:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Waziri mwenyewe Mheshimiwa Basil P. Mramba (Mb.) na Manaibu wake - Mheshimiwa Abdisalaam I. Khatibu (MB.) na Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu (Mb.), pia Makatibu Wakuu - Bwana G.S. Mgonja na P.M. Lyimo, Manaibu Katibu Mkuu - R. Khijjah na W. Nyachia, vile vile Wataalam wengine wote wa Wizara ya Fedha na Wafanyakazi wengine wote katika ngazi mbalimbali kwa michango yao mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya uchumi. Ni dhahiri kabisa kuwa hali ya uchumi inaridhisha sana. Ukuaji wa uchumi umeathirika kutokana na sababu ambazo binadamu hana kabisa uwezo wa kuzizuia. Jitihada hazishindi kudra. Kwa misingi hiyo, Wizara inastahili pongezi za kila mmoja wetu katika hili. Bado kuna matumaini makubwa Mheshimiwa Waziri chini ya uongozi wake mahiri sana na timu yake, hali itadhibitiwa na ukuaji wa uchumi utaendelea kama inavyokusudiwa katika miaka ijayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukusanyaji wa mapato ya ndani. Taarifa ya ukusanyaji wa mapato ya ndani kuweza kuvuka lengo kila mwezi, siyo taarifa nzuri, bali pia ni mojawapo ya viashiria muhimu vya ufanisi wa kazi ndani ya Wizara ya Fedha. Napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa hili kwani kulifanikisha kwake zoezi hili ndiyo kujenga ule msingi wa kufikia dhamira yetu ya kujitegemea na kupunguza utegemezi kwa wafadhili. Kushuka kwa kiwango chetu cha utegemezi wa wahisani katika Bajeti yetu kutoka asilimia 47% (2002/03) hadi asilimia 45 (2003/2004) na sasa kwa asilimia 41% (2004/2005) ni mafanikio makubwa ya kujivunia sote na nalazimika kumpongeza kwa dhati kweli kweli katika suala hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ufutaji wa kodi na ada kadhaa. Suala la leseni za biashara kwa ujumla wake limechukua sura mpya kabisa na ya kimapinduzi. Ada za leseni kufutwa na ukataji wa kila mwaka wa leseni hizo za biashara kusitishwa, madwa ya binadamu/mifugo, vyandarua (hasa kwa sisi tuishio Pwani kwenye mazalia makubwa ya mbu), vifaa maalum vya walemavu kuwa kwenye kiwango cha sifuri cha kodi; ni hatua ya kuwatambua wanyonge na kuwathamini. Vile vile uamuzi wake wa kijasiri wa Mheshimiwa Waziri wa kutoa unafuu wa asilimia 100% wa kodi ya mapato kwa wakulima na wafugaji, utachochea uzalishaji kwa kiwango kikubwa. Vifaa vya uvuvi (nyavu) na Vinginevyo pia vimejumuishwa katika kuwapatia unafuu wavuvi wetu. Kwa niaba ya wavuvi wa Bagamoyo, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, dhamira aliyowieleza Mheshimiwa Waziri ya kupendekeza kufanya marekebisho katika sheria mbalimbali za kodi, imedhihirisha moyo wake wa

kweli wa kumpa Mtanzania wa kawaida mazingira muafaka ya kujikimu na hata kupiga hatua kubwa zaidi ya kujiendeleza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sura ya Bajeti. Kwa hakima ni sura yenye haiba ya kuridhisha sana. Maeneo ya mapato *ABCD*, nimevutiwa kuona eneo A (mapato ya ndani Shs. 1739288m/=) limekiuka eneo B la (mikopo na misaada ya nje ikijumuisha na *HIPC* ya jumla ya Shs. 1367025m/=) kwa asilimia 27.23%. Huu ni mwelekeo mzuri sana Mheshimiwa Waziri. Maeneo ya matumizi *EFG* vilevile ni mazuri. Ombi langu Mheshimiwa Waziri ni usimamizi mzuri wa matumizi haya na kudhibiti ufujaji, ubadhirifu na wizi wa fedha hizi unazitafuta kwa taabu kubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba tuangalia ni kwa namna gani taarifa za Mdhibiti na Mbaguzi Mkuu (*CAG*) tunavyoweza kuzifanyia kazi na kuwaadhibu wahusika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kikamilifu na kwa dhati kabisa.

**MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO:** Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha anitatie kero ya mpiga kuwa wangu Mwalimu mstaafu ambaye hajalipwa pensheni yake. Ufafanuzi wa kero:-

Jina: Mwalimu Hemed Najumwe.

Jina la Uanachama: *TSCC No. ES-N6368*.

Mheshimiwa Spika, mwanachama huyu alipewa *Cheque No. 0230355* ya Shs. 6.69 milioni na Hazina, Pensheni *Dept.* tarehe 26/3/2004. Alipewa *cheque* hiyo *NMB Nachingwea*. Hajalipwa hadi leo. *NMB Nachingwea* inaeleza kuwa *cheque* imepotea huko *NMB Headquarters, Dar es Salaam*. Inadaiwa Hazina watatoa *cheque* nyingine. Naomba malipo yaharakishwe, uzembe ni wa *NMB Headquarters*.

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Spika, hotuba zote ni nzuri na kama utekelezaji wake utatekelezeka, kwani malengo ya mipango ambayo Bunge tunalipitisha. Watumishi wa ngazi za chini mikoani na Wilayani na kadhalika hawasimamii kikamilifu. Hivyo, ili Bajeti iwe na maana, hakikisha usimamizi wa karibu unakuwepo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Benki ya Wakulima. Serikali itoe maelezo ya faida yake nini na tofauti na Benki ambazo zilizokuwepo hapo nyuma na hazikuleta mafanikio kwa mkulima. Ni kwa jinsi gani na zitaendeshwa na nani tofauti na Watanzania waliofanya kazi huko nyuma? Ikiwezekana ziboreshe tu Benki zilizopo na ni jinsi gani mkulima wa kijijini atanufaika nazo.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Mtwara kuna mabonde ya maeneo ya Mto Ruvuma mazuri sana na yenye mbolea ya asili. Wakulima hutumia vijembe vidogo, hawawezi kudhibiti maji wakati wa mvua - mto huhamahama. Wanahitaji nguvu ya Serikali Kuu ikiwemo na Wataalam, jinsi ya kuwasaidia ili watumie vizuri bonde hilo kwa uzalishaji. Maji ni mengi ambayo yanaharibika bure wakati wa kiangazi. Wangeweza kuzalisha chakula cha kutosha, lakini wapi. Serikali itekeleze yale ambayo wakulima wenyewe

hawawezi. Je, kwa mfano huo mdogo, ipo sababu ya Tanzania kuwepo na njaa? Ingawa tumechelewa huko nyuma, basi kipindi hiki tuwandae vizuri wakulima wetu wakiwemo na vijana ambao Serikali inatamka kwamba ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wetu. Lakini hivi sasa hawalimi na hawazalishi - ni wavivu. Wakati wote ni kulala tu na wako mstari wa mbele kudai haki. Kipindi hiki mikakati itakayoandaliwa nguvukazi hii (vijana, itumike kikamilifu na Serikali ikikubaliana na ushauri wangu tutaondokana na aibu ya ombaomba Tanzania, siyo tu maskini.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuondoa gharama za leseni kwa wafanya biashara Wadogo Wadogo na kulipia ada kila mwaka. Nilipokea malalamiko mkoani ya wafanye biashara wakasema viduka vyao vimekufa kwa gharama za malipo wanayodaiwa na *TRA*. Hivyo kabla sijalifanyia kazi katika kikao hiki cha Bunge la Bajeti, jibu limepatikana kwani wenyewe ni wasikivu wa redio - wamesikia moja kwa moja. Naishukuru Serikali na kuipongeza, lakini nashauri ufuatiliaji wa ulipaji mapato. Kukadiria kodi zao lazima kuwe na watumishi wenye uwezo na wenye kupenda Raia na Serikali, sababu wakati mwingine haki hazitendeki kwa wafanya biashara kwa ukadiriaji na matozo yake.

Mheshimiwa Spika, dhamira yangu kubwa ni kuunga mkono hotuba zote mbil, hotuba ya Mheshimiwa Basil Mraba na Mheshimiwa Kigoda mia kwa mia.

**MHE. MARGARETH J. BWANA:** Mheshimiwa Spika, na penxca kutamka kuwa ninaunga mkono hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri wa Fedha - Mheshimiwa Basil Mramba kwa kazi nzuri sana anayoifanya katika Wizara hii. Wote tumeshuhudia mafanikio makubwa yaliyopatikana tangu amekuwa Waziri katika Wizara hii. Nampongeza sana. Aidha, Manaibu Waziri, nawapongeza pia Makatibu Wakuu na wote waliosaidia kufanikisha maandalizi mazima ya bajeti hii.

Pili, Mheshimiwa Spika, ninampongeza kwa dhati Kamishna Mkuu wa *TRA* - Ndugu Kitilye kwa kazi nzuri sana anayoifanya. Wote tumeshuhudia kuongezeka kwa mapato ya Serikali mwezi hadi mwezi. Hii inadhihirisha namna ambavyo wamejipanga vizuri katika kukusanya mapato haya. Nawapongeza wote anaoshirikiana nao katika kusimamia mapato hayo kote nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa ninaomba nichangie katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu vyombo vya Ulinzi na Usalama. Nimefurahishwa sana kwa kitendo cha kuongeza Bajeti katika vyombo hivi vya ulinzi na usalama. Hii imenitia moyo sana nikiamini kuwa mapungufu makubwa ya ukosefu wa vifaa vya ulinzi na usalama katika Mkoa wetu wa Rukwa sasa litapata ufumbuzi. Tulishaomba muda mrefu wa kununuliwa kwa *speed boat* ambayo itakuwa inafanya doria katika ukanda wa Ziwa Nyasa, kufuatia uvamizi wa maharamia ambayo yamekuwa yakivamia wananchi

wa maeneo hayo mara kwa mara na kuwafanya wananchi hao kuishi kwa wasiwasi muda wote.

Mheshimiwa Spika, tunaomba hiyo *speed boat* itakayonunuliwa basi iwe na *speed* kubwa kushinda hiyo wanayoitumia hao wavamizi. Pia tunaomba askari wetu wa mpakani nao pia wapewe zana bora na za kisasa ili kuimarisha ulinzi. Hivyo, vifaa kama *radio calls* pamoja na magari kwa vituo vya Polisi vya mpakani vinunuliwe na kusambazwa katika maeneo hayo. Visije vikawekwa maeneo ya mijini tu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mishahara ya Walimu. Walimu wa Wilaya ya Nkansi wamekuwa wakidai mishahara yao ya kuanzia mwezi Machi - Juni, 2004 na aorodha yao nimeiwasilishwa kwa Waziri wa Elimu kwa barua yangu ya tarehe 11/6/2004. Aidha, wapo Walimu wanafunzi ambao walianza kazi kuanzia mwezi Juni, 2003; wamekuwa wakidai mishahara yao kuanzia Juni, Julai, Agosti na Septemba, 2003.

Mheshimiwa Spika, ni nini kinachosababisha kutolipwa mishahara hiyo, hatufahamu. Hali ambayo inawafanya Walimu hao kuishi katika mazingira magumu sana. Ninaomba Wizara ya Fedha ikishirikiana na Wizara ya Elimu kulipa utanzushi wa suala hili. Pia ile mikopo iliyotolewa kwa Walimu hawa hawajapata. Sasa sijui zoezi hili la kutolewa mikopo bado linaendea au limekwisha.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na utata wa malipo ya Bima Pindi inapoiva. Lakini kule Rukwa yaelekea kuna matatizo. Walimu/Watumishi wengi wamelalamika kuwa Bima zao zimeiva, lakini wamekuwa hawalipwi na kuzungushwa ni kwingi. Tunaomba mtusaidie kufuatilia na kujua tatizo ni nini. Kwa nini malipo hayo yanaleta utata?

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kilimo. Nimefurahi sana kwa kuongeza fedha na kuathiri kuwakopesha wakulima wadogo wadogo. Ninaomba suala la pembejeo lingekuwa mikononi kwa Serikali baada ya kuwategemea watu binafsi ambao ndio wamekuwa ni waagizaji wakuu wa Pembejeo hususan mbolea. Mwaka 2003, Mkoani Rukwa mfuko mmoja wa mbolea uliuzwa hadi Shs. 27,000/= . Kwa kweli hatukuona hata ule unafuu uliosema na Serikali. Maana gharama ni zilezile. Katika ufuatiliaji wa suala hili tuligundua kwamba:-

(a) Kumbe Wizara haikuagiza mbolea. Badala yake walinunua mbolea kwa mfanya biashara. Wafanya biashara hao wanaagiza mbolea kidogo ambayo haitoshelezi na matokeo yake inauzwa kwa bei kubwa.

(c) Ucheleweshaji wa usambazaji wa mbolea. Kwa mfano, mwaka jana mbolea ilifika kwa kuchelewa na kukuta mahindi yameishaota. Hivyo, kwa upande wa Rukwa tunaomba mbolea iwe imefika Rukwa kati ya Septemba na Oktoba kila mwaka, ili mwezi Novemba wanapoanza kilimo wawe na mbolea tayari. Ninaomba mnisaidie Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo, ninaunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE ALHAJI SHAWEJI ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, mimi naunga mkono hoja ya Bajeti ya Waziri wa Fedha. Pamoja na kuunga mkono, naomba kuchangia na kupata maelezo katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, sura ya Bajeti katika mapato ya ndani, Waziri wa Fedha hakuonyesha kama utalii ni chanzo kikubwa cha mapato ya ndani na kwa sababu hiyo Mheshimiwa Waziri wa Fedha hakuonyesha katika mpango wa mwaka 2003/2004, Taifa letu limeingiza kiasi gani cha fedha.

Mheshimiwa Spika, upunguzaji wa viza kutoka dola za Kimarekani 200 hadi kufikia dola za Kimarekani 50 ni hatua muhimu sana ya kukuza sekta ya utalii. Lakini sura ya Bajeti katika mapato ya ndani, Waziri wa Fedha hakuonyesha kama utalii ni chanzo kikubwa cha mapato ya ndani.

Katika nchi nyingine duniani, utalii ni chanzo kikubwa sana cha mapato ya Taifa. Nyingi ya nchi hizo, utalii wake mara nyingi huwa masanamu na michoro ya vitu vya kale. Katika nchi yetu tunayo bahati kubwa sana kiutalii. Tunayo mapango mengi ya kale kule Kilwa, Njombe, Kondo na Bagamoyo, yenye vitu vingi vya kale ambavyo kama Serikali ingewekeza fedha za kutosha, vitu vya kale katika mapango ya Kilwa, Njombe na Bagamoyo ingekuwa chanzo kikubwa cha pato la Taifa. Aidha, nchi ina misitu yenye sifa kubwa, haipatikani kokote kule duniani. Misitu hiyo inaitwa *Eastern Mountain Arc* inapatikana Tanzania tu.

Hivyo, Mheshimiwa Spika, kama Serikali ingewekeza miundombinu katika maeneo haya, ingekuwa kivutio kikubwa sana cha kuvutia watalii. Ukichanganya mambo hayo na utajiri wa mbuga za wanyama pori na wanyama pori wenyewe, Taifa letu lingekuwa na chanzo kikubwa sana cha mapato ya Taifa. Nadhani ni vizuri Mheshimiwa Waziri wa Fedha anipe maelezo yaliyompelekea anyamaze kimya bila kutoa maelezo ya utalii na kuonekana si sehemu muhimu ya mapato ya ndani.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 65 aya 54, Mheshimiwa Waziri wa Fedha Amesema Bajeti hii inaonyesha jitihada za kupambana na umasikini. Mimi nakubaliana naye. Lakini naomba kumshauri Waziri wa Fedha kuwa sasa Serikali lazima iweke wazi dhamira ya utekelezaji wa mipango yake ya maendeleo. Kama inavyofahamika nchi ya Misri wakati walipokuwa wanajenga bwawa lao la Aswan na Ziwa Nasser, walipokosa wahisani kuwekeza katika mradi wao, Rais Nasser alitumia *Suez Canal* kumwezesha kupata fedha za kujengea Bwawa la Aswan. Kwa uamuzi wa dhamira hiyo, nchi ya Urusi ilikubali kushiriki katika ujenzi wa Bawa la Aswan.

Mheshimiwa Spika, kwa mifano kama hiyo ya kuwezesha kutekeleza dhamira ya mikakati kimaendeleo, namshauri Waziri wa Fedha akubali kufikia kutumia utajiri wa madini yetu kutuwezesha kujenga mabwawa katika Mto wa Rufiji, Mto wa Ruvuma, Mto wa Wami na Mto wa Ruvu. Nionavyo mimi, ujenzi wa mabwawa hayo utasaidia sana kupata *water resources* za kutumia kutupatia umeme na kuuza nchi za jirani na kutuwezesha kuboresha *Irrigation Systems* zetu katika kupanua na kuongeza kilimo

chetu. Kwa utekelezaji wa dhamira hii, Serikali itaweza kufuta tatizo la ajira kwa kiwango cha asilimia kubwa na kufuta tatizo la upatikanaji wa chakula kwa asilimia kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yake ya Bajeti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha katika ukurasa 65 amesema anatambua Watanzania wengi wanaishi vijijini na wanaotegemea kilimo kwa chakula na ajira. Amesema lazima mkakati wetu wa kuinua kilimo uwe imara zaidi. Alilosema Mheshimiwa Waziri, mimi kimsingi nalikubali. Lakini inabidi ayajazie nyama. Kwa maoni yangu, hamu ya kutamani mikakati yetu kuwa imara siyo kigezo cha kuinua kilimo, kwa sababu lugha hiyo ya kuinua mikakati kuendeleza kilimo karibu kila Bajeti ya Wizara ya Fedha inatajwa.

Mheshuniwa Spika, mimi nilifanya mazungumzo na Mheshimiwa Waziri wa Fedha tarehe 12/4/2004 katika viwanja vya Bunge kuhusiana na hoja ya maombi ya kupatiwa umeme *Berega Mission Hospital, Mgugu Secondary School*, Berega, Magubike na Maguha kutoka Dumila. Katika mazungumzo yetu, nilimweleza kuwa Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa miaka minne iliyopita alikuja kufungua daraja kubwa sana la Mto Berega. Kabla ya ujenzi wa daraja hili, wagonjwa wengi walipoteza maisha yao na maji ya Mto Berega, wakivuka kwenda Hospitali ya Misheni ya Berega.

Mheshimiwa Spika, nilimweleza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufungua daraja hili la Berega. Alitembela Hospitali ya Berega pamoja na Wodi ya wagonjwa. Baada ya kumaliza kutembelea Hospitali ya Berega, alikwenda kuweka jiwe la msingi katika Shule ya Sekondary ya Mgugu. Zipo shule tatu tu zenye sifa ya shule hii ya Mgugu hapa Afrika. Shule ya aina hii moja ipo Kenya ya pili ipo Tanzania na ya tatu ipo Senegal.

Mheshimiwa Spika, nilimweleza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kumaliza kutembelea hospitali ya Berega na kuambiwa kuwa hospitali hii inatoa huduma kwa mikoa minne, yaani Mkoa wa Manyara, Mkoa wa Tanga, Mkoa wa Dodoma na Mkoa wa Morogoro; na kuelezwa kuwa hii ndiyo hospitali kubwa pekee iliyo karibu na barabara ya kutoka Morogoro hadi Dodoma na hivyo kuwa katika *Highway* ya Dodoma - Morogoro. Pia aligundua umuhimu wa hospitali hii kwa ajili hii. Kwa ajili hii, alitoa ahadi kuwa Mama Anna Mkapa angeleta dawa kama mchango wake katika hospitali hii.

Aidha, Mheshimiwa Spika, baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano - Mheshimiwa Benjamin William Mkapa kuweka jiwe la msingi, nilimweleza Mheshimiwa Waziri wa Fedha katika Shule ya Sekondari ya Mgugu, alitoa ahadi ya kujenga nyumba ya Maktaba na akaahidi kuleta vitanda na magodoro mia mbili (200). Pamoja na ahadi hizo, pia alisema atatoa maelekezo ya kupatikana kwa umeme na kwamba atapanga kutembelea Berega bila taarifa rasmi.

Mheshimiwa Spika, nilimjulisha Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuwa ahadi zote alizozitoa amekamilisha. Dawa za hospitali ya Berega zilipatikana. Vitanda na

magodoro ya Shule ya Sekondari ya Mgugu yamepatikana, hivyo ametimiza ahadi yake. Pia alifanya ziara ghafla bila taarifa kutembelea Berega. Ahadi hii alitimiza. Alifanya ziara bila kutoa taarifa, kutembelea Berega.

Mheshimiwa Spika, nilimweleza Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuhusu ahadi ya kupeleka umeme. Nilimweleza kuwa Ikulu ilikwisha iandikia barua Wizara ya Nishati na Madini. Katika kutekeleza maagizo ya Ikulu, Wizara ya Nishati na Madini ilimwandikia *Regional Manager* wa *TANESCO*, Mkoa wa Morogoro ili apelike taarifa ya makisio ya kupeleka umeme kutoka Dumila kupitia Maguha, Magubike hadi Shule ya Sekondari Berega na *Berega Mission Hospital*.

Mheshimiwa Spika, nilimjulisha Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuwa *Regional Manager* alitekeleza kufanya bajeti kama alivyoagizwa na Wizara yake na kupeleka Wizarani. Bajeti hiyo ilionyesha kuwa mradi huo ni *viable*, yaani unaweza kujilipa.

Mheshimiwa Spika, nilimweleza Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuwa baada ya mimi kufuatilia katika Wizara ya Nishati na Madini, nafurahi kukujulisha kuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Dr. Ibrahim Msabaha alifanya ziara katika maeneo yote ambayo Rais Benjamin William alipitia. Kwa kweli Naibu Waziri alikiri kuwa maeneo hayo yanastahili kupelekewa umeme na gharama za umeme huyo zinalipika. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini - Dr. Ibrahim Msabaha aliahiri kuleta dawa katika kituo cha Magubike. Nafurahi kukujulisha kuwa ahadi hiyo ilishatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, nilimweleza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa nakala ya barua hii namwomba Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini atekeleze matakwa ya ushauri wake alionipa kwa kumwomba atekeleze matakwa ya maagizo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa kuingiza mradi huu katika bajeti ya mwaka wa 2004/2005 kwa lengo la kutaka kutimiza ahadi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Benjamin William Mkapa.

Mheshimiwa Spika, nilimweleza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, atamaliza kipindi chake cha uongozo hapo ifikapo mwaka wa kesho (2005), kwa maoni na ushauri wangu isingekuwa vizuri akaondoka bila kukamilisha ahadi yake.

Mheshimiwa Spika, nilimweleza Mheshimiwa Waziri wa Fedha katika mazungumzo yetu katika viwanja vya Bunge kuwa aliniagiza nimweleze Waziri wa Nishati na Madini aweke maombi hayo katika Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini ya mwaka 2004/2005. Mimi nimetekeleza kama ulivyonieleza na nakala ya barua hii nimempa Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kwa utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, tarehe 11/6/2004 baada ya kutoa hotuba yake ya Wizara ya Fedha, nilikutana tena na Mheshimiwa Waziri wa Fedha katika viwanja vya Bunge na kumkumbusha juu ya hoja hii ya umeme. Kwa mara nyingine tena ameniambia

nimwandikie ili katika kipindi cha siku tano (5) za kujadiliwa kwa Bajeti ya Wizara ya Fedha, atashughulikia hoja yangu hii.

Mchango huu unajumlisha pamoja na maombi yangu aliyonitaka Mheshimiwa Waziri wa Fedha, alichonitaka nimpatie ndani ya siku tano (5) wakati hotuba yake inajadiliwa na Wabunge. Ni matumaini yangu kwa tabia ya ukweli aliyo nayo Mheshimiwa Basil P. Mramba, suala la hoja yangu atalishughulikia ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuwa na Benki ya Wakulima, katika mwaka huu imetajwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Ubinafsishaji), Dr. Abdallah Omari Kigoda, uanzishaji wa Benki ya Kilimo, kama mikakati wa kuinua kilimo na uendelezaji wa mifugo na uvuvi. Katika bajeti ya mwaka jana, hoja ya kuanzishwa kwa Benki ya Wakulima, Wafugaji na Wavuvi; ilitamkwa katika Bajeti ya Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, kiutekelezaji mikakati huo wa kuanzishwa Benki ya Wavuvi, Wafugaji na Wakulima haukufanyika. Kutokana na matokeo hayo, nashauri Serikali itamke na iandae miundombinu ya kuendeleza kilimo na ufugaji bora. Haitoshi kumilikisha wananchi maeneo ya ufugaji bila kuwaandalia miundombinu ya msingi na wala haipendezi kuwadai fidia ya gharama za *surveying* wakati kwa maoni yangu *surveying* ni sehemu ya miundombinu anayotakiwa kuandaliwa mwananchi kabla ya kumilikisha.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yake ya Bajeti, Mheshimiwa Waziri amesema riba inatazamiwa kushuka hadi kufikia asilimia 13% na wale wanaowekeza (*deposit*) itakuwa asilimia 40%. Kwa hesabu hizo inaonekana mabanki ambayo kwa kawaida yana mtizamo wa kupata faida, yamelegeza kamba. Bado kwa maoni yangu, hatua hiyo haitasaidia kuinua kilimo kwa hoja kwamba gharama za inflation hazikuzingatiwa wala kuweka maanani. Pia utaratibu wa mabanki ya biashara ni kutoza riba kuanzia saa na siku ile mkulima anapopata mkopo.

Kwa hiyo, kwa maoni yangu kumwokoza mkulima ili kuinua kilimo chetu, iwepo dhamira ya kuanzisha Benki ya Wakulima ambayo itakuwa na riba ndogo ya asilimia 3% na kupewa *grace period* ya miaka mitatu (3) kabla ya kulipa na alipe katika *installment* kumi (10). Na Benki hii iwe chini ya Wizara ya Kilimo na Chakula. Pale itakapolazimu pia waandaliwe miundombinu. Kwa maoni yangu, njia ya utekelezaji wa utaratibu huu utainua na kukifanya kilimo chetu kiwe endelevu.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu si jangwa. Kwa hiyo, kupendelea au kuchagua baadhi ya mikoa na kuipa kipaumbele kwa kuwapatia mbolea na pembejeo nyingine, si mwelekeo wa kuimarisha kilimo. Kwa maoni yangu, kigezo kikubwa ni kujizatiti kwa kutambua mahitaji ya soko ni kutambua misimu ya nchi za masoko ya mazao yetu ili kuyafanya yawe na *demand* kila mazao yetu yanapoingia katika masoko ya ushindani. Haya utekelezaji wake itategemea sana uwezeshwaji wa wakulima kwa kupata miundombinu na mikopo. Pamoja na maelekezo hayo, Serikali inabidi iwe macho isije kujikuta huduma za msingi za kilimo zinaelekezwa kwa baadhi ya mikoa, jambo ambalo linaegemea sana kiuchumi, bado litagusa hisia za kisiasa. Hatua hiyo inaweza kujenga



msingi mbaya Kitaifa. Nashauri Wizara ya Fedha iangalie utekelezaji wa utaratibu huu kwa uangalifu sana.

Mheshimiwa Spika, katika mpango huu wa Bajeti ya mwaka 2004/2005, nimeshindwa kuelewa Mheshimiwa Waziri wa Fedha ametumia vigezo gani vilivyopelekea Wizara ya Fedha kujenga hoja ya kuandaa mpango wa Bajeti bila kuonyesha *Actual Estimated Financial Performance* Kiwizara na Kiidara na *Actual Estimated Physical Achievement* ya mpango wa Bajeti Kiwizara na Kiidara ya mwaka 2203/2004 ili tupate kujua *variance* Kiwizara na Kiidara kati ya *Approved Financial Budget and Estimated Physical Achievement Estimatives*. Kwa maoni yangu, *variance* inasaidia kujua kama utekelezaji wa Bajeti ni mzuri au mbaya. Kwa kutambua hiyo, *variance* upangaji wa malengo ya Bajeti, yanaweza kutoa picha kamili zaidi katika matayarisho ya upangaji wa malengo ya Bajeti ya mwaka unaofuata.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kanuni ya Bunge Na. 49 (7), nimegundua mara nyingi ingawa kanuni inaturuhusu kuchangia kwa maandishi, baadhi ya Mawaziri hupenda zana kutoa majibu ya Wabunge wanaochangia kwa kusema kwa mdomo kwa ajili hii. Naomba michango yetu tunayotoa kwa maandishi nayo ijibiwe na Mawaziri kama vile wanavyojibu michango ya Wabunge wanaochangia hoja kwa mdomo.

**MHE. BALOZI AHMED HASSAN DIRIA:** Mheshimiwa Spika, pongezi nyingi sana kwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango, kwa hotuba zao nzuri na zenye mwelekeo wa kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Tanzania inaingia katika *twenty first century*, na natumaini kutokana na ushindani wa uchumi duniani. *Vision* ya 2005 inaeleza wazi juu ya dhamira ya Taifa letu, na inatoa taama kubwa. Ni muhimu kwetu kwanza kuwa na chakula cha kutosha. Hivyo kilimo cha umwagiliaji maji ni muhimu. Hivi sasa tunalima asilimia 6% ya ardhi yetu. Hivyo kilimo bado kinataka kutiliwa nguvu zaidi

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana juu ya suala la *Credit Guarantee Scheme*. Hii ni muhimu sana kwa Taifa kama letu, linalotegemea kilimo. Hivi sasa tuna shida ya vijana wanaotoka mashuleni. Ni muhimu kuendeleza shule za Ufundi katika Taifa letu ili vijana wetu waweze kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wastaafu. Naamini hili ni jambo kubwa kwa Serikali kukubali kuwarejesha katika daftari la kupewa penshen wastaafu hawa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vyombo vya usalama, tunapongeza suala la kuongeza fedha kwa vyombo vya ulinzi kutokana na matukio ya ujambazi nchini. Pia ni jambo la kufurahisha sana kwa kuendelea kuweka kasma juu ya chakula cha dharura endapo hali ya hewa itakuwa mbaya.

Mheshimiwa Spika, ni vyema zaidi utambuzi wa Serikali kukumbuka wafanya biashara ndogo ndogo. Hawa wanachangia katika uchumi wa Taifa letu na wataingia katika mtiririko wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, biashara ya nje imepungua, na uagiziaji umekuwa ni muhimu sana kwa Serikali kupunguza au kufuta ushuru juu ya vyombo vya uvuvi na kufuta ushuru kwenye zana za kilimo.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi nyingi sana kwa Serikali na Waziri wa Fedha na Waziri wa Uchumi kwa kusema kuwa Bajeti hii ni ya kuukomboa umma wetu katika umaskini.

**MHE. ABU T. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia Bajeti ya mwaka huu wa fedha 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Mramba na Watendaji wake kwa kuandaa Bajeti yenye kuendeleza mafanikio ya mageuzi ya kiuchumi na kuelekeza mageuzi hayosasa kwenye sekta za Kilimo, Viwanda na Biashara na hasa kuwezesha kuwaingiza wafanya biashara ndogo ndogo kwenye mkondo rasmi wa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kupokea kwa vitendo kwa malengo ya kiuchumi mpana na mdogo wa Serikali pamoja na malengo ya tamko la *BoT - Monetary Policy Statement objectives* kwa mwaka 2004/2005 unaonyesha umahiri wa Wizara yake kutekeleza sera ya nchi ya utawala bora. Ni kwa taratibu hii pekee, ndipo nchi yetu itaweza kufanikisha kwa kasi ya maendeleo ya mageuzi yetu ya kiuchumi tuliyomkisha fanikisha hadi sasa. Pamoja na kukiri ubora wa Bajeti hii, ninayo haya ya kuongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ni kwenye Sekta ya Kilimo. Miaka iliyopita, mchango wa kuendeleza kwenye sekta hii kama ulikuwepo ulikuwa mdogo. Mungu bariki kutoka mwaka 2003/2004 wa kifedha, Serikali ilianza kujitengea kwa hela za ndani kwenye kuendeleza sekta hii. Nashauri juhudi hii iendelezwe. Mchango wa mwaka huu wa takriban *T.Shs. 10b./=* watia moyo. Lakini lazima tuendeleze azma hii kwa kutambua kuwa asilimia 45% ya pato la nchi linatokana na sekta hii.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kwenye kilimo, pia tutekeleze sasa azma ya kuinua Sekta ya Viwanda na Biashara, hususan kwenye mikakati yetu ya kukuza bidhaa zetu nje ambazo zinazalishwa kwenye sehemu tulizotenga na *EPZ - kama vile millennium Business Park Ubungo*. Kwa mauzo ya takriban US \$ 998.3 milioni kukuza mauzo kwenye sehemu za *EPZ*, kwa kuchunga US \$ 50,000 ni kiasi kidogo mno. Lakini naamini kwa tamko la Bajeti kuipa Wizara hii kipaumbele, juhudi zaidi zitafanyika kutenga mafungu makubwa zaidi siku za baadaye.

Mheshimiwa Spika, kwenye kuwekeza kwenye Sekta ya Kilimo, lengo liwe wazi. Tunahitaji matrekta zaidi, mbolea zaidi ili kuendeleza kuongeza kilimo cha umwagiliaji. Kwa sababu fedha nyingi za kuendeleza sekta hii hutolewa na wafadhili. Serikali iandae mikakati ya kuzungumza na wafadhili hawa kuelekeza kwenye mahitaji niliyoorodhesha hapo juu na kukubali tu misaada kwenye tafiti mpya. Kuendeleza tafiti ambazo zilizokwisha fanywa kabla ni kuchelewesha tija kwenye sekta hii.

Mheshimiwa Spika, hili la kuongeza tija kwenye kilimo likiunganishwa vizuri na hifadhi ya chakula kwenye ghala zetu za *SGR* kama tuna teknolojia mwafaka ya kutuwezesha kuhifadhi chakula hicho kwa muda mrefu. Naamini *millennium goals, global millennium goals* pamoja na kujikwamua kwenye dimbwi la umaskini litatoweka. Bajeti yetu itaelekea kwa upeo mzuri zaidi wa kujitegemea badala ya kuwa tegemezi. Kila msimu wa mavuno utakapofika tuhifadhi chakula cha kutosha. Tatizo la njaa mwaka huu ni fundisho tosha kwenye kuendeleza sekta hii. Kwa nini tutumie akiba yetu kununua chakula wakati uwezo wa kuwa na chakula tunao?

Mheshimiwa Spika, baada ya kuona vigezo vyote vya uchumi vilipofikia, *GDP growth, headline inflation rate, M2 Road Money Supply* pamoja to *M3*. Katika miaka ya 2003/2004 na 2004/2005 (mwelekeo) tuna kila sababu ya kuamini kukua kwa uchumi wa nchi yetu. Haya yote na ukusanyaji bora wa mapato ya ndani, hali iliyoongezeka toka 1995 hadi sasa kwenye kutekeleza mwelekeo wa nchi kama ilivyotamkwa na Chama Tawala hapo Desemba, 1992. Tanzania ina kila sababu ya kushinda kwenye mageuzi haya ya kiuchumi tuliyoyaanzisha kwenye awamu hii ya tatu.

Ahsante Mheshimiwa Spika, naunga mkono Bajeti hii kikamilifu.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Spika, ningependa kuchukua fursa hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa Waheshimiwa Mawaziri wa Mipango na Fedha, Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda (Mb.) na Mheshimiwa Basil P. Mramba (Mb.) pamoja na Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu wa Wizara hizo pamoja na Watendaji wengine wa Wizara na Taasisi zake kwa hotuba zao nzuri. Mpango na Bajeti ya mwaka 2004/2005 inaendeleza mikakati ya kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na kupambana na umaskini na hivyo kuleta matumaini makubwa kwa wananchi. Naziunga mkono hoja hizi mbili kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuchangia maeneo machache kwa shabaha ya ufafanuzi na mkazo. Kwanza kabisa, nimefarajika kwamba Serikali imeona umuhimu wa kuijumuishia sekta ya Viwanda na Biashara kuwa miongoni mwa sekta zinazopewa kipaumbele. Hii ni hatua sahihi hasa ikizingatiwa kwamba hatua hii ni muhimu siyo tu kwa ajili ya kupunguza nakisi ya urari wa biashara ya nje, kuongeza ajira, mapato ya fedha za kigeni na mapato ya Serikali hasa kwa kuzingatia hali ya utandawazi ambayo inalazimisha hatua za makusudi zifanyike ili kuhimili ushindani mkali unaoongezeka. Lakini dhamira hii nzuri ina nafasi ndogo ya mafanikio yanayotarajiwa kwa kuzingatia kiwango kidogo sana cha Bajeti walichopewa Wizara za Viwanda na Biashara pamoja na Ushirika na Masoko, ambazo zina jukumu kubwa la shughuli za utafiti na kuendeleza masoko pamoja na uhamasishaji na huduma nyingine za ugavi na uhimili kwa wenye viwanda, wafanye biashara na wanaushirika. Ili Wizara hizi na Taasisi zake ziweze kuchangia katika maendeleo ya kasi na endelevu. Hapana budi Wizara hizi zikapewa mgao wa Bajeti utakaowawezesha kuleta mafanikio yanayotarajiwa kulingana na kipaumbele kilichopo.

Mheshimiwa Spika, vikwazo dhidi ya maendeleo ya kazi vilivyoainishwa katika hotuba za Mawaziri na Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2004/2005, ni baadhi tu ya vikwazo. Vikwazo vingine ni pamoja na ughali na upandaji holela wa bei ya nishati, hasa umeme na mafuta ya petroli. Bila kuwa na kanuni na utaratibu madhubuti wa kudhibiti bei za nishati na asthara ya mfumuko wa bei unaoambatana na hali hiyo, haitawezekana kuongeza kasi ya ukuaji uchumi na kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, ningependa kumpongeza Kamishna Mkuu wa *TRA* pamoja na Wasaidizi wake kwa kazi nzuri na mafanikio makubwa katika kuboresha ukusanyaji wa kodi. Hata hivyo, ningependa nielimishwe kuhusu Kampuni ya Ukaguzi ya *COTECNA* kuwepo katika baadhi ya Vituo vya Forodha na kutokuwepo katika vituo vingine. Hali siyo tu inaweza ikaleta mwanya na kupunguza mapato ya uchumi wa forodha, bali pia kuwafanya baadhi ya wafanya biashara kukwepa vituo ambavyo *Cotecna* wapo.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa kuwaondolea wafanya biashara Wadogo Wadogo kero ya leseni na kodi mbalimbali ni ukombozi mkubwa na hamasa nzuri kwao. Kwa upande mwingine hali hii itapunguza mapato ya Halmashauri za Wilaya na kuwepo haja ya Serikali kufidia pengo hilo kwa ruzuku kubwa zaidi. Hata hivyo, sina hakika iwapo Shilingi milioni 11,200 zilizotengwa kwa ajili ya Halmashauri za Wilaya na Shilingi milioni 2,800 kwa ajili ya Viwanda na Biashara zitakidhi haja.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Jimbo langu la Mkinga, ninasikitika kuona kwamba mpango wa Bajeti ya 2004/2005 haikuwekea maanani matazamio makubwa ya wananchi wa Mkinga kuhusu uwekaji lami barabara ya Tanga - Horohoro, uwekwaji umeme vijiji vya Daluni, Gombero, Kwale, Mkinga na Manza, uanzishwaji wa Wilaya mpya ama ya Mkinga au Tanga Vijijini pamoja na miradi kadhaa ya maji. Ni matumaini yangu endapo kutakuwepo mwanya wa kupata akiba a ya mapato ya ziada, Serikali haitasita kutekeleza baadhi ya kero nilizoziorodhesha hapo juu.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Bajeti ya 2004/2005 ni mzuri sana kwa jumla. Hata hivyo, ni muhimu kuweka msisitizo mkubwa katika umakini, uadilifu mkubwa, jitihada kubwa za kuongeza ufanisi na tija, kuwa na taratibu thabiti za utekelezaji na kufuatilia utekelezaji pamoja na kudhibiti ubadhirifu, uzembe, rushwa na maovu mengine ili kuhakikisha mafanikio mazuri na uendelevu. La muhimu kabisa ni kuwa na ratibu (*plan of action*) ambazo zitaonyesha wahusika, mikakati na matokeo yanayotakiwa kwa vipindi mbalimbali na tarehe maalum za ukamilishaji na utoaji taarifa ili hatua za marekebisho au kuendeleza zikichambuliwa kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja ya Mipango ya 2004/2005 na Bajeti ya 2004/2005 kwa asilimia 100.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Fedha na Watendaji wote katika Wizara yake kutokana na kazi nzuri ya Bajeti iliyowasilishwa hapa Bungeni ya 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana baada ya hotuba ya Bajeti, yapo malalamiko niliyotoa kuhusu uwiano mbaya wa fedha zinazotengwa kwa mikoa yenye umaskini unaokithiri, hususan Rukwa, Kigoma, Tabora na Singida. Baada ya mazungumzo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha alisema ataomba tueleze ni maeneo gani tungependa tuongezewe fedha mwaka huu, na sisi tuliomba fedha kwa ajili ya barabara na maji vijijini. Bajeti nzima sijaona Mkoa wa Rukwa kama umepewa fedha za kutosha katika maeneo ya barabara na maji kama tulivyoahidiwa mwaka jana 2003. Kulikoni? Tunazalisha mahindi mengi kulisha Taifa hili, lakini barabara za kusafirishia mahindi hayo ziko wapi?

Mheshimiwa Spika, kilimo chetu bado ni duni na teknolojia ni duni. Utegemezi wa mvua isiyoaminika, hivi tutaendelea mpaka lini? Kwa mtindo huu, kwa nini Serikali isiwekeze fedha nyingi katika kilimo cha umwagiliaji maji mashamba? Tujifunze toka nchi kama Misri, Sudan na nyingine zinazotumia maji kwa umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, nampongeza kwa juhudi za kuondoa VAT kwa Pembejeo za kilimo, uvuvi na madawa. Tunaomba mbolea ipunguzwe bei na ruzuku ifike Rukwa mapema kabla ya msimu wa kilimo kwa kipindi cha 2004/2005. Vifaa vya kilimo vipatikane kwa bei nafuu na mikopo kwa wakulima ipatikane na isiwe na masharti magumu. Benki ya Kilimo ianzishwe haraka kwani kimekuwa kilio cha wakulima Wadogo Wadogo mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Spika, pensheni ya wastaafu itolewe kwa wakati. Lipo tatizo la Polisi waliofanya kazi kwa mkataba wa miaka 10, lakini wakaendelea hadi miaka 20 au zaidi, lakini hawapo katika mpango wa pensheni. Hili tatizo litazamwe upya ili waliovuka mkataba wa miaka 12 waingie katika mpango wa pensheni. Nashukuru kwa kuwarejesha waliochukua pensheni yao kwa mkupua kuendelea na pensheni sasa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mgao wa ruzuku kwa Halmashauri za Wilaya. Kumekuwepo na malalamiko ya mikoa fulani kutopewa fedha za kutosha za maendeleo. Ugawaji huu uzingatie umasikini wa Wilaya hizi maskini zaidi ambazo kwa miaka yote hazikuwa zikipata fedha za kutosha. Kwani msipozingatia hilo, haitakuwa na maana kwa sababu Wilaya zile ambazo tayari ni tajiri na zimekuwa zikipata fedha nyingi za maendeleo ndizo zitaendelea kupata fedha nyingi na hivyo maskini kuendelea kuwa maskini. Tunaomba msikie kilio chetu. Kwa nini kila mwaka tuseme jambo hili hili na Serikali isitusikie?

**MHE. CAPT. THEODOS J. KASAPIRA:** Mheshimiwa Spika, napenda mwanzoni mwa kuchangia kwangu kwa maandishi, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Ulanga Mashariki, natamka kwa ukamilifu kwamba naunga mkono hoja ya Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Comrade Basil P. Mramba (Mb.) na Mheshimiwa Comrade Abdallah O. Kigoda (Mb). Nawapongeza pia Naibu Mawaziri katika Wizara ya Fedha, Makatibu Wakuu na Wasaidizi wao.

Mheshimiwa Spika, katika Bunge hili nimepata kusema mara tatu - 2001, 2002 na 2003. Kuhusu sababu ambazo Waziri wa Fedha, Comrade Basil Mramba,

kuleta katika Bunge Bajeti yake ikigusa wakati wote watu wa kati na watu wa chini, sababu hiyo ni upana na uzoefu wake katika Serikali akiwa katika nyadhifa za Uwaziri na Mkuu wa Mkoa.

Mheshimiwa Spika, anajua Chama (CCM) sera zake, anajua hali ya watu kule chini na kwamba hao ndio tegemeo la uhai wa CCM katika sera zake za ushindi. Hebu angalia ukurasa 32 wa Bajeti ya 2004/2005, mwelekeo wa Bajeti 2004/2005. Hatua kuu 13 zitakazochukuliwa katika kuongeza mapato.

Mheshimiwa Spika, huwezi kuwa na sera safi au Serikali iliyojali watu, bila kuimarisha vyombo vya ulinzi. Na katika Bajeti ya Waziri wa Fedha Comrade Waziri Mramba, ukurasa 40 wa sehemu ya kumi na moja (11). Nashauri suala la wastaafu waliopokea mafao yao kwa mkupuo, Waziri amependekeza waanze kulipwa Januari, 2005.

Mheshimiwa Spika, nashauri jitihada zifanyike walipwe mapema, Januari, 2005 liwe ni lengo; lakini ikiwezekana walipwe mapema iwezekanavyo. Hao ni wenzetu, walifanya kazi nzuri na kwa uaminifu katika Taifa letu. Hao ni wewe na mimi. Ni bahati wao walianza mapema, lakini ingewezekana kabisa ikawa ni mimi au wewe.

Mheshimiwa Spika, Walimu ni moja ya eneo ambalo Bajeti imesema ukurasa 39 kwamba watalipwa malimbikizo ya mishahara yao. Naipongeza kweli kweli Ofisi ya AG inavyosimamia vizuri mno malipo, matumizi ya Serikali. Lakini wizi wa kalamu uliofanywa na watumishi wachache usiumize Walimu au watumishi wengine.

Kazi ya kuziba mianya ya matumizi mabaya itaendelea, utasimamisha mishahara ya watumishi wangapi katika Serikali? Walimu ndiyo viongozi pekee na muhimu katika Taifa letu na wako hadi vijijini. Nashauri tulipe suala hili uzito wa pekee ili Walimu hao walipwe haki zao.

Mheshimiwa Spika, wale wenzetu wenye biashara ndogo ndogo nao wamefutiwa kodi. Huo ni ushindi mkubwa katika Bajeti hii. Ni wakati mzuri kwa chombo chetu Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuongeza bidii na kuwa karibu na walipa kodi kwa kuweka malengo sahihi. Hata kuwa na kipindi katika *radio*, kutoa elimu kwa Watanzania juu ya wajibu wa TRA na kufanya mahojiano na wadau mara kwa mara.

TRA ya leo siyo TRA ya jana. Wafanyakazi wa TRA wanajituma kweli kweli. Ukienda Ofisi ya Kamishna Mkuu, hukuti watu hata kidogo. Hii ni dalili kwamba mgao wa kazi ni mzuri na unaelekea kwa wakuu wote wa vitengo Makao Makuu, Mkoani hadi Wilayani. Nampongeza Comrade Kitilya, Kamishna Mkuu wa TRA.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mipango na Ubinafishaji, Mheshimiwa Abdallah Kigoda nawapa hongera sana. Haijapata kutokea. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE HERBERT J. NTANGI:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wawili kwa mpangilio mzuri wa Bajeti zao kwa maendeleo ya Taifa letu 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia Watendaji wote wa Wizara hizo kwa ushauri mkubwa wanaotoa kwa Waheshimiwa Mawaziri wao na pia kwa Bunge, hasa wakati wa kujibu maswali Bungeni na katika vikao vya Kamati za Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kuelekeza mchango wangu wa maandishi katika maeneo yafuatayo: Kuhusu wawekezaji wanaosamehewa kodi.

Ili kupunguza utegemezi wa wahisani nje katika Bajeti yetu, tuangalie uwezekano wa kupunguza kwa asilimia 50%, misamaha ya kodi inavyotolewa kwa wawekezaji hasa katika sekta ya madini. Maeneo yafuatayo ni muhimu kuangaliwa:-

(a) Vifaa vya uzalishaji kama machine, mitambo, magari, magreda na kadhalika. Vifaa hivi vinabaki kuwa mali yao na inawezekana vikaondolewa baada ya mradi kwisha.

(b) Mafuta (dizeli na petroli) wanayotumia kwa muda wa mradi, yanasamehewa kodi. Hatuna njia ya uhakiki wa matumizi halisi ya mafuta haya wala Hatuwezi kusimamia matumizi bora au ya anasa yanayotumiwa ovyo na viongozi, au wafanyakazi wa makampuni yao.

(c) Kwa vile pia hawalipi kodi ya mapato, badi hawaoni kana kwamba kuna haja ya kujali kubana matumizi. Ni vema walipe kodi maalum ya mapato ili tuweze kujua kiwango cha faida wanayopata.

Mheshimiwa Spika, tukizingatia mapendekezo hayo, basi Bajeti yetu itapunguza utegemezi kwa kiwango kikubwa. Katika kusimamia usahihi wa viwango vya mafuta yanayohitajika katika sekta zinazosamehewa kodi, *TRA* inabebeshwa lawama na makampuni ya mafuta nchini kuwa inateua makampuni ya kuuza mafuta kwa wawekezaji hao.

Mheshimiwa Spika, iwapo kweli *TRA* inateua makampuni hayo, basi *TRA* inajitia udhaifu katika jukumu la usimamizi na udhibiti wa viwango halali vya mahitaji ya mafuta ya msamaha wa kodi. Ni vema *TRA* ikaratibu taratibu za tenda za makampuni hayo na kuwa na nakala ya mikataba kati ya wawekezaji na makampuni ya mafuta ili iwe huru katika kusimamia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi ya *flow meters* - *KOJ*. Maamuzi ya kuwa na *flow meters* ni mazuri. Hata hivyo, katika operesheni za kusafirisha mafuta kwa mabomba Kimataifa, kuna viwango maalum vya *pipeline losses*:-

(a) Je, yapo makubaliano gani kuhusu mapungufu ya mafuta kutokana na *standard pipeline losses*?

(b) Kuna wizi mkubwa sana wa mafuta katika mabomba kutoka eneo la Bandari *KOJ* kwenda kwenye makampuni ya mafuta? Kwa kuwa sehemu hiyo ya mabomba ni mali ya makampuni ya mafuta, Serikali imejikinga vipi kwa hasara hizo na lawama au mabishano makubwa kutoka kwenye makampuni ya mafuta? Hayo yote ni muhimu kwa shabaha ya kuongeza mapato ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu marekebisho katika *Financial Bill, 2004*. Yapo makosa kidogo ya uchapishaji katika *Part VIII - Amendments of the Income Tax Act, 2004* Sehemu ya 28. Katika *table* chini ya *Turnover, Tax band* ya pili, isomeke: “*Where turnover exceeds Shs. 3,000,000/= but does not exceed Shs. 7,000,000/=*”, badala ya Shs. 14,000,000/= *Tax band* ya tatu. Neno: “*exceed*” linakosekana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *flow meters*. Kwa kuwa mafuta mengi yanapitia Bandari ya Tanga kutoka nje ya nchi na pia Bandari za Mwanza, Bukoba na Musoma kutoka Kisumu Kenya, ili kuwa na uwiano wa usimamizi, ni lazima kuwa na *flow meters* huko. Vinginevyo tuwe na kituo kimoja tu Dar es Salaam cha kupokea mafuta yote ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja zote mbili.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefikia mwisho wa mjadala wa jumla, sasa nitamwita mtoa hoja ya kwanza, ile hoja ya Hali ya Uchumi ili aweze kuhitimisha hoja yake. Kanuni zinamruhusu dakika zisizozidi 60, lakini si lazima atumie zote.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:**  
Mheshimiwa Spika, napenda nikushukuru kwa kunipa fursa hii, ili niweze kujibu baadhi ya hoja zilizojitokeza katika hotuba yetu iliyoelezea Mwelekeo wa Mipango yetu katika kipindi tunachokwenda. Lakini vile vile kabla sijaanza kutoa maelezo yangu naomba kwanza niwatambue Waheshimiwa Wabunge, kwanza waliochangia hotuba hii ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji kwa maandishi, lakini vile vile niwatambue waliochangia hotuba hiyo kwa kauli. Naanza na wale waliochangia kwa maandishi. Mheshimiwa Stephen Masaba Kazi, Mheshimiwa Mwanaidi H. Makame, Mheshimiwa Alhaji Shawaji Abdallah, Mheshimiwa Balozi Ahmed Diria, Mheshimiwa Fati S. Mgeni, Mheshimiwa Peter Kabisa, Mheshimiwa Frank Mussati, Mheshimiwa Abu T. Kiwanga, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma na Mheshimiwa Mbarukh Mwandoro.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Edgar Maokola Majogo, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Capt. Theodos Kasapira, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Shah, Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Samwel Chitalilo, Mheshimiwa Esha Stima, Mheshimiwa Sijamini Shaame, Mheshimiwa Juma S. Kidunda, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mheshimiwa Ramadhani H. Khalfan, Mheshimiwa Remidius Kissassi, Mheshimiwa Lydia Boma, Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, Mheshimiwa Asha Ngede, Mheshimiwa Lucas Seleli, Mheshimiwa Thadeus



Luoga, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Amani A. Karavina na Mheshimiwa Grace Kiwelu. *(Makofi)*

Kwa wale Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kauli ni Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Nazir Karamagi, Mheshimiwa Abu Towagale Kiwango, Mheshimiwa Edward N. Ndeka, Mheshimiwa Elisa Mollel, Mheshimiwa Fatma S. Mchumo, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Mheshimiwa Omar Kwaang’w, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mheshimiwa Edson Halinga, Mheshimiwa Dr. Lawrence Gama, Mheshimiwa Ernest Mabina, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Issa Salum, Mheshimiwa Hashim Saggaf, Mheshimiwa Beatus Magayane, Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mheshimiwa Isaac Cheyo, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Suleiman Sadiq, Mheshimiwa Dr. James J. Wanyancha, Mheshimiwa Khalid Suru, Mheshimiwa John Singo, Mheshimiwa Philip Marmo na Mheshimiwa Abdula S. Lutavi.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Paul Ntwina, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Stanley Kolimba, Mheshimiwa Christopher Wegga, Mheshimiwa Musa Lupata, Mheshimiwa Dr. Milton M. Mahanga, Mheshimiwa Dr. Talala Mbise, Mheshimiwa Profesa Simon Mbilinyi, Mheshimiwa Dr. William Shija, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Philip Magani, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Mheshimiwa Bernadine Ndaboine, Mheshimiwa Salome Mbatia, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Frank Maghoba, Mheshimiwa Yete Mwalyego, Mheshimiwa Dr. Hassy Kitine na Mheshimiwa Ibrahim Marwa.

Aidha wengine ni Mheshimiwa Emmanuel Kipole, Mheshimiwa Profesa Juma Mikidadi, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Henry D. Shekifu, Mheshimiwa John Mwakipesile, Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa Haroub S. Masoud, Mheshimiwa Omar Mjaka, Mheshimiwa Shaibu Ahmada Ameir, Mheshimiwa Ali Machano Mussa, Mheshimiwa Stephen Kahumbi, Mheshimiwa Yusuf Kombo Juma, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Bernard Membe, Mheshimiwa William Kusila, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Benito Malangalila, Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Balozzi Ahmed H.Diria na Mheshimiwa Balozzi Getrude Mongella. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote hawa waliochangia hotuba zetu na tunapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu, kwamba ushauri wote na mawazo yote waliyotuletea ili kuboresha Mipango yetu na uendeshaji wa Serikali kiujumla katika masuala ya Mipango na Bajeti tutayafuatilia kwa karibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza napenda tena kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, wamekuwa wakitupa salaam za rambirambi kutokana na msiba uliotupata. Tumefarijika sana na tunawahakikishia kwamba tutajenga roho yenye nguvu zaidi kupambana na suala hili, lakini vile vile imetuhakikishia kwamba tunao ndugu zetu na wenzetu. Tunawashukuruni sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile niseme kwamba majibu yote ya hoja za Waheshimiwa Wabunge, tayari Wizara yangu imeshazijibu imeshazitayarisha na tayari tumekwisha kuziweka kwenye *pigeonholes* za Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, nitakayoyazungumzia hapa ninataka kuelezea tu hali yetu ya mipango na uchumi wetu. Lakini ya kina yamo katika karatasi ile ambayo tumeshaigawa kwa Waheshimiwa Wabunge, tukijibu hoja ya kila Mbunge, ambayo imejitokeza hapa Bungeni. Kwa hiyo, kama sitagusia mengine tukiangalia *documents* ile tutakuta kwamba tumeshaitolea ufafanuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nimekuwa Bungeni sasa kwa kipindi cha miaka tisa hivi, lakini lazima nikiri kuwa hakuna wakati ambapo mchango wa Waheshimiwa Wabunge, umekuwa ni wa kuangalia mbele tunakokwenda kwa makini kama wakati huu. Kwa kweli ninawapongeza kwa dhati Waheshimiwa Wabunge. Tunasema ahsanteni sana. *(Makofi)*

Kwangu mimi ninayesimamia Wizara ambayo ni mtambuka ni wizara ambayo ni *cross sectional is a jack of all trade*. Ushauri ulitolewa na Waheshimiwa Wabunge, utatusaidia katika mikakati ya kuona kuwa tunajitahidi kufanya kazi zetu ili kuendelea na malengo yetu ya uchumi tulivu na endelevu. Wakati huo huo tukiamini kwamba Serikali na uongozi wa kisiasa utaendelea kulinda mafanikio tuliyokwisha kuyapata na hapo hapo sisi kama Wabunge, tuendeleo kushirikiana na kuwahamasisha wananchi, tuendeleo na kufanya kazi kwa juhudi, maarifa na nidhamu ili tukuze uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, katika wiki hii moja tumekuwa tukijadiliana hapa na kuchambua Mipango yetu na Bajeti yetu ya Serikali. Ningependa tukumbushane kwamba hoja na changamoto zilizojitokeza kwetu sote hapa Bungeni na taifa letu kwa ujumla ni vema tukizifahamu, ili Watanzania tuchukue hatua mahususi za kuwajibika. Uwajibikaji huo hautatosha kama sisi Wabunge tutafikiri ni wa Serikali tu, hapana. Uwajibikaji huu ni wa Serikali, Wabunge, taasisi na asasi zote, wananchi na kila mtu katika kuleta maendeleo yetu. Tumejadiliana, tutakuzaje uchumi wetu, tumejadiliana tutafanyaje uchumi wetu uwe endelevu. Lakini vile vile tumejadiliana tutalindaje mafanikio hayo tuliyokwisha kuyapata. Hapo hapo tukitatua changamoto tulizozungumzia hususan zile za kukuza kilimo chetu. Inawezekana tukafikiria kuwa Tanzania ni hodari kwa kupanga mipango bali udhaifu wetu ni usimamizi na utekelezaji. *(Makofi)*

Lakini lazima nasi kama mawakala wa kuleta maendeleo sisi Wabunge, ni lazima tujiulize kila mmoja wetu, katika ukuaji huu wa uchumi na maendeleo haya kitaifa je, mimi kama Mbunge, nimechangia nini kiuwajibikaji katika kufikia hapa tulipo? Na baadaye tuiulize Serikali, taasisi na asasi zilizopo, wananchi na hatimaye kila mtu

kwamba ni vipi kila mtu amechangia katika kukuza uchumi na kuleta maendeleo katika nchi yetu. Hali hii inahitaji nidhamu ya hali ya juu ya utendaji kazi kama alivyosema Mheshimiwa Balozi Diria, tukiongozwa na *change of altitude* kwa maana ya msimamo sahihi na *the right mindset*. Hivyo ni vitu vya msingi sana kwani Serikali ina wajibu wa kuendeleza mazingira bora ya kuwawezesha wananchi kufanya kazi, amani, usalama na utawala bora wa sheria. Hilo ndilo jukumu la Serikali. (Makofi)

Lakini Mheshimiwa Spika, wananchi pia wana wajibu wa kuchukua umaskini na kuelewa kuwa hakuna atakayetufanyia kazi zetu za kuinua uchumi na huduma za jamii na baadaye akatuandalia sisi tutumie tu. Ni lazima tufanye kazi kwa bidii na juhudi zetu zote na kuelewa kuwa bado sisi tu maskini na tunauchukia umaskini. Mageuzi sasa ya kiuchumi, kisiasa na jamii hayatupasi kuteteleka. Hii *speed* ya sasa ya uchumi (*the global rate*) ya mabadiliko hayatupasi sisi kuteteleka kwani, tukiteteleka tutaachwa nyuma sana. Ndiyo maana uongozi wetu wa uchumi na wa kisiasa ambao unatuhusu sisi sote hapa lazima uzingatie tahadhari hii na sote tuhakikishe kuwa hakuna kurudi nyuma kwa maana ya kwamba *economic and political leadership* lazima ielewe kwamba *there is no rolling back*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ni vema tukakubali kwamba Mipango ya nchi yetu ni mizuri na Serikali inajitahidi kwa uwezo wake wote kusimamia na kuratibu Mipango hiyo. Ushahidi unajionyesha na ushahidi ni mafanikio tunayoyapata kutokana na matokeo tunayopata katika utekelezaji wa vigezo vya uchumi kwa jumla kama Waheshimiwa Wabunge walivyosema hapa ambapo ni kuhusisha ukuaji wa uchumi, kupungua kwa mfumko wa bei, kuongezeka kwa akiba zetu za fedha zetu za kigeni, uboreshaji wa huduma za jamii kama elimu, afya, maji na barabara. Sera zetu za kodi na nchi hii kama isingekuwa na mipango sahihi inayosimamiwa, mafanikio haya katu yasingeonekana hivi sasa.

Kwa hiyo, tunachosema mimi nadhani la msingi hapa ni kuona kwamba yale tunayoyapanga katika kipindi hiki na kijacho tunayasimamia na kuyatekeleza kwa wakati, ukamilifu na kwa mihadi kwa kufanikisha maendeleo ya Watanzania wote. Hii si kazi ya Serikali peke yake, bali ni ya Watanzania wote. Uchumi wetu sasa hivi unakua, Tanzania hivi sasa kwa ukuaji wa uchumi ukilinganisha na nchi za Afrika Mashariki sisi ni namba moja kwa kukua kwa uchumi wetu. (Makofi)

Pamoja na hali hii hata Bajeti yetu ingawaje tunaisema kwamba Bajeti yetu ni tegemezi lakini mwaka wa 2002 tulikuwa tunasema utegemezi wetu umefikia asilimia 47. Leo tunaambiwa kwamba utegemezi wetu utafikia asilimia 41, hiki si kiwango kikubwa ni kidogo lakini kinaonyesha dalili ya kwenda kuondokana na utegemezi. Lakini vile vile niseme kwamba suala lolote la maendeleo, wale wenzetu wazungu wanasema, *development is not an event, development is a process*. Kwa hiyo, kwa mchakato huu nina hakika kwamba tutaendeleza vizuri mipango yetu ya Bajeti ili kukuza uchumi wetu. Lakini vile vile niseme kwamba mipango yetu ni endelevu na haya pia yanaonyesha na kukua kwa Bajeti yetu. Mwaka wa 1995 Bunge hili lilikuwa linazungumzia Bajeti ya takribani labda bilioni 600 hivi.

Lakini leo hii Waziri wa Fedha Mheshimiwa Basil Mramba, ametuambia Bajeti yetu ni trilion 3.4 huko ni kukua kwa Bajeti kunako maanisha kwamba tunaendelea kujenga taifa letu. Aidha lazima tukubali pia uendelevu huu unaonyeshwa na hali ya uchumi tulionao hivi sasa. Mimi nafikiri kwa hili kama alivyosema Mama Getrude Mongella, lazima tujipongeze kwamba tunafanya kazi. Haya ni maendeleo mazuri hata hivyo bado inabidi tujidhatiti na athari zozote ambazo zinaweza kuyumbisha uchumi wetu. *(Makofi)*

Kwa mfano ukame tulioupata mwaka jana 2003 umesumbua sekta ya kilimo. Kilimo kimekuwa kwa asilimia 4, badala ya asilimia 5 mwaka jana na tumetumia fedha nyingi kuagiza chakula nje na mfumuko wa bei unaotokana na chakula umeongezeka kidogo. Mimi nafikiri la msingi hapa baada ya kukumbana na hali hii tunachotaka kukifanya ni kuendelea na juhudi zetu za kujenga uchumi imara ambao utaweza kuhimili mishtuko yoyote inayoweza kutokea. Kwa mfano upandaji wa bei za mafuta, ukame na kadhalika. Kwa maana hiyo, uchumi wetu lazima uwe imara kuji-*adjust* na *stockist disturbances* na *any shocks* ambazo zitaweza kuathiri uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali mipango ya nchi hii sasa tunaendelea vizuri kazi iliyobakia, mafanikio tuliyoyapata tunahitaji kuyalinda na kuyaendeleza na yapo maeneo lazima tuyafanyie kazi. Kwanza ni eneo la kuhakikisha kuwa usimamizi na utekelezaji wa mipango yetu unashirikisha ngazi zote kuanzia ngazi ya kaya hadi ngazi ya taifa. Hili linahitaji kufanyiwa kazi kubwa. Sisi sote katika Bunge hili Tukufu, kama viongozi tuendeleo bila kuchoka kuwahamasisha wananchi na zile hatua tulizokwisha kuziweka za uwezeshaji, tuhakikishe zinatumika na kutoa mafanikio kwa walengwa. Tufanye jitihada za haraka za kuhakikisha kuwa nyanja zote za uwezeshaji zinawafaidisha wananchi, pamoja na mikakati ya kupatikana kwa mikopo kwa wakulima na wafanyakazi. *(Makofi)*

Pili, ipo haja ya kuratibu mipango yetu kama Waheshimiwa Wabunge, walivyosema na kuendeleza dhana shirikishi ili wananchi kule vijijini waweze kuibua fursa za kiuchumi katika maeneo yao, ili tuanze na changamoto ya kupunguza umaskini wa kipato baina ya wakazi wa vijijini na mijini. Ni vema pia mipango yetu ikaandaa mazingira mazuri ya kuimarisha sekta binafsi ambayo sasa ni tegemeo la kukuza uchumi wetu. Mipango itakayowezesha na kuongeza sekta binafsi ni muhimu hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, mimi nakubaliana na ushauri wa Wabunge, kwamba sasa hivi tuendeleze kasi ya uwekezaji kwa wananchi wetu na wawekezaji kutoka nje. Uchumi wowote ambao unakosa kiu ya kuwekezwa mitaji utadumaa na nchi zile ambazo zilikuwa mwanzo zimeanza na siasa za ujamaa, nchi kama China ni nchi ambazo zimefungua milango yao hasa kuitisha wawekezaji kuwekeza kwa viwango vya hali ya juu. Tunaambiwa sasa kiuchumi hivi sasa uchumi wa China umeanza ku- *boil up*. Wachina wanatumia taratibu za kuupoza ili usikue haraka kuliko vile wanavyotaka, lakini ni kwa sababu ya kuwekeza mitaji kutoka Marekani, kutoka Japan, kutoka Ufaransa, kutoka Afrika ya Kusini na na kadhalika.

Hapa nakumbuka kauli aliyosema Mheshimiwa Balazi Ahmed Diria kwamba, kwa nini tumezungukwa na nchi tulizozisaidia katika ukombozi lakini bado hatujazitumia vizuri? Serikali inajaribu kuzitumia vizuri, lakini tuna changamoto ya kuondokana na ile *cultural revolution* ya kuelewa kwamba lazima tubadili mtazamo wetu na fikiri zetu. Mara nyingi tumejikuta tukisema uchumi wetu tunauza nje au tunawapa makaburu. Sasa hali hiyo, ni baadhi ya maeneo ambayo inabidi tuyafanyie kazi ili tuchukue fursa hizo.

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri kazi kubwa ambayo tunatakiwa kuifanya sasa ni kupunguza urasimu katika maamuzi yetu juu ya mipango ya kukuza uchumi katika uwekezaji ili kupunguza gharama za wawekezaji tukuze uchumi wetu. Tunapokuwa na urasimu mkubwa katika masuala ya kuendeleza uchumi hasa katika ile ya kuvutia ya kuvutia mitaji, Tanzania siyo nchi pekee ambayo wawekezaji hawa wanataka kuja, ziko nchi nyingi. Sasa tukipunguza urasimu huu kwa vyovyote sisi kama wakala wa maendeleo kama Wabunge, tutasaidia sana Serikali kuweza kuwaitisha wawekezaji hao na kuwekeza na kukuza uchumi wetu. Lakini vile vile tunapozungumzia wawekezaji tuisahau kuwa hata mkulima wetu kule kijijini naye vile vile ni mwekezaji. Kwa hiyo, lazima tumboreshe zaidi.

Mheshimiwa Spika, mimi naelewa katika lengo hili tumepiga hatua. Kituo chetu cha Uwekezaji (*Tanzania Investment Center*) kutokana na utafiti uliofanywa mwaka 2003, kimetoa matokeo kwamba katika nchi zote za ukanda wa Afrika Mashariki zikijumuisha Somalia, Ethiopia, Eritria, Sudan, Uganda na Kenya Kituo chetu ndicho kituo bora sana kwa utaratibu wake kwa kuvutia wawekezaji. Hili kwa kweli ni lazima tujipongeze sisi wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kwa mfano Dr. William Shija, alizungumzia kwamba hii dira yetu ya maendeleo mbona haeleweki. Lakini mimi napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa mipango yetu ya muda mfupi na wa kati tuliouweka pamoja na mkakati wa kupunguza umaskini ambao tumekuwa tukiuzungumzia karibu wiki moja hii, sasa yote inasaidiana na utekelezaji wa dira yetu ya maendeleo ya 2025. Ni kweli kwamba bado tunahitaji kuimarisha ushirikisho wa maeneo yote katika utekelezaji wa mipango yetu, lakini mageuzi tunayoendelea nayo sasa hivi kwa maana katika Serikali Kuu, katika sekta zetu na yale ya kutoa uwezo kwa Serikali za Mikoa, Wilaya na Mitaa, hadi vijijini ni mwelekeo wa kufikisha azma hiyo. Mimi nafikiri mambo mazuri yanakwenda kwa hatua, hekima na busara. Hivyo sote tukishirikiana mimi nina hakika kabisa uchumi wa Taifa letu utaendelea kukua kwa kasi kubwa tukiwa na nidhamu ya hali ya juu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, zipo hoja ambazo zimegusiwa na baadhi ya Wabunge, nakumbuka Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, wamesema kwamba hali za Watanzania ni duni na hazibadiliki. Mimi nadhani hoja hii si sahihi kwa jinsi ilivyo, si sahihi hata kidogo. Tumeshafanya maboresho katika maeneo mengi, tumefanya maboresho katika elimu, wananchi sasa wana nafasi watoto kwenda shule kusoma si kama zamani. Tumefanya maboresho katika maeneo mengi, katika afya, maji, barabara, mawasiliano na upatikanaji wa bidhaa muhimu kupitia viwanda vyetu ambavyo hapo mwanzo hali haikuwa hivyo. Lakini vile vile kama tulivyosema utaratibu

wa Serikali hii wa kuanzisha tena elimu ya sekondari, kama tulivyofanya elimu ya msingi itatoa fursa kubwa hata kuondoa zile tofauti kwamba ni mikoa gani imesomesha zaidi kuliko mikoa mingine. Yote hiyo ni uwezeshaji ambao tumesema kwa kwa kweli hali bora hatuwezi kusema hazibadiliki.

Mimi naweza kusema kwa mfano kupitia ubinafsishaji mashamba kwa mfano ya tumbaku, miwa na chai wananchi wengi vijijini wanaendelea kukuza kipato chao. Nitatoa mfano, nilikwenda Kilombero kwa Mheshimiwa Christopher Wegga, nilikuta wakulima wenyewe wakinieleza kwamba msimu uliopita wao kama wakulima wadogo wadogo wa miwa wameingiza shilingi bilioni 8. Hawa ni wakulima wenyewe wanasema. Katika kipindi hiki kinachokuja wananchi wa vijijini wanatarajia kuingiza takribani shilingi bilioni 15. Sasa yote haya ni matokeo ambayo yametokana na urekebishaji wa uchumi wetu na hiyo ni sawia kule Katumba Mwakaleli, kwenye viwanda vya chai, hiyo ni sawia katika maeneo ya Urambo wanakolima tumbaku. Wakulima sasa wanaendelea kuongeza mapato yao. Nimesema *development is not an event, it is a process*. Sasa ni lazima tuelewe kwamba tunapozungumzia maendeleo ni lazima twende hatua kwa hatua. Pia Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, alitoa takwimu za kuonyesha kwamba pato la Taifa la Mtanzania linashuka. Mimi napenda kusema kwamba pato la wastani la Mtanzania, limekuwa likiongezeka kila mwaka tangu mwaka 1995 hadi mwaka jana 2003.

Katika mwaka wa 1995 pato la wastani la Mtanzania lilikuwa ni shilingi 101,696 kwa bei za miaka husika na kuendelea kuongezeka hadi kufikia shilingi 286,000 mwaka 2003 kwa bei za mwaka husika. Upimaji wa pato la wastani *per capital income* unafanywa kwa kutumia pato la taifa kwa bei za miaka husika na wala siyo kwa bei za miaka ya nyuma *constant prices* kama alivyobainisha Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed. Upimaji huu unakuwa linganifu kimataifa na unatumia na mashirika na taasisi zote za kimataifa. Sasa kwa kutumia *constant prices* labda kwa sababu zinaonyesha *haziku-take into account exchange rates*, thamani ya fedha labda Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, alitaka aone kwamba kwa kweli pato la wastani la Mtanzania halijaendelea na kumbe si sahihi. Lakini hapa tulipofikia hatusemi kwamba ni pato ambalo kwa kweli Mtanzania anaweza kupata, ni lazima tukazane na jitihada zetu za kuongeza uchumi ili tuhakikishe kuwa pato la taifa la Mtanzania linaendelea. Kama alivyosema Mheshimiwa Profesa Mbilinyi na Wabunge wengine wengi katika Bunge letu hili, tumekuwa tukizungumzia kuhusu madini ya dhahabu ambayo yanahusisha takribani migodi minne iliyoanza kuzalisha hivi karibuni na mimi naelewa wazi Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Waziri wa Nishati na Madini watakuja kuelezea zaidi. Lakini nchi kama Ghana, Afrika Kusini na Zimbabwe tunaolewa kwamba zimeendelea kutegemea sekta hii sasa kwa zaidi ya miaka 100. Sasa ni vema hapa tukaweka rekodi sahihi ili kuondokana na dhana ambayo imekuwa ikishereheshwa mara kwa mara ambayo si sahihi kwamba sisi katika mapato yetu ya dhahabu kila tunachozalisha tunapata asilimia tatu tu inayoitwa mrabaha.

Mimi ningependa niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge wenzangu warejee kitabu cha hotuba ya Bajeti ya waziri wa Nishati na Madini aliyoitoa mwaka jana ambayo alionyesha ulinganisho wa nchi zote duniani zinazozalisha dhahabu na kuonyesha

kwamba mrahaba ule ni kiasi gani, kwa bahati nzuri ninao ulinganisho huo Argentina asilimia 3, Bolivia, asilimia 1 mpaka 5, Brazil asilimia 1, Colombia asilimia 4, Mongolia asilimia 2.5 nadhani taarifa zote hizi tunazo katika kitabu chetu cha hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini ya mwaka jana kwenye *hansard*. Tukiangalia inaonekana kabisa kwamba Tanzania hatupati asilimia tatu tu, kwa sababu pamoja na asilimia 3 ya mrahaba tusingahau kuna kodi, kuna *income tax, exercise duty, kuna with holding taxes*, zote zimeainishwa vizuri katika *document* ile aliyotoa Waziri wa Nishati na Madini. Sasa sisi Waheshimiwa Wabunge, kama mawakala wa maendeleo tunapokuwa tukizungumzia kwamba madini tunachopata ni asilimia 3 na asilimia 97 zinatoka nje hapo tutakuwa hatutoi takwimu sahihi kwa wale wanaotusikia.

Mimi nitatoa mfano kwa upande wa Tanzania kwa mfano kwa kila dola moja ya Marekani, tunapata asilimia 12, asilimia 2 inakwenda kwa miradi ya jamii, asilimia 15 ni mikopo ya benki, asilimia 12 ni gawio, asilimia 59 ni bidhaa zinazotumika kuendesha migodi, ambazo kati ya hizo asilimia 52 zinatumiwa hapa nchini na asilimia 48 kwa huduma toka nchi za nje. Lakini vile vile kodi ya mapato ni karibu asilimia 30. Sasa kama kuna utaratibu mwingine wa kuboresha sekta hii ya madini Serikali ya CCM ni Serikali sikivu. Kama mawazo yanatolewa na Waheshimiwa Wabunge na ninaelewa kuna tume imeundwa inafuatilia suala hilo, nina hakika tutafikia mahali Bungeni, hapa hapa tutaelezana taratibu za kutumia migodi yetu ya madini ambayo imeanza kwa miaka 4, 5 hii mikubwa ukilinganisha na miaka 100 kwa migodi kama ile ya Ubuwasi ya kule Ghana, *100 years* sasa hilo nadhani tusingahau taarifa hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge tu wametoa changamoto ya kukuza bidhaa zetu nje na sisi hilo tunakubaliana nalo sana. Kwa mfano katika kipindi hiki tumesema ongezeko la bidhaa zetu nje zilikuwa ni asilimia 26, wakati zile tuliloagiza kutoka nje zilikuwa asilimia 30. Mimi naelewa kwamba kwa kweli utaratibu huu hauwezi kuimarisha thamani ya sarafu yetu. Tunachohitaji kufanya ni lazima tuongeze uzalishaji wa bidhaa zetu nje na ndiyo maana sasa hivi tujitahidi na mikakati yote ya kuboresha usindikaji, viwanda vinavyosindikiza mazao yetu kama korosho, chai, pamba, tumbaku, lazima tukazane na *agro - processing*. Lakini vile vile ni lazima tufanye utaratibu makini wa kuendeleza *export processing zones* ili tuweze kuongeza uuzaji wa bidhaa zetu nje. Lakini la msingi lazima tuongeze uboreshaji katika sekta ya utalii, kilimo kama tulivyokuwa tunazungumzia hapa, mifugo hata sekta ya uwindaji.

Mheshimiwa Spika, suala lingine lilijitokeza ni lile la kusema dira ya maendeleo ya 2025 bado halijaeleweka. Lakini tukumbuke kuwa Serikali iliandaa semina nyingi. Hata Waheshimiwa Wabunge hapa, tulipata semina hizo na Mheshimiwa Dr. William Shija, alikiri hilo. Aidha utayarishaji wa dira husika umehusisha wadau mbalimbali na kuzingatia ngazi zote za utawala. Tatizo lililopo ni lile lililoguswa kuwa ni udhaifu wa ufuatiliaji, usimamizi wa utekelezaji. Mimi nimesema kwamba kazi hii si ya Serikali peke yake, kazi hii ni ya Watanzania wote kuwajibika kila sehemu Mtanzania alipo. Mipango na mikakati tuliyojiwekea hususan ya kupunguza umaskini ni mizuri wala hatuna haja ya kuihuisha. Suala la msingi ni *seriousness* yetu, nidhamu yetu na mihadi yetu katika kufanya kazi kwa bidii, kuwajibika kwa kufikia malengo yetu. Mimi nina hakika kabisa kufikia malengo yetu. Mimi nina hakika kabisa nchi zile zilizoendelea sasa

hivi mapinduzi makubwa waliyoyafanya kwanza ni nidhamu katika kufanya kazi na pili kuhakikisha kwamba maeneo tunapofanyia kazi tunafanya kazi kwa bidii ili kutoa matokeo mazuri.

Uzoefu wa kiuchumi lazima sasa uanze kutufundisha mambo mengi sana. Mimi nasema kwamba uzoefu wa kiuchumi *economic experience* unatufundisha kuwa maendeleo ya uchumi na kukua kwa uchumi sisi kama *development agents* sisi Wabunge ni lazima tuyathamini na kuyapima tukirejea hali halisi na tathmini kwa kuangalia *the real situation*.

Tusiyathamini na kuyapima kwa kuangalia hali ya kufikirika, *the ideal situation*. Lazima tulinganishe kati ya *real* na *ideal situation*, na hili kama alivyosema Mheshimiwa Mwanri. Kwa sababu hatuwezi kuzungumzia suala la kujilinganisha Tanzania katika kukuza uchumi na nchi kama Marekani tukaona kwamba ile ni *ideal situation* kwa kweli tutaona kama ni Wafalme Njozi.

Lazima tuangalie matatizo yetu, tuyatatie, tuyatatumie tujue tunayatatuliaje ufumbuzi kama tulivyofanya katika sekta ya elimu, tumesema watoto wetu hawasomi, sasa mimi nafikiria kwamba kama sasa tukianza teknolojia ya kufundisha watoto jinsi ya kwenda mathalani kwenye *exploration* ya mwezi tutakuwa tunapoteza wakati. Ni lazima tuhakikishe kwamba tuna-*deal* na *real situation*, na tutakapo-*deal* na *real situation* kama *development agent* hatutakata tamaa.

Lakini tuki-*deal* na *ideal situation* tunaweza tukajikuta tukizungumzia mapungufu ambayo kwa kweli yatatufanya tusahau mafanikio ambayo tumekwisha kuyapata. Lakini lazima niseme kwamba tukijilinganisha na nchi nyingi duniani na hizi za Afrika ambazo zimefanya *practical transformation* katika mifumo ya kiuchumi, sisi hasa hasa tuna miaka 14 tu. Tulianza mwaka wa 90.

Hivyo nafikiri kwa mafanikio tuliyoyapata ni lazima tujipongeze pamoja na sisi Wabunge tulivyoshirikiana na wananchi wetu katika majimbo yetu kubadilisha hali yao. Niseme hata hivyo kwamba hata katika nchi zinazoendelea uchumi wao siyo *perfect* kwa asilimia 100. Na tunavyoshauriana hapa Bungeni sote lazima tuelewe kuwa kama nilivyosema mwanzoni maendeleo si tukio bali ni mchakato. Mwaka 2002 kama nilivyosema Tanzania ilikuwa ya tatu kukuza uchumi katika nchi ya *SADC*, leo hii pamoja na *economic shocks* tulizozipata tumekuwa wa kwanza katika Afrika Mashariki. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tunashuhudia nchi kadhaa zikiungana kiuchumi, licha ya kwamba zimeshaendelea na kasi yao ya maendeleo ni kubwa. Kuna Jumuiya za Nchi ya Ulaya, Jumuiya za Nchi ya Mashariki ya Mbali. Siyo kwamba hazina matatizo. Lakini zinaungana huko zikiendelea kutatua matatizo hayo. Nasema hivi kwa sababu katika mchango ya Waheshimiwa Wabunge, limejitokeza suala la Muungano. Mimi nasema kwamba yale maeneo ya Muungano yanayokwamisha kukua kwa uchumi wetu lazima tuyafanyie kazi. Uchumi wa Zanzibar ni wa Tanzania Bara na wa Tanzania Bara ni wa Zanzibar. Azma hii ndiyo itakayotupa mafanikio wakati tunaendelea na taratibu



zetu za kufanya kazi katika *SADC, East African Co-operation, NEPAD* na Afrika kwa jumla. *NEPAD* ambayo tayari sasa hivi tumekwisha *review* tumekubali kuingia kwenye ile *African Pier Review Mechanism*. Tunachongojea ni karatasi hiyo kuletwa Bungeni ili wote tuiridhie tuendelee kufanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tumezungumzia tatizo la rushwa. Tatizo la rushwa ni tatizo ambalo ni la zamani na zee kama historia yenyewe. *It is old as history itself*. Rushwa ina majina mengi, wengine wanaita *kickbacks*, wengine wanaita bakshishi, wengine wanaita mlungula na kadhalika.

Sasa kulipigia kwetu kelele sisi Wabunge ni alama tosha kuwa tunachukia rushwa, kwa lazima tuipigie kelele, hatuwezi kunyamaza tu. Serikali imesambaza Vituo vya *PCB* hadi Wilayani. Wako kadhaa kama tulivyosikia jana wameshawajibishwa na kuchukuliwa hatua kwa ajili ya rushwa. Dola inafuatilia suala hili kwa karibu sana. Hatua hizo za Serikali tutaendelea nazo kama ilivyobainishwa katika hotuba zetu zote za Bajeti.

Lakini vile vile pamoja na taarifa nzuri iliyotolewa hapa Bungeni na Mheshimiwa Masilingi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Utawala Bora. Hivi sasa kampeni zinazoendeshwa nchini zimehamasisha sana wananchi kuchukia rushwa. Tuendelee na utaratibu huu wa kupiga kelele kuipigia kelele dhambi hii. Ziko nchi nyingine wala hazithubutu kupiga kelele ya tatizo hili kama tulivyolizungumzia hapa. Hili ni changamoto la kila mtu na tusikate tamaa tuendelee kila siku kulikemea.

Mheshimiwa Spika, tulipokuja kwenye marekebisho ya uchumi tumesema kwamba hoja ya kwanza ya kufanya ni lazima tuweke vyema misingi ya uchumi jumla *Macro Economic Fundamentals* na tutakapoweka *Macro Economic Fundamentals* katika hali mzuri ndiyo ishara ya kwanza ya kusaidia kupunguza tatizo la kupunguza umaskini. Na mara mnapomaliza kuboresha vigezo vya uchumi jumla ndipo mtakaweza kuanza kazi ya kuondoka *from the macro level to the micro level* kutoa mafanikio ya uchumi jumla kuiatiririsha vijijini. Serikali imeahidi hili na uamzi wa kuwaweza Watanzania kwa vitendo tayari umekwishaanza na umekwishatekelezwa tokea Bajeti ya mwaka jana 2003. Na ninayo furaha kusema Bajeti ya safari hii vile vile aliyoitoa Waziri wa Fedha imeendelea kuimarisha azma hiyo kwa Serikali.

Kwanza, utaratibu wa kuwapunguzia mzigo mkubwa wananchi, kupitia ruzuku za mbolea. Ufutaji wa ada za shule, ufutaji wa kodi mbalimbali ambazo zilikuwa ni kero zinawawezesha wananchi kuongeza mapato yao wanayopata kutokana na kazi wanazofanya.

Pili, Bajeti ya mwaka huu ya kufuta kodi na ushuru mbalimbali katika maeneo ya kilimo, mifugo na uvuvi, ni hatua muhimu ya kuwawezesha wananchi.

Tatu, utaratibu wa kuondoa ada za leseni katika eneo ambalo linawagusa wafanya biashara wengi wa vipato vya chini na vya kati vitasaidia sana kuwawezesha wanawake na wanaume walio wengi wanajihusisha katika shughuli za biashara ndogo na za kati.

Nne, uanzishwaji wa mifuko mbalimbali. Udhamini wa wakulima wadogo, azma ya Serikali ya kuanzisha Benki ya Kilimo na ile ya Viwanda, ni mikakati sahihi ya uwezesaji pamoja na hamasa ya kuanzisha vyama vya ushirika na vile vya kuweka na kukopa.

Tano, mkakati wa makusudi kama nilivyosema mwanzoni wa kuboresha elimu ya msingi, elimu ya sekondari moja kwa moja ni mpango wa uwezesaji kupitia maendeleo ya rasimali watu. Yote haya yanaendena na mipango tunayopanga ili kuinua uchumi wetu.

Kwa wale wataalam Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge nchini na duniani kote hivi sasa wanaelewa kuwa lile lengo letu la kupenyeshwa mafanikio yapatikanayo katika uchumi jumla kuyafikisha kwa wananchi vijijini sasa tunaanza kuyafanyia kazi kwa sababu suala hili linakwenda hatua kwa hatua. Lakini katika kipindi hiki ambacho mafaniko ya uchumi jumla yanatiririka kwenda vijijini ipo haja ya kujenga tabia ya umakini *seriousness* na nidhamu ya kila mmoja wetu tufanye kazi kwa jitihada zote.

Mafanikio ya kufikia ngazi za chini si *automatic* si sadaka au au msaada. Ni lazima sisi wenyewe tuvifanyie kazi. Kwa sababu maendeleo kama nilivyosema narudia tena ni mchakato na hili limeshauriwa sana na Waheshimiwa Wabunge hapa Bungeni. Mkakati huu utatuwezesha kutekeleza kikamilifu yale tuliyopanga na kuamua. Ni muhimu sasa twende katika maeneo yetu tukashirikiane na wananchi kuwaelezea mkakati huu muhimu.

Mheshimiwa Spika, ushauri wote uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge kama nilivyosema sisi Serikali tumeupokea. Ni kweli iko haja ya makusudi ya kuangalia utendaji wetu katika Sekta ya Kilimo. Ipo haja ya makusudi ya kukifanya kilimo kiwe ni kazi ya kuvutia. Maeneo yanayolenga katika kupunguza mzigo wa wakulima tuyafanyie kazi. Suala la pembejeo kama mbolea na zana bora, ni vema zikapatikana kwa wakati na kwa walengwa wenyewe. Uratibu wa pembejeo hizi tukijitahidi kuboresha kufika kwake Mikoani hadi kwenye Halmashauri za Wilaya badala ya Mawakala zinaweza sana zikapunguza gharama za wakulima na aidha hatua zitakazochukuliwa na Serikali kupitia Wizara ya Fedha zitakuwa na matokeo mazuri. Hili ni eneo ambalo inabidi tulifanyie kazi. Inabidi tusingitize uratibu wa masoko na usafiri ili kilimo kifaidike. Kilimo chetu ni lazima kipangiwe mkakati wa kuvutia wakulima wadogo na wale wakubwa ili wavutiwe na Sekta hii. (*Makofi*)

Pamoja na kuendeleza uboreshaji katika usindikaji wa mazao yetu kama vile korosho, katani, kahawa, pamba na mazao yaliyo asilia, mimi nina hakika kabisa kilimo chetu kitakuwa ni cha kuvutia. Aidha, eneo la umwagiliaji sasa tutalitafutia ufumbuzi wa karibu ili kupanga fedha zetu katika maeneo yatakayoleta *impact* badala ya kusambaza fedha hizi kidogo katika maeneo kadhaa wa kadhaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni lile la kuendeleza huduma za jamii. Uendelezaji wa huduma za jamii ni eneo muhimu sana la kupunguza umaskini usio wa kipato. Juhudi za Serikali hivi sasa za kuboresha elimu nchi nzima kwa mwaka ujao wa fedha shule za sekondari sio tu zitapunguza umaskini wa kipato vile vile itapunguza tofauti ambazo nimekuwa nikizielezea.

Mheshimiwa Spika, uradishaji na uendelezaji wa raslimali watu *human capital investment* ndiyo uliosaidia sana nchi kama Japan, Malaysia, Korea ya Kusini, India na kadhalika. Sasa hatua hizi sasa ni bora nasi tukaziingiza kwa nguvu zaidi. Lakini vile vile kuendeleza teknolojia ya habari na mawasiliano ambazo ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la maendeleo sio *sterile type* tunasema kwamba siyo lelemama suala la maendeleo. Linahitaji mihadi ya kina *commitment*. Uboreshaji wa miundombinu ya barabara unaoendelea sasa hivi utasaidia kukuza uchumi wetu. Aidha, tutakavyoendelea na uboreshaji wa miundombinu ya nishati kwa miradi kama vile Mradi wa Mchuchuma na matumizi mazuri ya gesi yetu ya Songosongo nina uhakika uchumi wetu utabadilika. Hivi sasa mapato ya Serikali yameongezeka kama tulivyosikia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na mipangilio yetu ni *forecast*. Tunachotaka kukifanya sasa ni kukazana na ufuatiaji na usimamizi na utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hoja zote zilizoulizwa na Waheshimiwa Wabunge tumezijiibu na *sectoral presentation* Wizara zitakapotoa hotuba zao nina hakika zitagusia kwa kina maeneo hayo. Tutaendelea kupanga, kuratibu, kuhimiza ufuatiliaji na utekelezaji ili yote tuliyoyapanga tuyatekeleze kwa uwezo wetu wote sisi sote na kila mtu kama Mtanzania. Tumeshanza kuimarisha vigezo vya uchumi kwa jumla. Tumekwishanza kutiririsha mafanikio ya uchumi kwa jumla huko vijijini, tukianza na kupambana na umaskini usio wa kipato. Tumeanza hatua kwa hatua sasa tokea Bajeti iliyopita kuanzisha mikakati ya uwezeshaji wa wananchi katika ngazi zote ili wawe kuibua fursa za kiuchumi zilizopo katika maeneo yetu kama nilivyokwishaeleza.

Nini la msingi basi, tukubali tuna changamoto za kupambana nazo. Lakini hapo hapo tukubali kuwa mafanikio tuliyoyapata chini ya Serikali ya Chama Cha Mapinduzi lazima tuyaonyeshe, tuyazungumze, kuyatetea na kuyaeleza bila woga. *(Makofi)*

Tusipofanya hivyo, hakuna atakayetufanyia kazi hii. Haijapata kutokea duniani popote pale kwa nchi yoyote isiyo na mipango mizuri na Bajeti nzuri halafu nchi hiyo ikazungumzwa dunia nzima kwamba uchumi wake unakuwa, mfumko wa bei unashuka. Mashule yanajengwa, akiba ya fedha za kigeni zinaongezeka, uwekezaji unaongezeka. Hiyo kwa kweli haijapata kutokea. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wenzangu, nawaombeni Mipango na Bajeti hii tuliyoandaa kwa mwaka huu ujao nyote muiunge mkono. *(Makofi)*

Hii Bajeti ya kiitikadi, hii ni Bajeti ya kusaidia Watanzania wote kwa jumla kuwawezesha kuingia katika mkondo wa kuibua uchumi wao. Suala la msingi ni kukuza

na kuendeleza uchumi wetu kwa nidhamu ya hali ya juu na kufanya kazi kwa bidii, maarifa na akili.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):**  
Mheshimiwa Spika, kwanza kabla sijaendelea na kufafanua baadhi ya hoja kwanza niseme moja kwa moja kwamba naunga mkono hoja zote mbili asilimia mia moja. *(Makofi)*

Pili na mimi kwa sababu ni mara yangu ya mwanzo kusimama hapa napenda kuwapa pole ndugu zangu Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda kwa kufiwa na baba yao mzazi na Mungu awape moyo wa subira na vile vile ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. Pia nampa pole Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, kwa kufiwa na mwanaye naye vile vile Mungu ampe subira na ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi.

Pia nawapa pole wale waliopata maafa mbalimbali, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere na Mheshimiwa Kilasi. Baada ya hayo napenda pia na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge kuwapongeza Waheshimiwa Mongella, Mheshimiwa Dr. William Shija, Mheshimiwa Athuman Janguo na Mheshimiwa Remidius Kissassi kwa kuchaguliwa kuwa *Member* wa Bunge la Afrika Mashariki na hasa Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, kwa kuwa Rais wa kwanza wa Bunge la Afrika. *(Makofi)*

Pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Sophia Simba kwa kuchaguliwa kuwa *Member* wa *SADC*. Sasa naenda moja kwa moja kufafanua badhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Nikianzia na hoja ya Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, inayozungumzia juu ya utaratibu wa *Cash Budget* kwamba unaathiri utekelezaji wa Bajeti na hivyo ungefutwa.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa *Cash Budget* umeendelea kutumika kama ni chombo muhimu cha kudhibiti Bajeti na matumizi ya Serikali. Tangu utaratibu huu utumike kumekuwepo na ufanisi mkubwa katika nidhamu ya matumizi na usimamizi wa fedha kwa ujumla. Hali ya sasa imekuwa tofauti sana na huko nyuma ambapo Serikali ilikuwa inatumia fedha zaidi ya mapato yake na hivyo kusababisha athari kubwa katika uchumi wa Taifa. Sasa hivi tunatumia kulingana na kile tulichonacho. Kutokana na usahihi mzuri wa mapato ya ndani na wafadhili kutoa sehemu kubwa ya misaada yao mapema, Wizara, Idara, Mikoa na Serikali za Mitaa, zimekuwa zikipatiwa mgao kwa mujibu wa Bajeti zao.

Aidha, pamoja na kutumia *Cash Budgeting* bado Serikali imeendelea kutoa kipaumbele kwa sekta za kuondoa umaskini. Sekta za kuondoa umaskini zimekuwa zikitengewa fedha kwa kila robo mwaka kulingana na mahitaji na taarifa za utekelezaji kwa kila robo iliyopita na kwa upande wa fedha za maendeleo hali ni kama hivyo. Hivyo

utaratibu wa *Cash Budgeting* hauna athari yoyote iwapo fedha zitatolewa kulingana na mpango wa utekelezaji, yaani kulingana na *action plan* tuliyokuwa nayo.

Kulikuwa na hoja juu ya usalama wa *National Payment System* iliyopo hivi sasa. Kama ilivyoelezwa ndani ya Ripoti ya Sera ya fedha za Benki Kuu ambayo nadhani Waheshimiwa Wabunge wengi wameisoma kwamba kuanzia tarehe 8 Aprili, mwaka huu mfumo mpya wa malipo yaani *Tanzania Inter-Bank System (TIS)* ilizinduliwa.

Mfumo huu wa kompyuta hufanya malipo yote ya fedha yafanywe papo kwa papo *within two hours* mtu mmoja au mteja mmoja anataka kulipa fedha Benki fulani au Taasisi fulani, unapeleka *system* hii *within two hours* fedha zile zinamfikia aliyehusika. Na kuna baadhi ya benki ambazo zimejiandikisha kwenye mpango huu. Kwa hivyo, sasa hivi hakuna tofauti kwamba fedha utazipeleka na zikae wiki nzima au wiki tatu.

Kuhusu hoja ya Bandari ya Pemba kutangaza kuwa ya kimataifa. Wizara ya Fedha imeshachukua hatua hiyo na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inavyojua kwamba bandari ya Mkoani Pemba sasa ni bandari ya kimataifa kuanzia *Government Notice* ya tarehe 1, mwaka jana 2003. (*Makofi*)

Kilichosalia hivi sasa ni utekelezaji wa Ofisi ya Bandari ya Zanzibar ili Bandari iwe ya kimataifa lazima iwe na uzio na bandari husika itoe vifaa vinavyotakikana ili kuhakikisha kwamba kuna usalama wa vyombo vyote vinavyoingia pale. Mojawapo ni uzio. Banda la karafuu kwa mfano Pemba na kuendelea huko mbele kuendelea upande wa Kusini na Kaskazini lazima yote iwekwe uzio na Ofisi ya Bandari ya Zanzibar ili bandari hiyo sasa hivi iweze kutumika kama bandari ya kimataifa. Kwa hivyo, lililobakia ni jukumu la *Port and Marine of Zanzibar* kukamilisha taratibu zilizosalia kuwa bandari hiyo itumike kama bandari ya kimataifa.

Hoja ya kuhusu kero kwa wafanya biashara wa Zanzibar. Namhakikishia Mheshimiwa Haroub, kwamba mimi nina ndevu, nitajulikana haraka. Lakini ninakuhakikishieni nikimvisha buibui yeye na viatu vya mchuchumio na mimi nikapiga kanzu na kilemba, kama nimefuatanana naye basi tutakuwa tumejigeuza vizuri sana. Na atakapofika pale itajulikana kwamba sio Abdisalaam wala si Haroub, pengine ni Haruba na Mohamed. Ili tuyaone hayo. Niko tayari, wala hakuna ulazima wa kwenda yeye na Waziri wangu na Naibu Waziri mwenzangu. Nitakwenda mimi na yeye kwa sababu tunaweza tukaongea lugha ile ile ambayo inafahamika na watumishi wa pale. (*Makofi*)

Ninachotaka kusema ni kwamba kuanzia tarehe 1 Julai, mwaka jana kwa makusudi na nilisema hapa Bungeni kwamba *TRA* kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara Zanzibar na wafanyabiashara wa Zanzibar walikutana wakaunda Kamati ya kutatua matatizo yao mbalimbali kuhusu biashara na mambo ya ushuru na mengineyo ya maendeleo kwa wafanya biashara wa Zanzibar na kwa Zanzibar kwa jumla. Walijiwekea wakutane kila baada ya miezi mitatu, kushauriana na kutoa mikakati iende namna gani ili kuondosha sulubu au yale yote waliyofanyiwa ambayo hayapendezi katika kufanikisha shughuli yao ya biashara.

Kamati hiyo imekutana mwezi wa *October, 2003* na mwezi Januari, 2004 mwaka huu na kwa hivyo matatizo yale yote wanayoyapata bado na ufumbuzi ambao umepatikana utakuwa wao wameshazungumza na *TRA* pamoja na Waziri wa Biashara wa Zanzibar, ambaye yupo hapa kama ni Mbunge na anashirikiana kabisa na Kamati hii kwa hivyo kama tatizo hili bado lilikuwepo nadhani na nina imani kwamba Serikali au Wizara ya Fedha ingelikwishajua na mkakati gani uchukuliwe kutokana na Kamati hiyo ambayo Waziri mwenyewe wa Biashara Zanzibar anashughulikia. (*Makofi*)

Kulikuwa na hoja juu ya kiwango cha utegemezi wa Bajeti na mara nyingi tumezungumza hapa na tumesema kwamba Bajeti yetu kuna utegemezi wa asilimia 41. Naomba nitoe ufafanuzi 41 inapatikanaje asilimia hii.

Katika Bajeti hii ya 2004/2005 misaada kutoka nje ni asilimia 23. Mikopo kutoka nje asilimia 18 ndiyo inafanya jumla asilimia 41. Hivyo utaona utegemezi wetu wa Bajeti hii ni asilimia 23 ambayo tunapata kama ni misaada. Kwa sababu sehemu ile tunaipata kama ni mkopo ni fedha yetu ambayo itabidi sisi tuilipe baadaye. Kwa hivyo, ukitazama haya hali halisi ya utegemezi ni asilimia 23 badala ya asilimia 41. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja kuhusu mpango wa kadhamini mikopo kwa wafanya biashara ndogo ndogo na za kati. Wakati Mheshimiwa Waziri wa Fedha akiwasilisha Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2003/2004 alielezea azma ya Serikali kuanzisha utaratibu wa dhamana kwa mikopo ya wafanya biashara ndogo ndogo na za kati. Baada ya kupata ridhaa ya Bunge, Serikali ilikamilisha maandalizi ya Kanuni na mwongozo wa mfuko huo na pia makubaliano na Benki Kuu kwa ajili ya uendeshaji wa mfuko.

Hii imefanywa makusudi kwa sababu hili ni jambo jipya kwa kweli. Kulichukua kwa haraka haraka lingeweza kutuletea matatizo na baadaye tukaanza kutatua matatizo hayo.

Lakini *right from the very beginning* ni muhimu kwanza kuhakikisha linakuja kwa mpango ulio madhubuti na kama baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walivyotushauri hapa tumeona kwamba ili kutumia fursa hii kikamilifu, wafanya biashara wadogo wadogo na wa kati wanashauriwa kujiunga na vyama vya ushirika na vya kuweka na kukopa yaani *SACCOS* na *SACCAS* na *NGOs* ambavyo vitaweza kufuatilia hii mikopo na kisha kuwakopesha wanachama na kwamba hii benki iwe inawakopesha, hizi *SACCOS* *SACCAS*, *NGOs* na siyo kukopesha mtu mmoja mmoja au mfanyabiashara mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja kwamba kuwavutia wawekezaji kukopa kutoka katika vyombo vya fedha vya ndani ya nchi, Serikali inatambua msingi wa malalamiko ambayo yamekuwa yakitolewa dhidi ya vyombo vya fedha ya kutotoa mikopo hasa kwa sekta ya kilimo. Serikali imekuwa ikichukua hatua kadhaa ili kuviwezesha vyombo hivi kutoa mikopo na baadhi ya hatua zinachukuliwa ni pamoja na

Kwanza, kuanzishwa kwa soko la mitaji pamoja na kuingiza Hati fungati za Serikali katika soko hilo.

Pili, kufanyia marekebisho Sheria ya Ardhi ili kuwezesha itumike kama dhamana.

Tatu, kuanzishwa kwa Mahakama ya Biashara ili kurahisha utatuzi wa mashauri ya kibiashara. Mategemeo yetu mategemeo ya Serikali ni kuwa baadhi ya hatua hizo pamoja na mwenendo mzuri wa uchumi jumla, viwango vya riba kwa mikopo vitashuka na hivyo kuyashawishi makampuni kukopa kutoka vyombo vya fedha vya ndani.

Takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa mikopo kwa sekta binafsi katika miaka ya hivi karibuni imekuwa ikiongezeka kama ilivyothibitishwa na ongezeko la 41.8% katika mwaka 2003.

Kulikuwa na hoja juu ya mgao wa fedha kwa *Tanzania Education Authority*. Ni kweli sheria inasema kiwango kiwe 2% kwa Bajeti 2% ni sawa na Sh. 200 bilioni. Keki tuliyokuwa nayo ni ndogo na uwezo nao ni mdogo tumeweza kutoa kiasi hicho kama Bajeti inavyoturuhusu. Ni sheria, hata sheria ya Vyama vya Siasa ina kiwango kwamba asilimia isiyozidi 2 ya mapato yote lakini hatuwezi kufikia hiyo na hata ile 1% vile vile hatujaipata tunatoa kwa mujibu wa fedha zinavyoturuhusu. Kwa hiyo, hakuna haja ya kubadilisha sheria kuhusiana na jambo hili.

Mheshimiwa Spika, vivyo hivyo kuhusu fedha kwa ajili ya Taasisi za Taaluma ambazo hazitoshelezi mahitaji yake, uwezo tuliokuwa nao hivi sasa hauturuhusu ukilinganisha na matakwa ya kila mmoja wetu katika kuhakikisha kwamba maendeleo ya nchi hii yanapatikana.

Kila mmoja hapa anasema aidha fedha hii itolewe niletewe mimi katika Wilaya kwa sababu ya hili au niletewe mimi katika Jimbo langu kwa sababu ya jambo hili lakini sasa keki iliyokuwepo ni ndogo ukitoa huku utampa nani tuseme ukitoa kwenye Wilaya uipeleke kwenye elimu kwenye Wilaya nako watasema kwa nini ukaitoa kwenye Wilaya yangu kwa mradi huu ukaitoa kwenye elimu?

Kwa hiyo, keki ni ndogo na ndio maana hatujaweza kukamilisha kupata idadi hiyo hasa kama ilivyo sheria. Sheria imetuwekea kiwango tu kwamba mfikie kiwango hiki sio zaidi ya hiki lakini haikusema lazima tupate kiwango kile kwa sababu mahesabu na hadhi ya uchumi wetu bado hatujaweza kufikia hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kufuta Ada ya Miliki ya Mashamba (*Land Rent*) ya Shilingi 200. Miaka miwili iliyopita Serikali ilipunguza Ada ya Miliki ya Ardhi kutoka Sh.600 hadi Sh.200 kwa eka moja baada ya kupata ushauri kutoka kwa wadau mbali mbali ikiwa ni pamoja na ninyi Waheshimiwa Wabunge, hapa hapa Bungeni, wakati tunajadili Bajeti wakati kama huu huu.

Suala la kufuta kodi ya mashamba vile vile lilijadiliwa na Kamati ya Ushauri ya Masuala ya Kodi ambayo ilitafakari kwa makini hali ilivyo sasa baada ya kupunguza kodi hiyo. Maoni ya wadau ni kwamba kitendo cha kufuta kodi ya Sh.200 kinaweza kupelekea baadhi ya wakulima kuhodhi ardhi bila ya kutumia kama ilivyokuwa nchini

Zimbabwe. Ardhi itakuwa haina thamani na hivyo kutothaminisha matumizi yake katika uzalishaji wa mazao.

Mheshimiwa Spika, bado nina imani kwamba kiwango cha Sh.200 ni kidogo na hakitaweza kukwamisha uwekezaji katika kilimo hasa ukizingatia hatua nyingine zilizochukuliwa hapa Bungeni za kuvutia uwekezaji katika kilimo na ufugaji kama alivyoelezea Mheshimiwa Waziri wa Fedha, wakati akiwasilisha Bajeti hii ya mwaka 2004/2005 kwamba utayarishaji wa ardhi sasa hautakuwemo unakuwa na 100% *depression* na unawekwa katika hesabu zako ili hapo baadaye baada ya mavuno au kupata chochote usikatwe kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja ya utekelezaji na ufuatiliaji wa mipango na Bajeti viimarishwe. Nakubaliana kabisa na umuhimu wa kufuatilia utekelezaji wa mipango yetu na Bajeti ya Serikali. Wote tunatambua kwamba Bajeti itakuwa ya manufaa pale tu ambapo itatumika kwa ufanisi kutoa huduma bora kwa wananchi. Kwa sababu hii, Serikali itaendelea kuimarisha eneo hili kwa kufanya ukaguzi wa miradi na matumizi ya kawaida mara kwa mara katika Wizara, Idara, Mkoa na Serikali za Mitaa. Kitengo cha Ukaguzi wa Kitaalam (*Technical Audit Unit*) pamoja na Idara ya Bajeti watafuatilia kwa karibu zaidi utekelezaji wa Bajeti hii ya mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, aidha, Mtandao wa Usimamizi wa Fedha chini ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, utaendelea kutumika kwa kutoa taarifa za matumizi za mara kwa mara ambazo zitasaidia uhibititi na usimamizi wa fedha za Serikali. Vile vile kama ilivyo kawaida yetu kila miezi mitatu tutakuwa tunatoa taarifa ya utekelezaji wa Bajeti hii, wapi bado hatujakamilisha na wapi tutaendelea. Hapo tunatarajia Waheshimiwa Wabunge watatushauri tufanye nini na wapi bado hatujatekeleza matakwa yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kuhusu Wizara ya Viwanda na Biashara kutengewa fedha kidogo pamoja na umuhimu wake kuwa mkubwa katika uchumi wetu. Ni kweli. Lakini Wizara ya Viwanda na Biashara kazi yake kubwa kwanza ni *facilitation, advocacy and regulation* sio wao wenyewe wanakwenda kuanzisha biashara au viwanda.

Kazi zao muhimu ni hizo na wanawezeshwa ili kufanya hizo kazi tatu muhimu na katika hizo vile vile kuna fedha ambazo wanazitumia kutoka Mashirika ya Kimataifa kwa mfano *WTO* na vile vile kuhudhuria mikutano ya Kimataifa na makongamano ambayo yanahusisha maendeleo ya biashara na viwanda kwa jumla kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa mashirika kama vile *TIRDO, CARMATEC, Tembo* na kadhalika. (*Kicheko*)

**MBUNGE FULANI:** Ndovu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Samahani *TEMDO* ndio maana ulimi wangu ulikuwa mzito kutamka neno hili. Mashirika haya yana vyanzo vyao wenyewe kutokana na huduma wanazotoa. Kwa hiyo, mahitaji yao hasa yale yanayolazimika yafanyike na wamekwama kabisa mara nyingi Wizara ya



Fedha inatizama kwa undani na kwa kushauriana na Wizara ya Viwanda na Biashara kuangalia wapi tunaweza kutoa fungu hilo la fedha na kuwasaidia ili wasikwame kabisa lakini mara nyingi hatujawa na matatizo kama haya kwa mashirika haya.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja juu ya ugawaji wa fedha za Halmashauri za Wilaya na miji kwa kutumia *formula*. Kuhusu hili, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba majibu ya hoja hii nina hakika yameandaliwa vizuri na Waziri wa Nchi, Ofisi wa Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Hivyo Waziri atakapowasilisha hotuba yake ya Bajeti ya mwaka huu 2004/2005 atatoa maelezo ya kina kuhusu matumizi ya *formula* katika kugawa fedha na ruzuku za mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, kuhusu malimbikizo ya mishahara na posho za Walimu, Serikali inakiri kwamba hii ni kero na ni kero ambayo tumeitengea fedha kwa kuhakikisha kwamba *increment* iko katika fungu la *increment, promotion* na *arrears* za Walimu na wafanyakazi wote wa Serikali ambao wana matatizo hayo. Kiasi cha shilingi 9,151,000 zimetengwa kwa mwaka huu kwa shughuli hiyo peke yake. Kwa hiyo, fedha hizo zimetengwa na bado Idara ya Utumishi, Wizara ya Elimu na Utamaduni na TAMISEMI wanashirikiana na Wizara ya Fedha kuhakikisha kwamba fedha hizi zinalipwa na zimetengwa katika Bajeti hii na kuanzia Julai, 2004 shughuli hiyo itaanza kuchukua kasi ambayo itatuwezesha kufikia mahali tusiwavunje moyo Walimu na wafanyakazi ambao wanadai madai yao mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu wastaafu kurejeshwa kwenye Daftari la Pensheni, kama nilivyojibu tarehe 8 Juni, 2004 siku ya Jumanne, swali la Mheshimiwa Ali Said Salum, Mbunge wa Ziwani, nilisema kwamba wafanyakazi wastaafu wa mkupuo watarejeshwa kwenye Daftari kuanzia Julai, 2004 ndio fedha zao zimetengwa.

Hotuba ya Bajeti imesema wataanza kulipwa January 2005 hii ina maana hatujatoka kwenye msingi wetu kwamba kuanzia Julai ndio wanaingia kwenye daftari miezi sita ndio analipwa fedha zake kuanzia Julai mpaka Desemba. Kama nilivyosema utaratibu huu bado hatujauondoa kwa sababu unatuweka katika hali nzuri ya kufuatilia mapato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu nyaraka mbalimbali, tuna *except* kuna wastaafu wengine miezi mitatu, minne nyuma kwa mfano Songea, Kagera, Morogoro wamekuja kama Chama cha Wafanyakazi Wastaafu, picha zao, kastaafu mwaka gani na yuko wapi wameshaleta hata kabla tangazo hili halijatangwa.

Ni matumaini yetu na wengine vile vile watakuwa na pengine *salary slip* tutachambua. Rekodi yoyote aliyokuwa nayo mstaafu ailete na Wizara haitomtenga kwamba yeye sio mstaafu. Bila shaka atakuwa na ushahidi kamili na sisi tutakwenda nyuma kwenye rekodi kuangalia kama kweli yule alikuwepo au hakuwepo au kama ni pacha wa yule aliyestaafu au vipi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nisingependa kengele ya pili igonge nikiwa hapa, kwa yale yaliyosalia, nina hakika Mheshimiwa Waziri mwenyewe atakuja kumalizia kutoa

ufafanuzi. Nasema tena naunga mkono hoja zote mbili kwa asilimia 100, ahsanteni. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwa ratiba iliyopangwa kisayansi, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni atakapoitwa mtoa hoja hii ya Bajeti. *(Makofi)*

*(Saa 06.15 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kabla ya yote nitoe shukrani zangu kwako wewe binafsi na kwa Naibu Spika, Juma Akukweti, kwa namna mnavyoendesha Kikao hiki cha Bajeti kwa ujuzi mkubwa na umahiri mkubwa. Mimi nina hakika mazingira uliyoweka yatasaidia Waheshimiwa Wabunge kupiga kura sahihi ambazo ni za kuunga mkono Bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii vile vile kumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Njelu Kasaka na wenzake kwa namna walivyoshirikiana nasi toka mwanzo wa Bajeti hii mpaka hivi leo. Napenda kuwahakikishia kwamba mawazo yao toka ngazi ya Kamati na yale yatakayokuja baadaye wakati tukizungumzia Muswada wa Fedha nitayazingatia. *(Makofi)*

Vile vile nimshukuru Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, kwa mawazo yake mazuri ambayo yote hayo ni ya kufanyia kazi. Kwa sababu Msemaji wa Kambi ya Upinzani alikuwa Naibu Waziri kwenye Wizara ya Fedha nina hakika hatasita kumpigia kura Waziri wake. Kwa sababu mila zetu ndivyo zilivyo, kuna kaka na bwana mdogo. Nina hakika wenzake Wapinzani watamuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niwashukuru wote waliochangia kwa njia mbalimbali wakiwemo waliotoa mawazo yao kwa maandishi na waliotoa michango yao kwa kuzungumza hapa Bungeni. Nami niwataje waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni wengi kidogo kwa hiyo nitaenda mbio, Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Nazir Karamagi, Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mheshimiwa Edward Ndeka, Mheshimiwa Elisa Mollel, Mheshimiwa Fatma Said Ali, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mheshimiwa Edson Halinga, Mheshimiwa Lawrence Gama, Mheshimiwa Ernest Mabina, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Issa Mohammed Suleiman, Mheshimiwa Hashim Saggaf, Mheshimiwa Beatus Magayane, Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou na Mheshimiwa Mgana Msindai.

Wengine ni Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mheshimiwa Isaac Cheyo, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Mwanne Mchamba, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Suleiman Sadiq. (*Makofi*)

Pia Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Mheshimiwa Khalid Suru, Mheshimiwa John Singo, Mheshimiwa Philip Marmo, Mheshimiwa Abdula Lutavi, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Paul Ntwina, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Stanley Kolimba, Mheshimiwa Christopher Wegga, Mheshimiwa Mussa Lupatu, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, Mheshimiwa Talala Mbise, Mheshimiwa Dr. Simon Mbilinyi, Mheshimiwa Dr. William Shija, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Philip Magani, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Mheshimiwa Salome Mbatia, Mheshimiwa Bernadine Ndaboine, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Frank Maghoba na Mheshimiwa Yete Mwalyego. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Dr. Hassy Kitine, Mheshimiwa Ibrahim Marwa, Mheshimiwa Emmanuel Kipole, Mheshimiwa Profesa Juma Mikidadi, Mheshimiwa Damas Nakei, Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mheshimiwa John Mwakipesile, Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Shaibu Ahmada Ameir, Mheshimiwa Ali Machano Mussa, Mheshimiwa Stephen Kahumbi, Mheshimiwa Yussuf Kombo Juma, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Bernard Membe, Mheshimiwa William Kusila, Mheshimiwa Benito Malangalila, Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Balozi Ahmed Hassan Diria na Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella. Jumla ya waliochangia ni Waheshimiwa Wabunge 81 nawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, waliotoa michango yao kwa maandishi ni Mheshimiwa Stephen Kazi, Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mheshimiwa Peter Kabisa, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Balozi Ahmed Hassan Diria, Mheshimiwa *Major* Jesse Makundi, Mheshimiwa Alhaji Shawaji Abdallah, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Masoud Abdulla Salim, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Dr. William Shija, Mheshimiwa Jumanne Hamisi Nguli, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, Mheshimiwa *Capt.*Theodos Kasapira, Mheshimiwa Abdulkarim Shah na Mheshimiwa Lucas Selelii. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Asha Ngede, Mheshimiwa Samwel Chitalilo, Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo, Mheshimiwa Ramadhani Hashim Khalfan, Mheshimiwa Esha Stima, Mheshimiwa Bakar Shamis Faki, Mheshimiwa Sijamini Mohamed Shaame, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Margaret Bwana, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Stephen Kahumbi, Mheshimiwa

Zahor Juma Khamis, Mheshimiwa Lydia Boma, Mheshimiwa Edgar Maokola Majogo, Mheshimiwa Remidius Kissassi, Mheshimiwa Ally Karavina, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa, Mheshimiwa Bujiku Sakila na Mheshimiwa Grace Kiwelu.

Mheshimiwa Spika, hawa wote nawashukuru kwa michango yao. Inaonyesha jinsi hotuba ilivyokuwa inasisimua na kila mtu alitaka aingie kwenye rekodi kwamba naye alishiriki kikamilifu. *(Makofi)*

Ningependa sasa nirejee hoja mbalimbali kwa pamoja kwa sababu ni nyingi sana, kwa hiyo, sitaweza kumjibu mmoja mmoja lakini nitajibu kwa mafungu ya hoja ili kusudi niweze kutenda haki kwa kila mtu.

Hoja ya kwanza ilihusu kilimo, tumekubaliana na Mheshimiwa Charles Keenja kwamba atakapowasilisha hoja yake atajibu maswali yale ambayo zaidi yalikuwa ya kiutendaji, sijui mbolea iliendaje, bei ilikuwaje na mambo ya namna ile atayajibu na yako mengi pamoja na fedha za *STABEX* na mengine mengi namna ile. Hata ile ya zao moja moja, chakula cha njaa yote hayo atayajibu kwa sababu yeye ndiye yuko upande wa utendaji.

Mheshimiwa Spika, mimi nitaeleza nilivyomwezesha ili aweze kufanya kazi na ndiyo maana ya Bajeti. Sasa nimewezechaje kilimo na kilimo hapa ni vitu vitatu. Kilimo chenyewe tunavyokijua, ni mifugo, Ushirika na Masoko ndiyo tafsiri ya kilimo kwenye Bajeti hii.

Kwa hiyo, napenda kusema kwamba kwa maana hiyo Bajeti ya Sekta ya Kilimo imekuwa ikiongezeka kila mwaka kwa muda wa miaka mitano iliyopita. Kila mwaka imekuwa ikiongezeka. Bajeti halisi ya mwaka huu imeongezeka zaidi ya ile ya mwaka 2003 kwa asilimia 18 bila kujumlisha mambo ya chakula cha njaa ambacho kwa mwaka huu kiko kwenye kasma nyingine. Hivyo ukiondoa chakula cha njaa bado Bajeti ya kilimo itaongezeka kwa asilimia 18. Maana yake ni kwamba ni shilingi bilioni 110 mwaka huu ambapo mwaka 2003 ilikuwa shilingi bilioni 93. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa suala la uwezesaji, ukiondoa hizo bilioni 110 ni vitu gani tena vingine vilivyoko kwenye Bajeti hii ambavyo vitawezesha kilimo kweli kuonekana kwamba kinasonga mbele. Kwanza, ni lile nililotaja hapa la ule Mfuko wa kudhamini mazao yanayouzwa nje hasa yale mazao wanayoita *Traditional Crops*. Mfuko ule wa *Export Credit Guarantee Scheme* hasa kwa Vyama vya Ushirika. Mfuko huu mwaka huu una shilingi nyingine bilioni 13 na kwa uzoefu wanajua wenzangu kutoka Mbozi, Mbinga, Mikoa ya Kilimanjaro na kutoka Mikoa mingi yenye mazao yanayouzwa nje walivyofaidika na jambo hili ndilo lililofufua Vyama vya Ushirika. Kwa hiyo, shilingi nyingine bilioni 13.

Mheshimiwa Spika, ziko zile fedha nyingine nilizosema za udhamini wa wafanyabiashara na wazalishaji wadogo wadogo shilingi nyingine bilioni 2. Hizi kwa mkulima zitasaidia hasa atakapokwenda kununua pembejeo kwa ajili ya mazao,

atakavyokwenda kununua hasa matrekta na dawa na hata mbolea. Vyama vya Ushirika na Vyama vilivyongana vikienda kuomba mkopo benki, ule Mfuko utawadhamini. Kwa hiyo, watakwenda benki watapata mkopo mkubwa kwa udhamini huu halafu wanakuja kuuziana wao kwa wao na wanaweza wakaendeleza kilimo chao.

Mheshimiwa Spika, wasisahau nilitangaza hapa kodi zote ndani ya kilimo, *out*. Hivyo ni nafuu kubwa sana na haikubagua mkulima mdogo wala mkubwa, kodi zote za *VAT*, ushuru wa kila namna *out* na nikaahidi kwenye hotuba ile kwamba endapo tutagundua nyingine ambazo labda zilikuwa zimefichama tutaziondoa pia.

Mheshimiwa Spika, nikasema kwamba ili watu waweze kufaidika na utaratibu huu ni vyema utaratibu wa kuanzisha Vyama vya Kuweka na Kukopa vya aina moja ama nyingine ukaendelezwa. Hii ni pamoja na Benki za Wananchi (*Community Banks*) ili kusudi hawa waweze kwenda kwenye benki kukopa fedha *wholesale*, halafu wao wanakuja kukopeshana kwa rejareja. Katika lugha ya kibenki inaitwa *linkage, linking with large banks*. Ni jambo ambalo tunataka kuliimarisha hasa kuanzia sasa na itawezekana kabisa kwa watu wadogo. Ninashukuru kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliosema hapa kwamba fedha hizi za mikopo zitaweza kumuendea mkulima mdogo mdogo kabisa ndani ya vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, najua yote niliyosema kwenye hotuba kwamba nitashugulikia wazo hili la benki na mimi nashukuru kumejitokeza mawazo mawili hapa. Kuna wanaosema hivi, benki hii itamfikiaje mkulima mdogo, njia ni *SACCOS*, Vyama vya Kuweka na Kukopa, *Community Banks* ndiyo njia au *Associations* za aina moja ama nyingine za wakulima. Hilo tutalifanyia kazi wakati wa mwaka huu wa fedha na tumaini langu ni kwamba tutakuja na jibu.

Kwa hiyo, kwa kweli hili ni jambo la kihistoria halijawahi kutokea. Kwa hiyo, nadhani kama alivyokuwa anasema Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda leo asubuhi, tujivunie hilo ambalo tayari tumeshaweka mfukoni. Mbele ya safari tutaendelea kulisahihisha na kuweka mambo bora kwa kushauriana kadri matatizo yatakavyojitokeza. Mwanzo wa maendeleo ndiyo mwanzo pia wa matatizo na ndiyo maana tuko hapa kutatua matatizo hayo. Kusingekuwa na matatizo tungekuja kufanya nini hapa, hapa hakuna mambo ya utalii, hapa kuna matatizo ya kutatua ndiyo maana tuko hapa. (*Makofi/Kicheko*)

Kwa hiyo, huko kwako ukiona yamejitokeza uanze kunieleza nipate kufahamu na mengine mimi nitayasikia, nitayaleta hapa na mengine nitayafikiria nitayaleta hapa ilimradi wote tunaelewa tunataka kwenda wapi. Hii ndiyo *point* kubwa kabisa. Kama nilivyosema hapa kilimo ndiyo uti wa mgongo na Bajeti hii niliyoweka hapa inanzia Wizara, inakwenda katika Mikoa na inakwenda katika Wilaya. Mwaka 2003 Wilaya tulizitengea shilingi bilioni 4 na mwaka huu tumetenga hizo shilingi bilioni 4 na marupurupu yote haya niliyoweka tena. Sasa Mungu akupe nini baada ya hapo, akupe nguvu tu ufanye kazi ya kilimo, hakuna namna nyingine. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema yaliyobaki Mheshimiwa Charles Keenja, tumelewana hivyo kwamba atajibu kwa sababu yeye yuko jikoni zaidi. Mimi nikijidai hapa kujibu mambo ya kilimo nitasema uongo, halafu mtakuja kusema Waziri alisema uongo, mimi ni mtu wa dini siwezi kusema uongo. (*Kicheko*)

**MBUNGE FULANI:** Kaokoka!

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kuna suala la mahusiano na Zanzibar limejitokeza sana hapa. Ningependa tu kusema kwamba kwa kweli ile Tume ya Mheshimiwa William Shellukindo iko kazini na kwa sasa hivi tunaendelea na ile asilimia 4.5. Lakini hii asilimia 4.5 nifafanue jambo moja, natambua kwamba Muungano huu hatuchangiani kwa asilimia, gharama za Muungano hatuchangiani kwa asilimia, SMZ hailipii hili Bunge lakini kuna Waheshimiwa Wabunge hapa Bungeni kutoka SMZ, Majeshi yetu SMZ haichangii, Mambo ya Nje haichangii, lakini wanachangia kwa kupunguza kwenye asilimia ili wapate asilimia 4.5 yaani yanachangia *indirectly*, lakini *cash* hasa ili uweke mfukoni *allowance* na nini inatoka upande wa Tanzania Bara.

Kwa hiyo, hii asilimia 4.5 siyo asilimia 4.5 kavu kavu ina mambo mengi yaliyofichama huko ndani, ni asilimia 4.5 *plus* ile ambayo hawachangii inakuwa *taking into account* ili kusudi labda badala ya kuwa asilimia 7 au 8 inakuwa asilimia 4.5 na hiyo ni makubaliano wala haina mgogoro. Ila tutaendelea kuiangalia. Fedha hizo maana yake ni nini? Kwa mfano, mwaka uliopita walipata shilingi bilioni 10.3 katika Bajeti kutokana na hiyo asilimia 4.5 na mwaka 2004 shilingi bilioni 12 zinatoka kwenye mfuko huku zinakwenda kule. Sasa kama kuna la ziada tutayaangalia mbele ya safari kama nilivyokwishasema. (*Makofi*)

Kuhusu Gesi ya Songo Songo ni kweli kuna utaratibu tuliojiwekea wa kugawana maliasili, petroli, gesi na kadhalika. Sasa hivi fedha zitakazotokana na gesi ya Songo Songo zitatumika kulipia mikopo ya gesi hiyo. Baada ya hapo tutakaa tena tutaangalia jinsi ya kugawana ndivyo itakavyokuwa na yakipatikana mafuta tuseme Pwani ya Pemba au Pwani ya Makunduchi na wapi huko tutagawane hivyo hivyo, maana yakipatikana huku tugawana na yakipatikana kule tugawana ndivyo Katiba inavyosema. Kwa hiyo, tunawatakiya kila la kheri pia wagundue mafuta tugawane na sisi tumeshagundua gesi na *Inshallah* Mungu atawabariki watapata mafuta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu kero kwa wafanyabiashara wa Zanzibar nashukuru Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud yuko hapa Waziri wa Biashara, anaelewa jinsi mwaka 2003 tulivyofanya mikutano kule Zanzibar tukaelewana na wafanyabiashara. Mkutano mmoja kabisa aliuongoza Mheshimiwa Waziri mwenyewe na mikutano hii inaendelea. Sisi tunavyojua hali inazidi kuboreka kutokana na mashauriano wanayoyafanya kati ya *TRA* na wenzetu wa kule Zanzibar. Kwa hiyo, hilo tunalo na tunaendelea kuliboresha.

Mheshimiwa Spika, niseme hili la ushirikishwaji wa wanawake katika Bajeti. Tanzania hapa tunafanya kitu ambacho watu wengi hawafanyi. Kuna kitu kinachoitwa

*Gender Women Mainstreaming*, kila jambo tunalofanya kwenye kila Wizara wanawake wanafaidikaje? Iko Kamati iliyoundwa kabisa na wale watu wa *NGO* ile inayoshughulikia akinamama wanajua hili na mwongozo upo na tunapotoa sisi miongozo ya Bajeti tunaandika kabisa wekeni jinsi wanawake watakvoyofaidika na Bajeti ya Wizara yako.

Kwa hiyo, utaratibu huo upo na tunakutana kila mara moja kwa mwaka tunaita hata hayo makundi ya wanawake ili tuweze kuelewana je, mwaka huu mmeona kasoro gani, semeni ili tusahihishe kwa mwaka ujao. Kwa hiyo, kuhusu hilo msiwe na wasiwasi akinamama mnaweza mkakaa tu, poa sisi tunawashughulikia mambo yenu yatakwenda vizuri. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ni jambo ambalo si kila mtu anafanya, sisi hapa tuna historia ndefu ya kuishi vizuri na akinamama. Kwa hiyo, akinamama na Waheshimiwa Wabunge mnaowakilisha Majimbo hayo waambieni kwamba Serikali yao inawatambua na ni Serikali ya CCM. Jambo hili liko kwenye Ilani na wasiwe na wasiwasi na mimi pia ni mtu ambaye nina mapenzi makubwa na maendeleo ya wanawake na historia yangu inajulikana ila tu sijaandika kitabu na wanawake wanajua na hata Waheshimiwa Wabunge hapa wanajua. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu msamaha wa kodi, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, alikuwa anazungumzia habari za msamaha wa kodi. Ni kweli alivyosema Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, kwa mara ya kwanza tulitoa msamaha wa kodi wakati wa njaa kwa mchele uliokuwa unaagizwa kwa sababu kulikuwepo na wasiwasi mkubwa kwamba kulikuwa hakuna mahindi ya kutosheleza, kulikuwa hakuna mahindi kabisa kwa nchi zinazotuzunguka.

Kwa hiyo, tukaona tuweke na mchele na huo mchele ulisaidia na shahidi ni Mheshimiwa William Lukuvi ambaye alionekana kwenye *Television* akizunguka huko kwenye masoko akiangalia habari ya bei. Alikuta mchele wa kwetu ulikuwa kidogo na ulikuwa unauzwa kwa bei ya juu zaidi, lakini ule mchele mwingine ulikuwa mwingi na ulikuwa unauzwa kwa bei ya chini zaidi. Lakini walaji walikuwa wanachagua. Mimi ningesikitika sana kama walaji wangelalamika kwamba wakitafuta mchele wa shilingi 200/= hawaupati ila ni mchele wa shilingi 700/= tu, kumbe michele yote ilikuwepo na mlaji alichagua alichopenda. Kwa hiyo, ndiyo kilichotokea. Sasa sijui kama bei zilikuja kuwaje kwa kweli mimi nilichofanya ni kuhakikisha kwamba vyakula vya kutosha vipo ndani ya nchi na ndiyo maana ya ule msamaha, mengine yaliyotokea huko sokoni kwa kweli siwezi kujibu maana ule siyo uwanja wangu tena.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo lingine kuhusiana na mahindi. Wale waliokuwa wanasema Tanzania ilikwenda kuomba mahindi Ethiopia tulinunua bwana hatukwenda kuomba. Tulikuwa na fedha tukanunua mahindi Ethiopia, tukanunua mahindi Afrika ya Kusini na tukanunua mahindi katika nchi nyingi na tukanunua mahindi Kenya. Sasa tatizo ni kama kweli umeenda kuomba kwa nchi kama ile, sisi hapa tulikuwa na fedha na nyie mlinipa hizo fedha hapa. Si mlinipa ile fedha mnakumbuka na ndiyo maana nilisema sisi ni nchi yenye stamina, tuna uwezo kwenye Bajeti wa kununua na tunaweza

tukanunua popote palipo na bei nzuri, kama Ethiopia mahindi yalikuwa na bei nzuri niyaache tu kwa sababu ni nchi katika historia ina njaa. Lakini wakati ule ilikuwa na chakula. Kwa hiyo, mimi nilifanya jambo la kiuchumi tu na hakuna wasiwasi mkubwa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu wahakikimali wa Serikali. Kwa Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Wahakikimali wa Serikali kwa kweli ni Mkaguzi Mkuu wa Serikali ndiyo anayeweza kukagua Serikali za Mitaa. Sasa kama mnaona Mhakikimali wa Serikali hasa aingie humo ni suala la kubadilisha tu sheria na mimi nitapeleka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Waziri wa TAMISEMI tuone kama jambo hilo lina busara gani, mimi halinimumizi wala halinimumizi Serikali lakini iko dhana kama Serikali Kuu ikakague Serikali za Mitaa ama namna gani.

Mheshimiwa Spika, kwa nini wawekezaji hawakopi nchini. Wawekezaji walikuwa hawakopi nchini kwa sababu mbili kubwa. Kwanza, benki zetu hizi ni ndogo mno, tena Waheshimiwa Wabunge tumetumia muda mrefu hapa kuzungumzia juu ya benki, mnajua benki hizi ndogo ni matawi ya barabara ndogo ndani ya Wilaya. Lakini hapa inaitwa benki ina kibao kikubwa na Meneja mkubwa anayevaa tai kama mimi hapa. Hizi ni benki ndogo kabisa.

Mimi wakati ule nikiwa Waziri wa Viwanda na Biashara niliua Kiwanda cha Sigara, mimi ndiye niliyeua kile kiwanda. Wale walionunua kile kiwanda Kampuni ya Marekani ikasema fedha yenu iko hapa bilioni 58, lakini tuiweke wapi, benki zenu hizo zikifilisika mtalipwaje hizi bilioni 58, ikabidi tukubaliane hizo fedha ziwekwe kwenye *ESCROW Account*, Ulaya ikawekwa kule ndiyo baadaye ikaja taratibu kwa sababu hizi ni benki ndogo mno ni sawasawa na *SACCOS* ndani ya kijiji, kabisa ni benki ndogo. Lakini sasa zimeanza kuja benki kubwa *Standard Chartered, Barclays, ABSA* hawa ni wakubwa wana *network* ya Kimataifa, wale sasa ndiyo wamekuja na wakaleta ushindani mkubwa hapa. (*Kicheko*)

Kwa hiyo, wawekezaji sasa wameanza kukopa kwenye benki hizo na kwa sababu ushindani ni mkubwa na wenyewe wameanza kuteremsha riba ya kukopa. Kwa hiyo, hali inabadilika na hasa baada ya kubadilisha ile sheria mwaka 2003 ya *reassure* zaidi mabenki nina hakika hata wao wenyewe sasa wameishaanza kukopa kwenye benki zetu. Kwa hiyo, sababu ni hiyo tu kulikuwa hakuna sababu nyingine.

Kwa mfano, mgodi mmoja kama ule wa Kahama au Kiwanda tu kama hicho nilichosema cha Sigara ni shilingi bilioni 58 ni fedha nyingi, lakini benki zote zile zilizojilundika pale Dar es Salaam zina tawi moja moja na zile zilizojitahidi zina tawi Dar es Salaam na lingine Mwanza, zilizojitahidi zina tawi moja Dar es Salaam na lingine Arusha mahali pengine hawana chochote huko yaani kwa lugha ya Kimataifa hizi benki zetu ni sawasawa na *SACCOS* iliyo ndani ya kijiji.

Mheshimiwa Spika, kwa nini asilimia kubwa ya akiba za kigeni iko katika *dollar*. Kulingana na taarifa kutoka Benki Kuu ni kweli kwamba karibu asilimia 67 ya akiba ya fedha za kigeni iko katika *dollar* za Marekani ikifuatiwa na *Euro* asilimia 16, *Yen* ya



Kijapan asilimia 6, *Pound* ya Kiingereza asilimia 6 na sarafu zingine ndogo ndogo asilimia 5. Utaratibu huu unatokana na kwamba kwanza mapato karibu yote ya fedha za kigeni hulipwa kwa *dollar* za Marekani. Pili, malipo mengi ya nje ikiwa ni pamoja na malipo ya madeni, bidhaa na huduma hufanyika kwa *dollar* za Kimerakani na tatu, kutokana na sababu zilizotolewa malipo yote kwenye soko la fedha za kigeni hufanyika kwa *dollar* za kimarekani.

Ningependa kusahihisha shilingi ya Tanzania haikufunganishwa na *dollar*. *It is not pegged to the dollar*. Hii shilingi yetu ni huru kabisa, lakini mnajua maji yanatiririka kwenye mteremko, maji huenda kwenye bonde, sasa bonde liko kwenye *dollar* kwa hiyo, maji yote yataelekea huko ndiyo hiyo tu hakuna kitu kingine cha ziada hata ungekuwa wewe mfanyabiashara ndiyo ungefanya hivyo. Ndiyo maana mnaona *dollar* inavuma zaidi kuliko fedha nyingine. Ingawa kwa sasa hivi *Euro* ina nguvu kuliko *dollar* lakini Taifa halijaathirika kutokana na kupungua kwa thamani ya *dollar* ya Kimarekani kulinganishwa na *Euro*. Ningependa kusesitiza hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu deni la Taifa, kwanza, ningependa tuelewane kidogo. Mfanyabiashara hodari hafanyi biashara kwa fedha zake, narudia tena mfanyabiashara hodari hafanyi biashara kwa fedha zake, anakopa mradi tu yale masharti yawe mazuri na ile ya kwako unaiweka kibindoni. Kidogo yako na kidogo ya kukopa, huwezi kutumia yote na nchi hivyo hivyo. Nchi mahiri hazitumii akiba zake zote, zinakopa na mkopaji mkuu kuliko wakopaji wote duniani ni Serikali ya Marekani. Serikali ya Marekani ni mkopaji mkubwa kabisa kwa sababu ya utaratibu wa kuendesha Serikali tu unakopa tu. La msingi ni nini, usikope kwa bei ya mlevi, maana mlevi anakopa lalala, unakopa kwa bei ambayo inaleta maslahi.

Kwanza ni ya chini yaani wanaita *concessional*. Shahidi wangu hapa ni Mheshimiwa Joseph Mungai, hivi wiki iliyopita tumesaini Mkataba wa Elimu ya Sekondari amekopa kwa asilimia robo tatu ya moja, *three quarter of one percent* mkopo wa Benki ya Dunia. Hivi sasa ninavyozungumza tena kidogo ningeisahau naelekea *BADEA*. Kule nimekwenda kukopa hela za kununua mbolea na dawa, ni kati ya marupurupu ya Waziri Charles Keenja namletea hela hiyo.

Mimi nakwenda kukopa kwa mbolea na dawa ile ni asilimia moja. Mheshimiwa John Magufuli anajua. Hizi barabara zake zote hizi tunazozikopeshea fedha 1%, 2%, 2.5% tunatengenezea barabara. Unaambiwa miaka kumi usilipe na miaka 40 ndiyo umalize kulipa. Wajukuu watalipa, kwanza watakuwa matajiri kuliko sisi tumeshatembea tembea. (*Makofi/Kicheko*)

Kwa hiyo, ukope kwa bei nafuu na ulipe mbele wakati na wewe umeshakufa. Ndiyo siku ya kulipa. Eeh, nchi zote zinaendeshwa hivyo. Kwa hiyo, si lazima kukopa. Jambo hilo kwenye misamiati hii ya kigeni inaitwa *Debt Sustainability*. Jambo kubwa lililo katika ulimwengu huu wa kukopa ni *Debt Sustainability*, kwamba usikope mpaka ufilisike. Kopa ukijua kwamba hata ikifika hiyo miaka 40 nitaweza kulipa. Kwa hiyo, kuna utaalumu. Huo ni utaalumu kabisa na ndiyo maana kwenye ile sheria mliyoipitisha hapa inasema na wewe Waziri wa Fedha usiende kukopa kopa kabla hujashauriwa na

wataalam. Iko ile Kamati ya madeni, kuna Katibu Mkuu wangu na Makatibu Wakuu wengine, kuna Gavana wa Benki na watu wengine wa aina ile, ndiyo wanakaa wanasema hii sawa sawa kopa. Hili Waziri hapana, labda twende tukazungumze zaidi na ndiyo tunavyofanya. Kwa hiyo, *Debt Sustainability* yaani uwezo wako wa kulipa baadaye. Na wala tusishangae wala tusiogope. Kama baada ya kusamehewa madeni tunaendelea kulipa kwani tungefanya nini, lazima tuendeleo kulipa ilimradi ufanye hesabu, ujue uko kuna mtu atakayeweza kulipa.

Hiyo ndiyo hoja na ndivyo ilivyo na watu wote wanaelewa hapa kama Mzee Iddi Simba na watu wengine waliobobea wanajua kabisa haya ninayozungumza. Kwa hiyo, msiwe na wasi wasi. Mwulizeni baada ya hapa. Kwa hiyo, msiwe na wasi wasi, nchi yenu iko imara na tunakopa kwa misingi hiyo na hakuna kutetereka. Kama nilivyosema hapa *circular* imeshatoka ya Rais, hakuna mtu kukopa bila Mheshimiwa Basil Mramba kupiga *tick*. Mramba usiende ukapiga *tick* kama hujashauriwa na ile Kamati. Taratibu oyee!!! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, akiba ya fedha za kigeni ni kubwa mno. Mnajua mara nyingine hili jambo la akiba ya fedha za kigeni watu wanafikiri zimewekwa mahali kama kihenge. Kwanza nieleze sheria iliyounda Benki Kuu ya mwaka 1995 inataka wakati wowote akiba ya fedha za kigeni ndani ya Benki Kuu isipungue miezi minne. Lazima ndani ya Benki Kuu wakati wowote kuwe na akiba isiyopungua uwezo wa kununua bidhaa na huduma ndani ya nchi kwa miezi minne. Hiyo ni sheria. Lakini sisi tunasema tunaweza tukaongeza zaidi. Kiutendaji sisi tunasema miezi sita. Lakini kwa hali halisi hata leo tunavyozungumza miezi minane na nchi nyingi huwa ni mwaka mmoja.

Sisi hapa tunasema miezi nane, lakini tukisema hivyo hatusemi kwamba basi ndiyo hizo fedha zimerundikwa kwa kwenye kihenge na baadaye kwenye jengo kama hili mpaka kule, zinazunguka duniani hizi fedha zina mizunguko huko duniani, lakini ukizihitaji hapo hapo unapiga kidogo zinaingia. Unapiga hivi kidogo zinakwenda huko. Ndiyo mambo ya fedha sasa hiyo ni siku nyingine.

Kwa hiyo, kigezo hiki kinatumika katika nchi nyingi na kinatambuliwa na Shirika la Fedha Duniani. Nchi yenye akiba chini ya hapo huonekana kama vile ina matatizo ya kiuchumi. Nchi ikishahisiwa ina matatizo ya kiuchumi. Kwa mfano, ingefika siku wakaanza kuona eeh, miezi nane inaporomoka, imekuwa minne, imekuwa miwili, unajua kutatokea nini? Watu wote wenye hela nchi hii watahamisha. Watahamisha inaitwa *capital flight*. Hii ilitokea wakati hali ya hatari kule *South East Asia*, Malaysia, Indonesia na Korea Kusini. Wawekezaji wote walihamisha fedha zao wakapeleka Ulaya na Amerika kwa kuhofu kwamba nchi ile sarafu zake zilikuwa zinaporomoka na akiba ya fedha za kigeni ilikuwa inaporomoka ndani ya nchi zile.

Mahathir Mohamed, aliyekuwa Waziri Mkuu wa Malaysia yeye alikuwa mtu mwenye akili kuliko wastani, akazuia akaweka *exchange control*. Ukishakwenda mahali ukakuta nchi ile ina *exchange control* maana ina matatizo ya kiuchumi. Ukishaweka *exchange control* watu hawaamini kwa nini ameweka kizingiti ambapo tunajua sisi

tunaweza tukatoka asubuhi tukaingia usiku, lakini ametuwekea kizingiti ili tusingie usiku aah, wanahamisha fedha kwa *capital flight*.

Kwa hiyo, sio jambo rahisi tu, nilikuwa nazungumzia katika mjadala. Watu wanasema aah, mabepari wanaweka fedha nyingine zinakwenda. Pesa haiendi kwa asiye na pesa. Pesa haipendani na mtu asiye na pesa. Tena hili ni *simple thing in economics*. Watu wote ambao niliwafundisha *fact* hii wakati nikiwa Mkuu wa Mkoa nilifika Vijijini shahidi yangu Mheshimiwa Njelu Kasaka, nikawaambia tu pesa haipendani na maskini. Ndiyo maana kwenye vitabu imeandikwa, aliyenacho ataongezewa na asiyenacho hata kile kidogo atanyang'anywa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu pesa ina hulka, haiendi kwa maskini. Lazima uibembeleze sana ikae mfukoni. Hata ikiingia inaingia asubuhi, jioni inatoka. Kwa hiyo, lazima ukaekae kama tajiri ili fedha yako isikimbie. Tunaitwa nchi maskini lakini kwenye suala hili usiweke weke umaskini. Nilishawahi kusema sawa sawa na kwenda kununua suti Paris. Hata kama huna hela bwana siku moja ununue suti ukae naye angalau mara moja unafua asubuhi, unapasi mchana, unavaa jioni. Usikaekae kama maskini kila wakati fedha itakukimbia. (*Makofi/Kicheko*)

Kuhusu huduma kwa walipa kodi. Hili ni suala linalohusu *TRA*. Mimi ningependa nimshukuru sana Mheshimiwa Profesa Simon Mbilinyi, alilisemea vizuri jambo hili. Kwa kweli namshukuru sana. Sasa niseme hivi ni kweli kabisa kwamba kati ya Mamlaka za Mapato hapa Afrika ya Mashariki, Tanzania ni *number one*. Ya jirani yangu pale mnawajua Wilaya ya Rombo iko wapi kila siku anafukuza Mkurugenzi Mkuu kwa kitu kinachoitwa ufisadi. Wao wana lugha yao ufisadi. Ie nyingine mpakani mwa Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi na ndugu yangu hapa Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, kila siku Tume ya Majaji huchunguza mpaka imefika mahali nadhani sasa wamekwenda kuleta wazungu wawasaidie. Mwanamke tena wamemweka pale ili asaidie saidie kuleta *stability*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hili la kwetu nakwambia lina sifa ya Kimataifa. Mkurugenzi Mkuu wetu *Commissioner General* wa Shirika hilo ndiye Mwenyekiti wa Wakusanya Kodi Wakuu wa *Commonwealth*. Wale wote wako na ndio Mwenyekiti wao. Maana wanamkiri, wana jambo la kujifunza kwake. Lakini sisi hatuna historia ndefu ya mamlaka hii, tuna historia fupi tu. Sijui kama hamuwezi kujua Mheshimiwa Jakaya Kikwete anajua.

Mimi nilikuwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika hilo, kikao cha kwanza Waziri wangu alikuwa Mheshimiwa Jakaya Kikwete. Kikao cha kwanza tumeazimia vunja Shirika hili. Nikatumwa mimi, Mwenyekiti kwenda kwa Waziri, Mheshimiwa Jakaya Kikwete kumwambia Azimio la kwanza la kikao vunja Shirika hili. Mheshimiwa Jakaya Kikwete kweli akavunja kwa sababu nililiona hili ni *non starter*. Mheshimiwa Jakaya Kikwete akavunja ndiyo tukaendelea tukaanzisha Shirika la sasa mahiri lenye mfumo unaoeleweka. Kwa nini nilisema vunja, nilijua hili ilikuwa tu mchezo, lile la kwangu halingefanikiwa. Lakini yaliyokuja nyuma yangu yamefanikiwa. Mimi sasa niko nalo tena naliongoza. Unaona mambo. (*Makofi*)

Sasa naongozaje? Kwanza tuzungumze habari ilivyotokea. Watu waliokuwa Hazina wakati ule mwaka 1995 Idara ya Kodi ndiyo waliokuwa waanzilishi. Lakini wale walikuwa na mambo mengi ilibidi kuwachuja. Wengi walichujwa na wengi waliondoka. Isipokuwa Idara moja ya Forodha ndiyo ilikuwa haina watu kabisa wa kuwapata hivi kwa urahisi maana ile ni kazi ngumu kidogo. Ni kazi ya kitaalamu sana. Wengi walibaki kwenye Idara ya Forodha na ndiyo ilikuwa inazungumzwa juzi ooh, kule forodha, *long room*, kuna ukabila na nini.

Sasa mimi ningependa niseme kwamba Mheshimiwa Mbunge mmoja nadhani alikuwa Mheshimiwa Dr. Ibrahimu Marwa. Juzi alizungumza hapa jambo ambalo mimi limenikera sana kwa sababu mimi najulikana kwa kihistoria. Mimi sio mkabila. Mimi ni mzalendo mwananchi. Mimi ni mwana-CCM, ninaiamini CCM. Kama nilivyosema nina dini wala hakuna hata ungemwuliza Katibu Mkuu wa CCM wanajua kwamba mimi ni mwana-CCM. Mwaka ule wa harakati za upinzani walunifuata wapinzani wakasema unaona bwana wachaga wote wamehama, wanakwenda upinzani, wewe unafanya nini kwanza una gari la zamani.

Nikasema gari langu la zamani litanifikisha tu maana hamjui nilikotoka nalo. Wanasema Mzee panda gari hili lina *video* na kadhalika. Nikasema gari lenu la *video* mwende nalo huko mkifika salama Mungu awabariki. Lakini nabaki na la zamani na Ubunge nikakosa. Nilikosa nikijua kabisa kwa sababu nilipewa kiti cha bure nikakataa. Mimi mwana-CCM hamjui nilitoka wapi na CCM na nitafia humo. Ndiyo ikatokea yale maneno ooh, Mramba amekula matapishi. Sasa ndiyo nakula matapishi na ya kwangu ni matamu zaidi. (*Makofi/Kicheko*)

Kwa hiyo, kuna kitu kwenye kiingereza kinaitwa *innuendo* yaani ile kusemasema kana kwamba fulani kwa sababu amekaa pale ndiyo anajenga jenga mambo ya ovyo ovyo hapana. Mimi niliwahi kumwuliza Mheshimiwa Ibrahimu Marwa siku moja alipotaja jambo hili nipe majina, niambie unamzungumza nani. Akasema aah, mzee unajua hii mambo. Baadaye ikatoka barua iliyoitwa ni barua ya Malalamiko ya Wananchi wa Musoma Mjini. Walikuwa wanalalamika juu ya Shirika hili. Barua hiyo imekwenda kwa Waziri Mkuu, Waziri Mkuu akataka maelezo. Ni barua ndefu sitaki kuisema sana lakini kwa kifupi ilieleza utaratibu wao ukoje, wanavyojijajiri. Kuna Kamati ya Wakurugenzi wa Bodi. Nani Mkurugenzi wa Bodi, Dr. Enos Bukuku ndiyo Mwenyekiti wa hiyo Bodi. Kwenye Bodi ile yuko Mheshimiwa Estherina Kilasi, yuko huko, yuko Mheshimiwa Dr. Raphael Mlolwa yuko hapa, Mbunge wa Kahama sijui leo yuko wapi. Wako kwenye Bodi ile. Waseme hapa kama waliona mimi nikichokonoa kuuliza nani ameingia nani anatoka. Hawa ndio wanawajiri hawa viongozi wa ngazi za juu isipokuwa mmoja Kamishna Mkuu anayeajiriwa na Rais.

Lakini mimi napendekeza na mimi niwaambieni wala sioni aibu kama nilimpendekeza aliyeko sasa kuwa Kamishna Mkuu kwa sababu gani. Sioni aibu kwa sababu gani? Kwa sababu nilimwomba Mwenyekiti. Mimi niliandika barua kwa Mwenyekiti tafuteni watu kule ndani kama hawako mniambie nitangaze. Mwenyekiti akasema tunao wengi. Majina haya, nikasema amueni huko, wakaamua wenyewe. Sasa

wakishaleta jina mimi niseme hapana kwa sababu huyu ni Mchaga! Niseme hivyo?  
(Makofi)

La msingi sio hilo, la msingi je, *is he performing*, anatimiza wajibu au kama hatimizi wajibu wewe mzee tunavyokuletea kwamba huyu hatimizi wajibu unamlinda linda? Kama unamlinda linda, kosa na mimi lazima nilaumiwe, tena niwaambieni. Hilo sasa naliacha twende kwenye Taifa. Kuna watu fulani wenye vipaji na kuna Taasisi moja hapa simuoni Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, leo yeye anaongoza Jeshi.

Mheshimiwa Spika, Mkuu wa Majeshi anatoka Mkoa mmoja na Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, sasa Sarungi aondoke au Mkuu wa Majeshi aondoke?

Juzi Profesa Sarungi amesema hapa kwamba sisi hatuchagui vyeo kwa kufuata mtu anatoka wapi, huko jeshini. Alisema hapa akijibu swali. Kwa hiyo, naomba mniambieni, mimi nina orodha hapa ya Wakuu wote wa Mikoa kwa *TRA*, ya Wakuu wa vitengo mbalimbali ndani ya *TRA* na utaratibu uliotumika. Tena kwanza sio kweli kwamba wamerundikana. Sio kweli kwa mfano kwenye Wilaya Wakuu wale wa Mikoa ni asilimia 15 ndio wametoka Mkoa wa Kilimanjaro ingiza Wapare wote na Wachaga na wengine wanatoka Mkoa ule pamoja na Wahindi na Waarabu wanaoishi Mkoa ule. Eeh, inabidi tuzungumze mambo ya ukabila hapa *is a...*

**WABUNGE FULANI:** Inatosha. (Makofi)

**WAZIRI WA FEDHA:** *TRA* hiyo, sasa inafuata Mpango wa Maendeleo. Katika mpango huo moja kubwa kabisa ninalofanya ni kufanya kazi kwa teknolojia na mmeona wakitangaza. Wanasema sasa tunataka kuingiza *scanner*. Kuna mashine iliyoingia pale Dar es Salaam. Mizigo ikiingia unaweza ukaitazama kama vile unavyotazama kwenye kiwanja cha ndege ndani ya mfuko ukaona kuna kitu gani. Sasa hivi mtu akiingia pale Uwanja wa Ndege wa Dar es Salaam akiwa anazungumza zungumza na wajamaa pale kuna mtu kule anamwona ndani ya *screen* kama *TV* hivi.

Mheshimiwa Spika, tunaboresha na tumeanzisha utaratibu wa kuzungumza na wateja, *point* ya Profesa. Kila mwezi tunazungumza na wateja mnasemaje nani mbaya wenu nini na kadhalika. Wameanzisha utaratibu mwingine wa kuchambua watu wanaolalamikiwa inaitwa *Ethics Committee* huko ndio wanaangalia malalamiko yote ya kikazi na kadhalika. Ziko ngazi mbili au tatu Mkoani na Taifani wanachukua hatua. Nilisema tena siku moja wale ambao wanaonekana ovyo wanawafukuza au wanawachukulia hatua. Wale wanaonekana wanafaa wanasema huyu anafaa na kadhalika. Lakini kama tulivyoona hata kwenye magazeti wiki mbili zilizopita hivi kuna mmoja pale alimwita mhindi akamdai shilingi milioni 10 ili amsamehe sijui kodi ya *VAT* na kadhalika. Kwa mshenzi yule na kwa hiyo Polisi walimkamata. Mimi nasema mfukuzieni huko mbali kwa sababu amekiuka maadili ya kazi. Kwa hiyo, wako wachache ambao tunao bado wanaendelea kutuletea aibu, lakini kuna utaratibu wa kushughulika nao na utaratibu huo ulivyo ni mzuri kabisa.

Mheshimiwa Spika, labda nitangaze hapa hapa niliunganishe. Tunavyozungumza kuna meli kule bandarini ambayo imeingiza mafuta isiruhusiwe kuingia ndani kwa sababu wanasema imekiuka labda taratibu za *standards*. Leo mchana tulipata wawakilishi wenye mafuta wakilalamikia jambo hilo. Tulikutana chini ya uongozi wa Waziri Mkuu na Waziri Mkuu ameniruhusu kwa niaba yake nitangaze ifuatavyo:-

Moja lilikuwa langu kwa sababu niliulizwa hapa. Moja juu ya hizo meli badala ya kuziacha zizagae tu pale na hakuna mtu mwenye uamuzi ziingie ndani ya nchi zimwage mafuta wakati Mawaziri husika wa Viwanda na Biashara na Nishati na Madini wakielewa hili jambo vizuri na kuliwekea msimamo unaoeleweka ndani ya Serikali. Kwa hiyo, wale wanaofanya biashara hiyo hapa kama wako ile meli yenu inaingia wakati wowote kuanzia sasa hivi na msiwe na wasi wasi mnaweza mkalala salama angalau kwa leo usiku. (*Makofi/Kicheko*)

La pili, hawa wenye mafuta wamekuwa wakitulalamikia. Mnakumbuka mwaka 2003 tulisema na limejitokeza hapa. Tulisema kwamba hawa watakapoingiza mafuta katika ule udhibiti ndani ya siku 30 walipe kodi yake. Wamelalamika toka tuachane hapa. Wanalalamika wanataka siku 60. Katika kikao hicho Waziri Mkuu amefanya *compromise* amewaambia na sisi wote tulimshauri Waziri Mkuu tulikuwa kwenye kikao kile cha Mawaziri hapa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwamba sasa tunawapa siku 45 badala ya siku 30 wawe wamelipa kodi zetu. Siku 15 za kwanza walipe asilimia 25, siku 15 zifuatazo asilimia 50 na siku 15 za mwisho walipe asilimia 25. Hiyo ni kwa kutambua kwamba hata sasa hivi kuna vurumai kwenye mafuta na sio wakati mzuri wa kugombana na hawa watu wenye mafuta na hasa kwa sababu bei pia zinazidi kupanda duniani.

Kwa hiyo, liliulizwa hili swali na nalijibu sasa katika fursa hii kwa sababu linaangukia kwenye majukumu ya *TRA*. Mwezi Julai, kile chombo kinaingia, tukifunga na ile hoja kwamba sasa itakuwaje labda tuwe na kituo kimoja tu Dar es Salaam au vituo kadhaa hilo jambo tumelichukua na jana Waziri Mkuu aliita kikao kingine tumelizungumza, tumepeana *homework* tutaliambia kama mafuta yote yaingilie Dar es Salaam au yaingilie wapi na wapi au iweje.

Mheshimiwa Spika, hilo Waziri Mkuu ameshaagiza jana usiku. Wengine hapa hatulali msituone hivi. Tunawafanyieni kazi tu maana mnauliza hapa. Kwa hiyo, nataka muamini kwamba tulikuwa kazini na tumeshamaliza maneno hayo mnaweza mkarudi kule mkawaambia kwamba Serikali yenu ni sikivu kama alivyosema Dr. Abdallah Kigoda, leo. Serikali sikivu hailali. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kulikuweco marejesho ya kodi kwa wale wanaochelewa. Ni kweli kuna malalamiko juu ya urejeshaji wa kodi za aina mbalimbali kama *VAT* na kadhalika hasa kwenye Makampuni makubwa. Nimeunda Kamati wiki mbili zilizopita. Nimeunda Kamati ya wataalamu na Wizara ya Fedha na *TRA* tuweze kuelewana juu ya utaratibu bora zaidi na upesi iwezekanavyo lalamiko hilo litakwisha na tutarudi kwenye utaratibu mzuri.

Mheshimiwa Nimrod Mkonzo, aliuliza swali zuri hapa, je, *VAT* ya wale wananchi wanaojenga shule. Utaratibu wa *VAT* hausamehi mtu mmoja mmoja. Wale watu wa Musoma na wengine wanaotaka wafaidike na misamaha ya *VAT* kwa sababu wanajenga shule na kadhalika Kijijini ni lazima watumie chombo (*NGO*) fulani ili kwa njia hiyo waje sasa waombe hiyo misamaha unayotaka. Kwa sababu kwenye utaratibu wa sheria kuna misamaha ya *NGOs* na misamaha ya Madhehebu lakini hatuna misamaha ya Kijiji wala mtu. Kwa hiyo, kama mnataka kufaidika sasa hivi waende hivyo mbele ya safari tutaangalia tena njia bora zaidi na iweje.

Kuna marekebisha ya viwango vya kodi. Nitaomba msamaha kwamba kwenye hotuba yangu vile viwango nilivyokuwa nimeweka vya kodi za hawa watu wadogo wadogo ukurasa 49 kule mwisho kabisa *paragraph* 45 kuna vile viwango nilivyoweka vya kodi za wale watu wadogo. Namshukuru sana Mheshimiwa Herbert Mntangi, alisahihisha tena kwenye mchango wake. Ni kweli kulikuwako hilo kosa hata mimi nililiona siku ile nikisoma.

Nililiona, tulishajua lakini tulishachapisha. Kwa hiyo, tutaleta masahihisho kwenye *Finance Bill* itakapokuja. Lakini masahihisho yale kimsingi pale ambapo mtu ambaye haweki kumbukumbu atalipa shilingi 35,000. Sasa yule mwenye kumbukumbu atalipa shilingi 33,000. Bila kumbukumbu shilingi 95,000 na kumbukumbu shilingi 85,000. Bila kumbukumbu shilingi 291,000 na kumbukumbu shilingi 290,000. Bila kumbukumbu shilingi 520,000 na kumbukumbu shilingi 458,000.

Kama nilivyosema utaratibu huu unampendelea anayeweka kumbukumbu. Sasa tunataka watu waweke kumbukumbu. Unamwadhibu kidogo asiyeweka kumbukumbu. Lakini wote wana nafuu vyovyote vile iwavyo ana nafuu kuliko zamani, akilipa kodi hii pamoja na *stamp duty*. Kwa hiyo, hii ndiyo nafuu kwa wote hawa awe na kumbukumbu asiwe na kumbukumbu na nitaleta mabadiliko haya na mengine madogo madogo katika *Finance Bill* ambayo nitaitangaza na mtaiona itakapokuja wakati wake mwisho wa kipindi hiki.

Kuhusu mrabaha wa madini, msamaha wa pili. Naomba msamaha kwa sababu nimetumia neno baya. Kwenye hotuba hii nimetumia neno baya la mrabaha. Sikuwa na nia ya mrabaha

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kumalizika)*

**SPIKA:** Malizia hotuba yako kwa utulivu, usisikilize hiyo kengele.

**WAZIRI WA FEDHA:** Sikuwa na nia ya mrabaha kwa sababu mrabaha ule wa asilimia 3 kwenye madini hayo unalipwa sasa hivi. Unalipwa kwa Mheshimiwa Daniel Yona. Tayari unalipwa asilimia 3 huko. Unalipwa kwenye Jasi, *Pozzolana* na Chokaa, unalipwa.

Mheshimiwa Spika, nilichokuwa nataka mimi kufanya ni kusema *cess* maana yake ile sheria ya mwaka jana tuliyoibadilisha ilikuwa juu ya *cess*, ushuru kodi zile

ambazo tulifuta tukasema ni za kero. Hiyo kwa sababu wameilalamikia na nina barua hapa zile Halmashauri zimenilalamikia. Ni kodi kwa wale wanaochimba na ndiyo maana kwenye hotuba nikataja kwamba ni mali ghafi ya viwanda. Sasa kwa sababu hali ya hewa imeshaharibika iwe kweli isiwe kweli naondoa ile.

Mheshimiwa Spika, lakini nataka nisahihishe hilo tu kwamba sikuwa nazungumzia habari za mrabaha kwa sababu walikuwa wanalipa tayari nilikuwa nazungumza hawa warejeshewe kodi yao tuliyokuwa tumeifuta kwa makosa mwaka jana. Lakini kwa sababu hali ya hewa imeshaharibika mimi nasema naondoa hiyo mpaka ile Tume inayochunguza jambo lote hili ikamilishe shughuli na ilete jambo zima ambalo limekamilika kama ni udongo kama ni dhahabu au chochote. (*Makofi*)

Lile la *television*, hili la *television* haikuwa nia yangu wala Serikali kwa ujumla kutoza kodi ule ushuru wa 5% kwenye vile vi-*television* vidogo vidogo vya watu, Halmashauri za Vijiji sio hizo. Wako wazito ndio tunawatafuta. Kwa hiyo, zile za Halmashauri zitaendelea kama ilivyo. Nilitaka niseme hivyo tu Manispaa, Jiji, Halmashauri za Miji hizo zitaendelea kama zilivyo. Vile vile mtaelewa sasa nimerudi kwenye *Finance Bill*.

Mheshimiwa Spika, la tatu kwenye *Finance Bill* ni lile la *Visa*. Tulikuwa tumesahau kitu kinachoitwa *Multiple Visa*. Kuna *Visa* za kibiashara na *Visa* nyingine zinazoitwa *Multiple Visa* yaani yule mtu anaingia na kutoka mara nyingi sana ndani ya nchi kumbe huwa na utaratibu tofauti.

Mheshimiwa Spika, sasa tunapendekeza upya kwamba kile kiwango tulichokuwa tumeweka cha dola 50 kwa *Visa* za kawaida zibaki lakini kwa hizi za kuingia na kutoka, zisiwe *double*. Kwa sababu kwa kawaida huwa zinakuwa juu sana. Zilikuwa zaidi ya 200, juu zaidi ilikuwa 500 huko.

Kwa hiyo, tunapendekeza hiyo ya kwanza iwe kama ilivyokuwa nilivyoomba hapa na hii ya pili ya *Multiple Visa* iwe dola za Kimarekani 100 na iwe kati ya miezi 6 na 12. Hili tutalileta tofauti na watu wa Wizara ya Mambo ya Ndani tunawashukuru walikuja kutusaidia kusema kuna kitu kingine ambacho tulikuwa tumesahau.

Mheshimiwa Spika, labda nimalizie tu kwa kusema kwamba mimi nimefarijika sana kwa jinsi mjadala huu ulivyokwenda. Kwa sababu umefanyika kwa uelewa mkubwa na mimi nimejifunza jinsi Waheshimiwa Wabunge hapa wanavyoelewa kilimo. Waheshimiwa Wabunge wanaelewa sana mambo ya kilimo hapa. Hilo moja nakiri na mambo mengine ya uchumi.

Naomba tu kitu kimoja nimejifunza mengi. *Book* hili ni nusu ya mambo niliyoandika tutakwenda kuyafanyia kazi. Kama ilivyo kawaida yangu maana mimi sisemi kitu ambacho siwezi kufanya. Mnanielewa nikishasema nakwenda kufanya kazi maana yake nakwenda kufanyia kazi mengi na mazuri.

Ningependa kuendelea kusema pale ambapo mnaona mna mawazo ya ziada hata baada ya kutoka hapa endeleeni kuwasiliana nami kwa sababu kila mwisho wa Bajeti ni



mwanzo wa Bajeti ijayo. Mwaka ujao wale wanaosema kwamba Bajeti hii ni porojo sasa wanaelewa na wale wanaosema kwamba Bajeti hii iliwekwa eti ili kuifagilia CCM na hasa ile ya ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kweli kama ilivyokuwa, mkubwa mmoja wa Chama kimoja amepata matatizo huko kwenye ziara. Hebu fikiria hiyo sasa hivi kama ni fujo tu ilitokea au akapigwa pigwa na nini, tuseme angekatwa masikio na pua wakati na yeye anataka kuwa Rais wa nchi hii, unajua ingekuwa ndiyo mwisho hata wa kufikiria jambo hilo.

Kwa hiyo, mambo haya tunayasema sema kwa utani, lakini nia yetu sisi siyo kumsaidia mtu yeyote kushinda au mtu yeyote kutoshinda. Nia yetu ni kuhakikisha kwamba watu hawatakatwa masikio wala kichwa, wala miguu na kwamba Polisi wakiitwa wanakwenda haraka *rapid deployment* na wana vyombo vya kwenda kukabiliana na *army*. Hiyo ndiyo nia yetu tu. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia kuna li-*book* hili tunalozungumzia, lile ni *book* la mabilioni ya pesa, *voters register* ni la mabilioni, ni lazima tuweke pale.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kuna Wilaya ambayo *OCD* peke yake ndiyo mwenye gari ukimuita ukasema kumetokea tatizo hapa anakuuliza una gari? Kama unalo uje unichukue. Sasa, Polisi gani hao? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ndiyo, mnajua wengi hapa wanalalamikia mambo haya, kwa hiyo, tunataka kujiandaa siyo tu mpaka mwaka ujao, kuanzia Bajeti hii Polisi wawe wamekaa imara na kukitokea jambo lolote la aina yoyote wawe tayari kwenda usiku, wawe tayari kwenda mchana na siyo gari moja kwa Wilaya, hata mbili hata tatu na wakae wametulizana. Ndiyo kazi tunayofanya hapa. Kwa hiyo, sasa wale wanaosema hii ni porojo, wewe ni Hakimu wa ajabu anayeamua kesi kabla hajasikiliza mashahidi. Ni Hakimu wa ajabu kabisa, hiyo porojo nani ame-*improve*? Tukutane hapa mwaka ujao tuambizane ilikuwa porojo ama ilikuwa ndiyo yenyewe? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mtu mzima kabisa anaweza akaandika porojo za namna hii? Halafu mimi huo uchawi nimeununua wapi wa kudanganya watu wote hawa kwa porojo? Watu wote wenye akili hapa niwadanganye kwa porojo, haiwezekani! Kwa hiyo, nipeni ruksa nikafanye kazi na hayo mliyosema niyamalize. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba Bajeti hii ilivyo mia kwa mia na hao wenzangu wa Upinzani mie nawaheshimu sana wana kazi ya kufanya, lakini siyo lazima kila wakati *no, no, no*. Kuna *no, yes* na leo ni *yes*. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja tena. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, umefika wakati sasa wa kuamua kupitisha au kutokupitisha Bajeti ya Serikali. Kwa utaratibu wetu nitamtaka *Sergeant-at-Arms* apige

kengele kwa dakika moja ili kuwajulisha waliopo nje kwamba sasa tunaanza kazi ya kupiga kura.

*(Hapa kengele ilipigwa ili Waheshimiwa Wabunge waliopo nje ya Ukumbi waingine ndani ya Ukumbi wa Bunge)*

*(Hapa upigaji kura kwa kutaja majina ulianza)*

Mheshimiwa Frederick T. Sumaye	-	Ndiyo
Mheshimiwa William V. Lukuvi	-	Ndiyo
Mheshimiwa Anna Margareth Abdallah	-	Ndiyo
Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib	-	Ndiyo
Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete	-	Ndiyo
Mheshimiwa Zakia Hamdan Meghji	-	Ndiyo
Mheshimiwa Balozi Dr. Pius Y. Ng'wandu	-	Ndiyo
Mheshimiwa Edgar D. Maokola-Majogo	-	Ndiyo
Mheshimiwa Daniel Ndhira Yona	-	Ndiyo
Mheshimiwa Harith B. Mwapachu	-	Ndiyo
Mheshimiwa Gideon Asimulike Cheyo	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda	-	Ndiyo
Mheshimiwa Prof. Juma Athumani Kapuya	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Mary M. Nagu	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Edward N. Lowassa	-	Ndiyo
Mheshimiwa Wilson M. Masilingi	-	Ndiyo
Mheshimiwa John P. J. Magufuli	-	Ndiyo
Mheshimiwa Basil P. Mramba	-	Ndiyo
Mheshimiwa Prof. Pillemon M. Sarungi	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri	-	Ndiyo
Mheshimiwa Charles N. Keenja	-	Ndiyo
Mheshimiwa Prof. Mark J. Mwandosya	-	Ndiyo
Mheshimiwa Joseph J. Mungai	-	Ndiyo
Mheshimiwa Arcado D. Ntagazwa	-	Ndiyo
Mheshimiwa Brig. Jen. Hassan Ngwilizi	-	Ndiyo
Mheshimiwa Balozi George C. Kahama	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Dr. Asha-Rose M. Migiro	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Juma Alifa Ngasongwa	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Andrew John Chenge	-	Ndiyo
Mheshimiwa Juma J. Akukweti	-	Ndiyo
Mheshimiwa Shamim Parkar Khan	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatibu	-	Ndiyo
Mheshimiwa Tatu Mussa Ntimizi	-	Ndiyo
Mheshimiwa Prof. Pius P. Mbawala	-	Ndiyo
Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir	-	Ndiyo
Mheshimiwa Bujiku K. Sakila	-	Ndiyo
Mheshimiwa Mizengo K. P. Pinda	-	Ndiyo
Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita	-	Ndiyo

Mheshimiwa Capt. John Z. Chiligati	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. R. Msabaha	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Hussein Alli Mwinyi	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Hezekiah N. Chibulunje	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha	-	Ndiyo
Mheshimiwa Anthony M. Diallo	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Abdulkader A. M. Shareef	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Rita Louise Mlaki	-	Ndiyo
Mheshimiwa Njelu E. M. Kasaka	-	Ndiyo
Mheshimiwa Athumani S. M. Janguo	-	Ndiyo
Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed	-	Hakuwepo
Mheshimiwa William H. Shellukindo	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. William F. Shija	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. John Samwel Malecela	-	Ndiyo
Mheshimiwa Eliachim J. Simpasa	-	Ndiyo
Mheshimiwa Omar S. Kwaangw'	-	Ndiyo
Mheshimiwa Anne S. Makinda	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Sophia M. Simba	-	Ndiyo
Mheshimiwa Mgana I. Msindai	-	Ndiyo
Mheshimiwa Prof. Henry R. Mgombelo	-	Ndiyo
Mheshimiwa Wilfred Muganyizi Lwakatare	-	<i>Abstain</i>
Mheshimiwa Isaac M. Cheyo	-	<i>Abstain</i>
Mheshimiwa Thomas Ngawaiya	-	<i>Abstain</i>
Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa	-	<i>Abstain</i>
Mheshimiwa Muttamwega B. Mgaywa	-	<i>Abstain</i>
Mheshimiwa Pillemon Ndesamburo	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Benedicto M. Mutungirehi	-	<i>Abstain</i>
Mheshimiwa Ali Said Juma	-	<i>Abstain</i>
Mheshimiwa Dr. Willbrod P. Slaa	-	<i>Abstain</i>
Mheshimiwa Ali Said Salim	-	<i>Abstain</i>
Mheshimiwa Adelastela E. Mkilindi	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Grace S. Kiwelu	-	<i>Abstain</i>
Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha	-	<i>Abstain</i>
Mheshimiwa Shoka Khamis Juma	-	<i>Abstain</i>
Mheshimiwa Mohamed Juma Khatib	-	<i>Abstain</i>
Mheshimiwa <i>Major</i> Jesse J. Makundi	-	<i>Abstain</i>
Mheshimiwa Frank G. Maghoba	-	<i>Abstain</i>
Mheshimiwa Bakari Shamis Faki	-	<i>Abstain</i>
Mheshimiwa Khamis Ali Saleh	-	<i>Abstain</i>
Mheshimiwa Karim Said Othman	-	<i>Abstain</i>
Mheshimiwa Dr. Amani W. A. Kabourou	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Aisha Phillipa Magina	-	<i>Abstain</i>
Mheshimiwa Teddy Louise Kasella-Bantu	-	<i>Abstain</i>
Mhe. Freeman Aikaeli Mbowe	-	Hakuwepo

Mheshimiwa Masoud Abdulla Salim	-	<i>Abstain</i>
Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah	-	Ndiyo
Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah	-	Ndiyo
Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah	-	Ndiyo
Mheshimiwa Mohamed A. Abdulaziz	-	Ndiyo
Mheshimiwa Bahati Ali Abeid	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud	-	Ndiyo
Mheshimiwa Kijakazi Khamis Ali	-	Ndiyo
Mheshimiwa Omar Mjaka Ali	-	Ndiyo
Mheshimiwa Salim Omar Ali	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Fatma Said Ali	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Khamis Salum Ali	-	Ndiyo
Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali	-	Ndiyo
Mheshimiwa Mohamed Abdully Ally	-	Ndiyo
Mheshimiwa Shaibu Ahmada Ameir	-	Ndiyo
Mheshimiwa. Kheri Khatib Ameir	-	Ndiyo
Mheshimiwa Rostam Aziz	-	Ndiyo
Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar	-	Ndiyo
Mheshimiwa Elizabeth N. Batenga	-	Ndiyo
Mheshimiwa Joel Nkaya Bendera	-	Ndiyo
Mheshimiwa Lydia Thecla Boma	-	Ndiyo
Mheshimiwa Zamda S. Bozzen	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Dr. Batilda Salha Burian	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Robert Jacob Buzuka	-	Ndiyo
Mheshimiwa Margareth J. Bwana	-	Ndiyo
Mheshimiwa Kisyeri W. Chambiri	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Aaron D. Chiduo	-	Ndiyo
Mheshimiwa Diana M. Chilolo	-	Ndiyo
Mheshimiwa Samwel M. Chitalilo	-	Ndiyo
Mheshimiwa Anatory K. Choya	-	Ndiyo
Mheshimiwa Omar Said Chubi	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Paschal C. Degera	-	Ndiyo
Mheshimiwa Leonard N. Derefa	-	Ndiyo
Mheshimiwa Balози Ahmed Hassan Diria	-	Ndiyo
Mheshimiwa Abdullatif Hussein Esmail	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Abdallah Khamis Feruzi	-	Ndiyo
Mheshimiwa Chifu Abdallah Fundikira	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Zainab A. Gama	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Lawrence M. Gama	-	Ndiyo
Mheshimiwa Lephy Benjamin Gembe	-	Ndiyo
Mheshimiwa Jina Khatib Haji	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji	-	Ndiyo
Mheshimiwa Ussi Yahaya Haji	-	Ndiyo
Mheshimiwa Edson M. Halinga	-	Ndiyo

Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan	-	Ndiyo
Mheshimiwa Salama Khamis Islam	-	Ndiyo
Mheshimiwa Yahya Kassim Issa	-	Ndiyo
Mheshimiwa Ismail J. R. Iwvatta	-	Ndiyo
Mheshimiwa Yussuf Kombo Juma	-	Ndiyo
Mheshimiwa Peter Kabisa	-	Ndiyo
Mheshimiwa Charles H. Kagonji	-	Ndiyo
Mheshimiwa Janet Bina Kahama	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Rhoda L. Kahatano	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Stephen M. Kahumbi	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Diodorus B. Kamala	-	Ndiyo
Mheshimiwa Nazir M. Karamagi	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Ally A. Karavina	-	Ndiyo
Mheshimiwa Capt. Theodos J. Kasapira	-	Ndiyo
Mheshimiwa Stephen M. Kazi	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Ramadhani H. Khalfan	-	Ndiyo
Mheshimiwa Zahor Juma Khamis	-	Ndiyo
Mheshimiwa Sharifa Mbarouk Khamis	-	Ndiyo
Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib	-	Ndiyo
Mheshimiwa Juma S. Kidunda	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Aisha O. Kigoda	-	Ndiyo
Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo	-	Ndiyo
Mheshimiwa Estherina Kilasi	-	Ndiyo
Mheshimiwa Halima Omar Kimbau	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Paul P. Kimiti	-	Ndiyo
Mheshimiwa Emmanuel Enock Kipole	-	Ndiyo
Mheshimiwa Remidius E. Kissassi	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Hassy H. B. Kitine	-	Ndiyo
Mheshimiwa Abu T. Kiwanga	-	Ndiyo
Mheshimiwa Stanley Haule Kolimba	-	Ndiyo
Mheshimiwa Mwanamkuu Makame Kombo	-	Ndiyo
Mheshimiwa Parseko V. Kone	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Hadija Kasola Kusaga	-	Ndiyo
Mheshimiwa William J. Kusila	-	Ndiyo
Mheshimiwa Lekule M. Laizer	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Masumbuko R. M. Lamwai	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Benedict K. Losurutia	-	Ndiyo
Mheshimiwa George M. Lubeleje	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Thadeus M. Luoga	-	Ndiyo
Mheshimiwa Musa A. Lupatu	-	Ndiyo
Mheshimiwa Abdula Suleiman Lutavi	-	Ndiyo
Mheshimiwa Ernest G. Mabina	-	Ndiyo
Mheshimiwa Philip Alfred Magani	-	Ndiyo
Mheshimiwa Beatus R. Magayane	-	Ndiyo
Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe	-	Hakuwepo

Mheshimiwa Dr. Milton M. Mahanga	-	Ndiyo
Mheshimiwa Mwanaidi Hassan Makame	-	Ndiyo
Mheshimiwa Danhi B. Makanga	-	Ndiyo
Mheshimiwa Paul Ng'wala Makolo	-	Ndiyo
Mheshimiwa Jackson M. Makwetta	-	Ndiyo
Mheshimiwa Benito W. Malangalila	-	Ndiyo
Mheshimiwa Anne Kilango Malecela	-	Ndiyo
Mheshimiwa Philip S. Marmo	-	Ndiyo
Mheshimiwa Ibrahimu W. Marwa	-	Ndiyo
Mheshimiwa Robert K. Mashala	-	Ndiyo
Mheshimiwa Janeth E. Mashele	-	<i>Abstain</i>
Mheshimiwa Haroub Said Masoud	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Chegeni R. Masunga	-	Ndiyo
Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Halimenshi K. R. Mayonga	-	Ndiyo
Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia	-	Ndiyo
Mheshimiwa Monica N. Mbega	-	Ndiyo
Mheshimiwa Prof. Simon M. Mbilinyi	-	Ndiyo
Mheshimiwa Talala B. Mbise	-	Ndiyo
Mheshimiwa Bakari Muhema Mbonde	-	Ndiyo
Mheshimiwa Mchande Salim Mchande	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba	-	Ndiyo
Mheshimiwa Bernard K. Membe	-	Ndiyo
Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki	-	Ndiyo
Mheshimiwa Fete Saad Mgeni	-	Ndiyo
Mheshimiwa Jenista J. Mhagama	-	Ndiyo
Mheshimiwa Prof. Juma Mtupa Mikidadi	-	Ndiyo
Mheshimiwa Mohamed H. Missanga	-	Ndiyo
Mheshimiwa Margareth A. Mkanga	-	Ndiyo
Mheshimiwa Nimrod E. Mkono	-	Ndiyo
Mheshimiwa George F. Mlawa	-	Ndiyo
Mheshimiwa Oscar T. Mloka	-	Ndiyo
Mheshimiwa Raphael Mlolwa	-	Ndiyo
Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o	-	Ndiyo
Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed	-	Ndiyo
Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed	-	Ndiyo
Mheshimiwa Sumri A. S. Mohamed	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Elisa D. Mollel	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Balozzi Getrude I. Mongella	-	Ndiyo
Mheshimiwa Alhaji Ahamadi H. Mpeme	-	Ndiyo
Mheshimiwa Benson M. Mpesya	-	Ndiyo
Mheshimiwa Kilontsi M. M. Mporogomyi	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Felix C. Mrema	-	Ndiyo
Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Ruth B. Msafiri	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. James A. Msekela	-	Ndiyo

Mheshimiwa Herbert J. Mntangi	-	Ndiyo
Mheshimiwa Jeremiah J. Mulyambatte	-	Ndiyo
Mheshimiwa Hasnain Mohamed Murji	-	Hakuwepo
Mheshimiwa James P. Musalika	-	Ndiyo
Mheshimiwa Ali Machano Mussa	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Ali Sheha Mussa	-	Ndiyo
Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa	-	Ndiyo
Mheshimiwa Frank M. Mussati	-	Ndiyo
Mheshimiwa Prof. Daimon M. Mwaga	-	Ndiyo
Mheshimiwa John L. Mwakipesile	-	Ndiyo
Mheshimiwa Prof. David H. Mwakyusa	-	Ndiyo
Mheshimiwa Yete S. Mwalyego	-	Ndiyo
Mheshimiwa Venance M. Mwamoto	-	Ndiyo
Mheshimiwa Mbaruk K. Mwandoro	-	Ndiyo
Mheshimiwa Shamsa S. Mwangunga	-	Ndiyo
Mheshimiwa Ludovick J. Mwananzila	-	Ndiyo
Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri	-	Ndiyo
Mheshimiwa Omar M. Mwenda	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Damas P. Nakei	-	Ndiyo
Mheshimiwa Abdillahi O. Namkulala	-	Ndiyo
Mheshimiwa Bernadine R. Ndaboine	-	Ndiyo
Mheshimiwa Richard M. Ndassa	-	Ndiyo
Mheshimiwa Edward N. Ndeka	-	Ndiyo
Mheshimiwa Job Y. Ndugai	-	Ndiyo
Mheshimiwa Asha Ali Ngede	-	<i>Yes</i>
Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye	-	Ndiyo
Mheshimiwa Khadija Saleh Ngozi	-	Ndiyo
Mheshimiwa Jumanne Hamisi Nguli	-	Ndiyo
Mheshimiwa Ireneus Ndunguru Ngwatura	-	Ndiyo
Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga	-	Ndiyo
Mheshimiwa Said J. Nkumba	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. Lucy S. Nkya	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Paul E. Ntwina	-	Ndiyo
Mheshimiwa Tembe K. Nyaburi	-	Ndiyo
Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami	-	Ndiyo
Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa	-	Ndiyo
Mheshimiwa Rosemary H. K. Nyerere	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Thomas S. Nyimbo	-	Ndiyo
Mheshimiwa Mathew Taki Ole-Timan	-	Ndiyo
Mheshimiwa Omar Juma Omar	-	<i>Abstain</i>
Mheshimiwa Dr. Suleiman Juma Omar	-	Hakuwepo

Mheshimiwa Ramadhani Nyonje Pandu	-	Ndiyo
Mheshimiwa Semindu K. Pawa	-	Ndiyo
Mheshimiwa Mwaka Abraham Ramadhani	-	Ndiyo
Mheshimiwa Faustine Kabuzi Rwilomba	-	Ndiyo
Mheshimiwa Suleiman Ahmed Sadiq	-	Ndiyo
Mheshimiwa Hashim A. Z. Saggaf	-	Ndiyo
Mheshimiwa Mohamed Ali Said	-	<i>Abstain</i>
Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh	-	Ndiyo
Mheshimiwa Issa Mohamed Salim	-	Ndiyo
Mheshimiwa Gwassa A. Sebabili	-	Ndiyo
Mheshimiwa Lucas L. Selelii	-	Ndiyo
Mheshimiwa Haji Juma Sereweji	-	Ndiyo
Mheshimiwa Sijamini Mohamed Shaame	-	Ndiyo
Mheshimiwa Abdulkarim E. H. Shah	-	Ndiyo
Mheshimiwa Leonard M. Shango	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Henry D. Shekiffu	-	Ndiyo
Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti	-	Hakuwepo
Mheshimiwa Iddi M. Simba	-	Ndiyo
Mheshimiwa John E. Singo	-	Ndiyo
Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud	-	Ndiyo
Mheshimiwa Esha Hassan Stima	-	Ndiyo
Mheshimiwa Issa Mohammed Suleiman	-	Ndiyo
Mheshimiwa Khalid S. Suru	-	Ndiyo
Mheshimiwa Aridi Mwananche Uledi	-	Ndiyo
Mheshimiwa Dr. James M. Wanyancha	-	Ndiyo
Mheshimiwa Maria D. Watondoha	-	Ndiyo
Mheshimiwa Christopher S. Wegga	-	Ndiyo
Mheshimiwa Martha Michael Wejja	-	Ndiyo
Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir	-	Ndiyo

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Makatibu Mezani, sasa watahesabu kura halafu tutatangaza matokeo. (*Makofi*)

(*Hapa Makatibu Mezani walihesabu kura kama zilivyopigwa na Waheshimiwa Wabunge*)  
(*Matokea ya kura*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja ilikuwa ni kwamba, Bunge hili likubali kupitisha Bajeti ya Serikali ya mwaka 2004/2005 ambao hawakupiga kura upande wowote, waliosema *abstain* walikuwa 24, ambao walisema hapana hakuna hata mmoja, ambao hawakuwepo Bungeni kwa sababu hawapo Dodoma ni 48 na waliosema ndiyo ni 222. Kwa hiyo, natangaza kwamba Bunge hili limepitisha Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2004/2005. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kufika hatua hiyo, sasa Bunge linaahirishwa hadi siku ya Jumatatu saa tatu asubuhi.



*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka  
2004/2005 yalipitishwa na Bunge)*

*(Saa 12.27 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu,  
tarehe 21 Juni, 2004 Saa Tatu Asubuhi)*

